**5 FEBRUARI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 5 Februari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Na. 67

**Kuongeza kiwango cha malipo ya pensheni kwa wastaafu**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, lini kanuni mpya za malipo ya pensheni kwa wastaafu ya kila mwezi ya kutoka asilimia 50 mpaka 67 zitaanza kutumika?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Gazeti la Serikali Na. 357 la tarehe 20 Mei, 2022 lilitangaza Kanuni Mpya ya Mafao ambayo iliboresha kiwango cha mafao ya pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu kutoka asilimia 50 iliyokuwa ikilipwa awali na kuwa asilimia 67. Matumizi ya Kanuni hizo yalianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizo ziliandaliwa kwa kushirikisha wadau wote muhimu (wadau upande wa Serikali, Wafanyakazi na Waajiri) kwa lengo la kufanya maboresho ya

Pensheni ili kuyaainisha mafao ya wanachama na kuifanya mifuko kuwa endelevu, ahsante.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado kuna baadhi ya wastaafu wanalalamika kwamba hawapati hayo mafao yao. Pia wastaafu ambao wapo Zanzibar tayari wameshaongezewa, kutokana na kiwango walichokuwa wanapata kimeongezewa.

Je, Serikali ina mpango gani hapa kwetu Tanzania Bara ili na wenyewe waweze kuongezewa hayo mafao?

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la kwamba kuna watu ambao hawapati. Lazima tukiri na kuwa wawazi kwa kazi nzuri ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, kulikuwa kuna changamoto kubwa awali na tunakiri hilo kwa sababu ya mifuko kuwa mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tulijaribu kufanya ile *harmonization,* ambayo ilipelekea kwenda kutengeneza mfumo huu wa kikokotoo kipya ambapo kwa sasa ukiangalia mkupuo wa mafao tunalipa kwa asilimia 50 mpaka 67 na ile pensheni ya kila mwezi imetoka asilimia 25 kwenda 33. Sasa malipo hayo kwa sasa mifuko imekuwa ikilipa ndani ya siku 30. Inalipwa kama nyaraka zote na kila kitu kimekamilika hata kabla ya siku kumi mtu anakuwa amepata mafao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, changamoto ya mafao kwa sasa hatuna kama Mheshimiwa Mbunge anayo anaweza kutupatia. Kwa upande wa Zanzibar suala la mifuko siyo la

kimuungano. Kule wenzetu wametangulia tunawapongeza kwa kazi hiyo. Sisi tupo tayari kwenye hatua nzuri ya kufanya *actuarial evaluation*, ambayo itatusaidia kule taarifa ambayo itaangalia ustahimilivu wa mifuko na kiwango cha upatikanaji wa mafao kama kimepanda. Basi tunakwenda kufanya maboresho hayo na hilo litakuwa ni zoezi la haraka na tayari miaka mitatu ya kufanya *evaluation* hiyo imeshatimia na tuko kwenye zoezi hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana; watumishi wengi nchini wameendelea kulalamikia sana suala la kikokotoo. Hii ni kwa sababu kikokotoo kinasababisha wachukue mafao kidogo yale ya awali.

Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaboresha kanuni ya kikokotoo ili kuwafanya watumishi wengi hasa walimu wapate mafao mengi ya mkupuo ya awali? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi lakini pia kwenye maelezo yangu na ufafanuzi wa awali. Mkupuo wa awali tulikuwa tunalipa asilimia 25 kwa sasa tumefika asilimia 33. Mungu jalia mbele kwa jitihada anazofanya Mheshimiwa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan, tutaenda hata zaidi ya asilimia hizo. Pensheni ya mwezi tulikuwa asilimia 50 sasa tumefika asilimia 57. Utaona hiyo *level of growth* ambayo ni kubwa sana na ni *supersonic speed* ya kuweza kuhakikisha kwamba wafanyakazi wastaafu wanapata mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi katika hilo Mheshimiwa Rais, ameonesha dhamira yake ya dhati sana. Ni kipenzi cha wafanyakazi na Vyama vya Wafanyakazi. Wakati wote tumekuwa tukikutana katika utatu kwa maana ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, kwa ajili ya kuona namna gani tunaweza kufanya maboresho haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuona hata kwenye kipindi cha Korona na mazingira magumu tumeweza kupandisha asilimia…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, malizia hilo. Umeshamjibu vizuri. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Musukuma.

Na. 68

**Kutokamilika miradi ya *CSR Geita DC***

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini miradi ya *CSR* katika Halmashauri ya Geita haikamiliki licha ya kupokea shilingi bilioni 18 kila mwaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imekuwa ikipata miradi ya Uwajibikaji wa Makampuni ya Madini kwa Jamii *(CSR)* yenye thamani ya shilingi bilioni 4.3 kila mwaka kuanzia mwaka 2018. Jumla ya shilingi bilioni 25.8 zimepokelewa hadi kufikia Disemba, 2023. Jumla ya miradi 819 imetekelezwa, kati yake, miradi 661 ni miradi ya elimu, miradi 124 ya afya, miradi tisa ya kilimo, na miradi 25 ya sekta mbalimbali. Aidha, miradi 653 imekamilika sawa na asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa Uwajibikaji wa Makampuni ya Madini kwa Jamii *(CSR)* kutokukamilika kwa wakati kunakosababishwa na kwanza, kupanda kwa gharama za vifaa sokoni, pili, manunuzi ya vifaa kufanywa na makampuni yenyewe na baadhi ya maeneo ya miradi kutopitika hususani nyakati za mvua. Serikali imetunga Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za mwaka 2023. Kufuatia Kanuni hizi, Kamati ya wataalamu imeundwa ambayo itakuwa inapitia miradi na kushauri namna bora ya utekelezaji, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ninataka kumwambia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza Halmashauri ya Wilaya ya Geita, hatuna tatizo na barabara yoyote kusema kwamba kuna sehemu ambako hakupitiki katika kutekeleza miradi iliyopagwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza. Halmashauri ya Geita inapokea bilioni 4.3 kila mwaka. Mwaka 2022/2023 tulitenga hizo pesa na hazikutumika. Tunavyozungumza bajeti yetu imeisha mwezi wa Disemba 2023,

hatujatumia hata asilimia moja. Miradi hii inasimamiwa na Wizara tatu; Wizara ya Fedha, Wizara ya Madini na Wizara ya TAMISEMI. Hakuna hata Waziri mmoja aliyewahi kuja kuikagua miradi hii; je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kufuata na mimi kwenda kunithibitishia hiyo miradi uliyotajiwa imekamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, miradi ya Serikali inatekelezwa, kwa mfano, kwa milioni 500 shule inakamilika au kituo cha afya kinakamilika na majengo saba. Miradi inayotekelezwa na *CSR ni* jengo moja ambalo halikamiliki kwa miaka mitatu hadi leo. Mheshimiwa Waziri upo tayari kufuatana na mimi kwenda kuthibitisha hayo majibu uliyoyatoa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu moja, kwa sababu hoja ni uende naye. Kwa hiyo, jibu ukishakubali basi limekwisha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekubali kwamba tutakwenda na Mheshimiwa Musukuma. Tukafanye ziara na ninamhakikishia Serikali inaendelea kupitia kanuni ili kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa thamani ya fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza; kwa kuwa Fungu la *CSR* linaikumba pia Halmshauri yetu ya Ilala kwenye kupitisha bomba la gesi.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha na sisi kwenye Halmashauri ya Jiji la Ilala kupewa ile mrabaha wa kupitisha lile bomba la gesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umemuelewa hilo swali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba maeneo yote ambayo kuna miradi ya makampuni sheria ifuatwe ili waweze kupata ile huduma ya jamii kwa maana *CSR*. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria zipo kanuni zipo. Tutahakikisha kwamba Halmashauri ya Ilala pia inapata haki yake kutokana na ujenzi wa bomba hili la gesi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba swali namba 69.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abeid Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 69

**Kuzigawa Kata za Jimbo la Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itazigawa Kata za Mtinko, Makuro, Ughandi na Ngimu pamoja na kukifanya Kijiji Kivuli cha Mukulu kuwa kijiji kamili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid

Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa kuzingatia mwongozo wa mwaka 2014 ambapo kusudio hujadiliwa katika vikao vya Ngazi ya Halmashauri, Wilaya na Mkoa kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Hivyo, maombi ya kugawa Kata za Mtinko, Makuro, Ughandi na Ngimu pamoja na kijiji cha Mikulu yatafanyiwa kazi na Serikali itakapoanza kuanziasha maeneo mapya ya utawala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, ninashukuru kwa maelezo mazuri ya Serikali ingawa hayajajibu swali langu la msingi kwamba ni lini maeneo haya ya utawala yatagawanywa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari vikao vya wilaya kwa maana ya *DCC* pamoja na *RCC* vimeshakaa na kuleta mapendekezo Serikali. Kwa hiyo, nilitegemea nipate majibu sahihi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa imebainika kwamba kuna gharama kubwa sana zinatumika katika kuendesha shughuli za Serikali kwenye kusimamia miradi, lakini kutokana na ukubwa wa maeneo haya Serikali ina mpango gani? Haioni haja ya kuongeza fedha kwa ajili ya usimamizi wa miradi kwenye maeneo yetu haya ikiwemo vyombo vya usafiri?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sote Waheshimiwa Wabunge, ni mashuhuda kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana ya kujenga miundombinu ya majengo ya utawala kwa maana ya Ofisi za Halmashauri, Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Vijiji na Kata, kazi hiyo bado inaendelea haijakamilika. Ndio maana Serikali imeweka kipaombele kwanza kukamilisha majengo ambayo tayari yanajengwa ili yatoe huduma vizuri. Baadaye tutakwenda kuanzisha maeneo mengine ya utawala ili tuhakikishe kwamba maeneo yaliyoanzishwa yanatoa huduma ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu uhitaji na ukubwa wa kijiografia ya maeneo haya. Mara Serikali itakapoanza kutoa kipaumbele katika kuanzisha maeneo mapya ya utawala tutawapa kipaumbele Halmashauri hii ya Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na ukubwa wa maeneo na kuongeza gharama ya usimamizi wa miradi ni kweli. Ndio maana Serikali inaendelea kupeleka vifaa vya usimamizi yakiwemo magari, pikipiki na kadhalika. Ninamhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia mapato ya ndani tutaweka kipaumbele kwenye yale maeneo ambayo yana maeneo makubwa zaidi ya kijiografia na Serikali kuu tutaendelea kufanya hivyo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, pamoja na mpango mzuri wa wa Serikali, kuna maeneo yanahitaji uangalizi wa haraka na muhimu sana kwa sababu athari

zinazopatikana kutokana na jiografia kiutawala zinakuwa ni kubwa sana. Eneo kama la Gana Kitongoji kimoja kina watu zaidi ya 6,000 na kina visiwa zaidi ya vitano. Ni kwa nini Serikali isiangalie kwa umuhimu mkubwa kufanya mgawanyo wa maeneo haya sehemu Gana kwenye Kata ya Ilangala ili kuweza kurahisisha mazingira ya kiutawala kwenye maeneo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri:

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la Gana, Ukerewe ni eneo ambalo lina visiwa vingi. Kwa hiyo, lina eneo kubwa la kijiografia na ni ngumu kuli-*manage* kiutawala Serikali inatambua hilo. Yote ni ya kwetu kukamilisha miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo ni muhimu lakini pia, kuanzisha maeneo mapya ya utawala ni muhimu. Kwa hiyo, lazima tuweke kipaumbele ndio maana tumeanza na kipaumbele cha kukamilisha maeneo ya utawala yaliyopo na baadaye tutakwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mkundi, kwamba tunafahamu hilo na Serikali italipa kipaumbele pale wakati utakapofika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 70

**Halmashauri zisizonunua mafuta ya watu wenye Ualbino**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa Halmashauri zisizonunua mafuta ya watu wenye Ualbino?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwezesha upatikanaji wa mafuta kwa watu wenye Ualbino kupitia Halmashauri kote nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 jumla ya Halmashauri 41 zilitenga na kununua mafuta kinga yenye thamani ya shilingi milioni 47 na kuyagawa kwa wahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeelekeza halmashauri ambazo hazikutenga bajeti na kununua mafuta ya watu wenye Ualbino kuzingatia maelekezo ya Serikali yaliyotolewa kupitia Barua Kumb.Na. AB.24/227/01/63 ya tarehe 8 Agosti, 2021, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na ninaipongeza kwa hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa. Kwa mujibu wa jibu la msingi inaonesha

kwamba katika vipindi viwili vya mwaka (2021/2022) na (2022/2023) imetengwa jumla ya milioni 47 kwa Halmashauri 41.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu ya haraka haraka kwa bei ya 15,000 ya mafuta unapata kwamba ni mafuta 76. Sasa Serikali imesema kwamba ilishatoa maelekezo mwaka 2021. Itakumbukwa kwamba Bunge la Bajeti mwaka 2022, Serikali ilitoa maelekezo na ikasema kwamba itatilia mkazo upatikanaji wa mafuta haya.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mafuta haya yanapatikana kwa utoshelevu uliopo ama kwa mujibu wa idadi ya watu wenye ualbino nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilitoa maelekezo kuhakikisha kwamba Halmashauri zote kwanza, zinaainisha na kuwatambua watu wenye ualbino katika maeneo yao; na pili kutenga fedha kwa ajili ya kununua mafuta hayo na kuyagawa kupitia vituo lakini pia katika ofisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo tulipata ni kwamba baadhi ya maeneo walikuwa hawajakamilisha tathmini na utambuzi wa watu wenye ualbino ili waweze kujua mahitaji ya fedha zinazotakiwa kutengwa kwa ajili ya mafuta yao. Kwa hiyo tuliwapa maelekezo hayo na tayari halmashauri 41 zilitenga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mwaka ujao wa fedha tutaweka kipaumbele na msisitizo mkubwa zaidi kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinatenga fedha kwa ajili ya mafuta ya watu wenye ualbino.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kuhamasisha uwekezaji katika viwanda wa kuzalisha mafuta ya ualbino ili kuleta unafuu wa bei?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje katika uwekezaji wa maeneo mbalimbali na tuna mazao ya aina mbalimbali, tuna mazao ya parachichi na mengine ambayo yanaweza yakazalisha mafuta. Kwa hiyo, kwanza tutumie fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshaendelea kuboresha mazingira ya wawekezaji; hivyo tunatoa wito kwa wawekezaji ambao wana uwezo wa kutengeneza mafuta hayo ya kusaidia wenzetu wenye ualbino basi watumie fursa ambazo zipo katika maeneo yetu mbalimbali waweze kuzalisha ili tuwe na uwezo wa kuwa na mafuta hayo kwa wingi ndani ya nchi yetu; na Serikali itaendelea kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri umeshajibu vizuri. Mheshimiwa Bilakwate. Haujasimama eeh?

Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lipo kwenye Wizara ya Kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Samahani swali linahusiana na nini? Tunakwenda swali namba 71 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Felix.

Na. 71

**Mchango wa biashara ya kaboni kwenye Pato la Taifa**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, biashara ya Kaboni katika misitu ya asili na ya kupanda imechangia kiasi gani kwenye pato la Taifa tangu iingie nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe Mkoani Kigoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni kumeibuka soko huria la biashara ya kaboni ikijumuisha misitu ya asili na ya kupanda. Biashara hii ya kaboni imeanza kushamiri hapa nchini na kuonesha inaweza kuchangia kwenye pato la Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2018 – 2022 fedha zilizopokelewa kupitia miradi inayotekelezwa kwenye halmashauri mbalimbali hapa nchini inafikia kiasi cha shilingi bilioni 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 tumepokea jumla ya miradi mbalimbali 35 ya biashara ya kaboni, pindi mchakato wa usajili utakapokamilika na

kuanza kutekelezwa kwa miradi hii, tunategemea kupata wastani wa dola za Marekani bilioni moja, sawa na shilingi trilioni 2.4 ambazo zitachangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri; pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani ya kutoa elimu ihusuyo biashara ya kaboni kwa wananchi wanaozunguka hifadhi za misitu hapa nchini?

(b) Kwa kuwa biashara ni matangazo, je, Serikali inatumia njia gani kutangaza misitu yetu yote nchini ambayo idadi yake ni 589 kwa makampuni ya kigeni yanayojishughulisha na biashara ya kaboni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Ndugu yangu, Mheshimiwa Felix Kavejuru kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu katika ajenda hii si mara moja tu hata katika *side meetings* tunazofanya amekuwa kipaumbele sana kugombania Mkoa wa Kigoma na hasa Halmashauri yake ya Buhigwe katika suala zima la biashara hii ya kaboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati uliokuwepo ni kwamba tumefanya mkutano na Wakuu wote wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha tunapeleka meseji hii ya biashara ya kaboni. Bahati nzuri zoezi hili linakwenda vizuri, na Ofisi ya Makamu wa Rais

kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta na hasa Ofisi ya Maliasili ambayo vile vile kwa pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumekuwa tukishirikiana katika suala zima la kupeleka juu hii elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kupitia vyombo vyetu mbalimbali vya habari tumeweza sasa hivi kuanza kutoa elimu hii kwa watu wajue kwamba kuna fursa hii kubwa ya biashara ya kaboni. Kwa hiyo huu ndiyo mkakati ambao tunaendelea nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunatumia fursa hii kuitangaza; na hasa nishukuru sana katika mkutano tuliofanya mwaka huu kule Dubai *(Cop 28)* miongoni mwa jambo kubwa ambalo tulitangaza kwa wadau mbalimbali wawekezaji katika suala zima la biashara ya kaboni. Naomba niwahakikishie Watanzania, mpaka hivi sasa mwitiko wa wawekezaji ni mkubwa na wengi wamejitokeza. Sasa niwaombe hasa Waheshimiwa Wabunge, kwamba tutumie fursa hii hasa katika maeneo yetu ili tuone kwamba hili ni eneo kubwa sana ambalo tunaweza tukapata pato la kuongeza mapato ya halmashauri zetu na katika Pato la Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Kasaka.

Na. 72

**Ujenzi wa Barabara ya Makongolosi – Rungwa**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Makongolosi – Rungwa?

**NAIBU SPIKA:** Meshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Mkiwa (kilometa 503.36) kwa awamu; ambapo sehemu ya Mbeya – Chunya – Makongolosi (kilometa 111) ujenzi umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya Noranga – Itigi – Mkiwa (kilometa 56.9) sehemu ya Noranga – Itigi (kilometa 25.) umefikia asilimia 72 na kwa sehemu ya Noranga – Doroto (kilometa 6) na Itigi – Mkiwa (kilometa 25.6) kazi ya ujenzi imeanza na utekelezaji wa mradi unaendelea. Kwa sehemu iliyobaki ya barabara ya Makongolosi – Rungwa – Noranga (kilometa 356) Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia akiwa Mkoani Singida akizindua barababra alitoa maelekezo barabara hii ya kuanzia Makongolosi mpaka Mkiwa ianze kujengwa.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza maelekezo hayo barabara hii ianze kujengwa kuanzia makongolosi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara ya kuanzia Makongolosi kupita Mkwajuni, Wilaya ya Songwe mpaka Mbalizi imekuwa inaahidiwa mara nyingi kuanza kujengwa.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha barabara hii na yenyewe ianze kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi, tunatambua kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Singida kwenye ziara alitoa maelekezo kwa Wizara ya Ujenzi kuhakikisha kwamba tunaijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami. Tunachofanya sasa hivi Serikali, barabara hii ilishakamilishwa usanifu. Tunaendelea kutafatuta fedha ili kutimiza hayo maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Hata hivyo tulitenga kiasi cha fedha kwenye bajeti kwa ajili ya kuanza kwa awamu lakini sasa maelekezo ya Mheshimiwa Rais yatazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake sehemu ya Makongolosi kwenda Mkwajuni, barabara hii imeshatengewa fedha kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi kwa kipande cha kutokea Mkwajuni kuja Makongolosi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ni lini barabara ya Moshi - Arusha kipande cha Moshi na pale Kikavu kitapanuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa swali zuri na fupi. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Taratibu za manunuzi zinaendelea. Barabara aliyoitaja inasaidiwa na wenzetu wa *JICA*, kwa hiyo tupo tunaendelea kuifanyia kazi tuanze kujenga hiyo barabara kwa kipande kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na hilo Daraja la Kikavu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mgakorongo - Kigarama mpaka Mlongo ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Jiandae Mheshimiwa Almas.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi, barabara hii ilishatangazwa na ilishapata mkandarasi. Sasa hivi kinachoendelea tu ni taratibu za manunuzi kukamilika ili kipande cha kuanzia Murongo kuja Mkorongo tuanze kukujenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri; je, ni lini barabara ya Mambali – Bukumbi – Shitage – Mulibede mpaka Ushetu itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Maige itajengwa kwa awamu na tayari mameneja wa mikoa ikiwepo Mkoa wa Tabora kama ilivyopangwa kwenye bajeti wapange ama watangaze kwa kiasi kile ambacho kimepangwa kwenye bajeti kuanza kuijenga barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Natambua kwamba Barabara ya Mbuguni imekuwa inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu; na kwamba kazi hiyo ilimalizika mwishoni mwa mwaka jana 2023. Je, ni lini sasa ujenzi wa kuijenga kwa kiwango cha lami utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada kukamilisha usanifu wa kina tunategemea kwamba barabara hiyo sasa itaingizwa kwenye mpango wa bajeti huu ambao tunaendelea ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ndio kwanza tunaanza kuandaa bajeti zetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

Na. 73

**Kukarabati Skimu ya Umwagiliaji Masengwa –Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, ni kuna mpango gani wa kukarabati skimu ya umwagiliaji ya Masengwa-Shinyanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Masengwa iliyopo Kata ya Masengwa Wilaya ya Shinyanga, Mkoani Shinyanga inachangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa zao la mpunga na mbogamboga kupitia kilimo cha umwagiliaji. Skimu hii ina uwezo wa kumwagilia hekta 540. Kutokana na uchakavu wa mfereji mkuu wa skimu hiyo eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni hekta 133. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kupitia wataalamu wake wa ndani waliopo katika ngazi ya Wilaya na Mkoa wanaendelea na kazi ya kubaini mahitaji

halisi ya ukarabati wa skimu hii ili iweze kuwekwa katika mpango wa bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba ni hekta 133 tu ambazo zinamwagiliwa na kuna hekta 407 ambazo zimebaki; je, ni lini hiyo kazi ya kuhakiki itaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Eneo la Mwamnyepe, Kata ya Bubali kuna mto na kuna umwagiliaji ambao wananchi wao wenyewe walianzisha; je, ni lini Serikali itakwenda kukarabati na kuboresha mradi wa umwagiliaji ambao umeanzishwa na Wananchi wa Bubali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tumeweka *commitment* ya Serikali kwenye Mradi wa Umwagiliaji Masengwa ambao uhakiki unaendelea sasa hivi na tutamaliza katika mwaka huu wa fedha; na ndiyo maana *commitment* yetu katika mwaka wa fedha unaokuja 2024/2025 tutaingiza katika bajeti yetu ili utekelezaji uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kata ya mradi ambao umeanzishwa na wananchi jambo hilo na lenyewe tumelipokea ninaiagiza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iende ikafanye uhakiki ili sasa tutafute fedha kwa ajili ya kuweka kwenye bajeti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi, Skimu ya Umwagiliaji ya Msenembo iliyopo katika Halmashauri ya Manyoni ina hali mbaya sana. Mwaka huu

wakulima wameshidwa kulima kabisa. Je, Serikali ina mkakati upi wa kuwanusuru wakulima hawa ili waweze kuendelea na kilimo chao cha umwagiliaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kwenye skimu zote, na ndiyo malengo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ametuelekeza; moja, kuhakikisha tunaekebisha skimu zote ambazo zilikuwa zinatumika awali na sasa hivi zinahitaji marekebisho makubwa.

Pili, kuhakikisha maeneo yote yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tunajenga miradi mipya kwa ajili ya umwagiliaji. Tatu tujenge mabwawa makubwa ya umwagiliaji ili kuhakikisha wananchi wanalima katika kipindi chote cha msimu yaani kwa maana ya mwaka mzima. Kwa hiyo mkakati uliopo kwako upo katika maeneo yote. Niwahakikishe wananchi kwamba Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na uhakiki katika maeneo yote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka juzi na mwaka jana mmeahidi kupeleka fedha kwenye Skimu ya Ruafi, lakini mwaka huu hali ni mbaya na wakulima hawawezi kuendelea kulima. Je, mna mkakati gani sasa kupeleka pesa kwa haraka na mkarabati ile skimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Skimu ya Ruafi na yenyewe ni moja ya skimu ambayo tume yetu imepata taarifa juu ya kinachoendelea

kule na sisi Waziri wa Fedha amekutana na Waziri wa Kilimo kuhakikisha wanatupatia bajeti ili yale maeneo yote ambayo yameharibika sasa tuweze kuyarekebisha. Kwa hiyo hili nikuondoe shaka na tunalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bahati Ndingo.

Na. 74

**Mafao ya wastaaafu wa Shamba la Kapunga – Mbarali**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa mafao wastaafu wa Shamba la Kapunga Wilayani Mbarali lililokuwa linamilikiwa na *NAFCO*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ndingo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ubinafsishaji kati ya mwaka 2003 na 2004, Serikali ililipa mafao ya wastaafu wote wa Shamba la Kapunga isipokuwa mafao ya mkataba wa hali bora ambayo hujumuisha mishahara miwili baada ya notisi, gunia tatu za mpunga kwa kila mwaka waliofanyia kazi au fedha taslimu kwa bei ya wakati huo ilipofungwa mikataba na mwisho walipwe mishahara ya miezi minne kila mmoja kwa kila mwaka waliofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madai hayo ni ya muda mrefu takriban miaka 19 iliyopita na baadhi ya wanaodai taarifa zao hazijahakikiwa. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa

Serikali inaendelea na uhakiki wa madai hayo ili kupata ufumbuzi kulingana na sheria, kanuni na miongozo ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bahati.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza; tathmini tayari ilishafanyika Mheshimiwa Naibu Waziri na mpaka barua Wizara ya Fedha ilienda na wazee hawa wapo 65, na wanachokidai Serikalini ni shilingi milioni 261. Naomba *commitment* ya Serikali juu ya hili kwa sababu ni suala la muda mrefu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge makini kabisa wa Mbarali kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya wananchi wake na kwa kweli hawakukosea kumchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepokea mahitaji haya yanayohusu wazee wetu wa Mbarali sambamba na baadhi ya maeneo mengine kama Mbunge alivyohitaji *commitment* nimuombe tu aridhie nimelichukua tukio hapa hapa Bungeni nitampa *status* ikiwezekana tukiweza kulikamilisha kabla hajarudi, akirudi awape taarifa tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Salim Mussa Omar.

Na. 75

**Kuzuia wasichana chini ya miaka 18 kwenda klabu**

**MHE. SALIM MUSSA OMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia wimbi kubwa la wasichana wenye umri chini ya miaka 18 kwenda klabu za usiku kwenye miziki na starehe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Omar Salim, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kifungu cha 158(1)(b) ambacho kinakataza watoto wenye umri chini ya miaka 18 kushiriki shughuli za mikusanyiko ya usiku zikiwemo klabu na kumbi za starehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu ya malezi na makuzi ya watoto ili kuwapa wazazi na walezi uelewa wa athari za kuwaacha watoto bila ulinzi hasa wakati wa usiku na kuwakumbusha wajibu wao wa kulea na kutunza watoto katika maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, tunaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau wa maendeleo hususan wamiliki wa kumbi za starehe, kwa lengo la kuweka mikakati na mbinu jumuishi za kusimamia ulinzi na usalama wa mtoto, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimefurahi kupata majibu ya Serikali, lakini niseme tu kwamba ulimwengu wa sasa wasichana na hata wavulana walio wengi, tunapokua tunakua katika hali ya ukuza; ni ngumu sana wakati mwingine kutambua umri wa mtu kwa kumwangalia usoni. Naishauri Serikali iweze kuweka *mechanisms* nzuri sana kwa ajili ya kuweza kutambua umri wa ndugu zetu katika kumbi hizi za starehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbi limekuwa kubwa na wasichana ni ngumu sana kumjua kwamba huyu yuko *under 18* kwa kumwangalia usoni. Hatimaye inafikia mahali huko akiombwa namba ndani ya kumbi za starehe tunawa-*attack* watu kwamba wanabaka hali ya kuwa sisi wenyewe Serikali na wazazi tunaachia wanafunzi kwenda katika kumbi za starehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hili lichukuliwe kwa umuhimu wake kwa sababu sote ni wachunga na tutaulizwa uchungaji wetu umechungaje, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, alikuwa anatoa ushauri zaidi ya jambo lolote lingine, hongera na ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

Na. 76

**Msaada kwa wahanga wa mimba za matukio ya ukatili wa kijinsia**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kuwasaidia wahanga wanaopata mimba kutokana na matukio ya ukatili wa kijinsia kama ubakaji na udhalilishaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mipango na mikakati ya kuwasaidia waathirika na manusura wa vitendo vya ukatili kwa kuhakikisha wanapatiwa huduma muhimu zinazolenga kuwasaidia kukabiliana na athari zinazotokana na vitendo hivyo. Aidha, huduma zinazotolewa ni pamoja na huduma za afya, huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii. Huduma za hifadhi, chakula na malazi kupitia Nyumba Salama na Urejeshaji wanafunzi shule kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile ubakaji na udhalilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali imeendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 na mikopo ya wanawake kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)* kwa lengo la kusaidia wanawake kujiinua kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa mimba zinazotokana na ubakaji, ni mimba zisizotarajiwa hasa kwa walengwa; je, Serikali imeweka adhabu gani kwa wanaofanya kitendo hiki? *(Makofi)*

Swali langu la pili; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwabaini watoto wote wanaozaliwa kutokana na mama zao kubakwa ili kuwapa huduma? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAUME NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza Serikali imeweka adhabu kali ikiwemo kifungo kwa ajili ya udhalilishaji, ukatili na ubakaji, kwa lengo la kupunguza vitendo vya ukatili katika jamii na mimba za utotoni. Pia inaendelea kutoa elimu ili kuhakikisha kwamba vitendo hivi vya ukatili vinakwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, Serikali itaendelea kutoa huduma za kijamii kwa wahanga waliofanyiwa vitendo vya ukatili na ubakaji ili kuwabaini watoto hawa, wale waathirika wa vitendo vya ukatili na waliobakwa, tunawaomba wanapokwenda kuripoti katika vituo vya afya, basi kesi zao jinsi zinavyokwenda ndipo tutakapojua jumla ya watoto ambao wamezaliwa kutokana na ubakaji na kuwapa huduma zinazostahiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Malima.

Na. 77

**Vitendea kazi Kituo cha Polisi Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka vitendea kazi kama vile magari na pikipiki katika Kituo cha Polisi Wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Wilaya ya Mpwapwa ina magari mawili yanayohudumia Wilaya hiyo ambayo ni PT 3759 na PT 1975 *Toyota Land Cruiser Pickup* pamoja na pikipiki nne. Kwa kuwa magari na pikipiki hizo bado hazikidhi mahitaji, Serikali itaendelea kutenga fedha za kununua vitendea kazi hivyo kwa ajili ya Jeshi la Polisi na kuvigawa kwenye maeneo yenye changamoto kama Wilaya ya Mpwapwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; utaratibu wa Serikali wa kupeleka Polisi Jamii karibu katika kila Kata umeonesha mafanikio makubwa. Usalama wa wananchi na mali zao umeimarika; je, ni lini Serikali itapeleka Polisi Jamii katika Kata zote za Jimbo la Mpwapwa? Hilo swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili; je, Serikali ina mpango gani kupeleka pikipiki kwa wale wachache ambao wako kwenye Kata chache za Jimbo la Mpwapwa ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa George Malima, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini Polisi Jamii watapelekwa katika Kata zote za Jimbo la Mpwapwa ni kwamba, hayo ndiyo Maelekezo ya Serikali hususan Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambapo kupitia Jeshi la Polisi Mheshimiwa Rais ameridhia kutoa mafunzo kwa askari na ajira, kwa maana ya Wakaguzi Kata ili kuwezesha Kata zote kupata askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia jukwaa hili kumwelekeza *IGP*, ahakikishe kule ambapo hawajapangwa kama Mpwapwa kama ilivyoelezwa, basi kata zote zipate Askari Kata. Kwa sababu ajira zilizotolewa zinatosha kuziwezesha kata zote kupata Askari Kata kwa kiwango cha Mkaguzi wa Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwapatia vitendea kazi, ni kwamba mwaka huu tunashukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na dhamira ya Mheshimiwa Rais mwenyewe, ameridhia kutoa zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ununuzi wa magari 101 pamoja na pikipiki ili kuwezesha Wilaya, Mikoa ambayo haina magari pamoja na Kata kuweza kupata vitendea kazi hivyo. Mara pikipiki hizo zitakapopatikana Wilaya ya Mpwapwa pia itapelekewa, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilayani Hanang halina vitendea kazi kabisa; je, Serikali ina kauli gani ili kuwapatia vitendea kazi hasa vya usafiri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunafahamu na imeelezwa hapa wakati Mheshimiwa Waziri wangu akisoma Bajeti kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilikuwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi na ndiyo maana limekuwa likipata changamoto kuokoa kwenye maeneo yanayohitaji uokozi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeridhia ku-*process* mkopo wa zaidi ya dola milioni 100 kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Zimamoto kupata vitendea kazi na vifaa vingine ikiwemo magari, maana yake usafiri. Ili viweze kuwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha. Mara vitendea kazi hivyo vitakaponunuliwa, Jeshi hilo litapewa ikiwemo Wilaya yako ya Hanang. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar, halafu Mheshimiwa Butondo ujiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, uko tayari kumuondolea udhalili *OCD* wa Nyang'hwale, kwa kupitisha bakuli kwa kuomba fedha kwa ajili ya kutengeneza gari lake ambalo siyo zuri na ni bovu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri kuwepo kwa baadhi ya *OCDs* kwenye Wilaya mbalimbali ambapo wana magari yaliyochakaa ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, magari yatakayonunuliwa kupitia shilingi bilioni 15 tulizopewa, vipaumbele ni Wilaya zisizokuwa na magari au magari yaliyochakaa sana ikiwemo Wilaya yake ya Nyang'hwale. Namhakikishia

Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Nyang'hwale itapewa katika mgao huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya Wilaya ambazo hazina magari kabisa na sasa hivi tunatumia gari moja la kuazimwa na Mgodi wa *Williamson Diamond Limited;* ni lini magari haya mapya yaliyotolewa na Serikali yataletwa katika Wilaya ya Kishapu ili kutatua tatizo kubwa lililopo katika Wilaya hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshajibu kwenye maswali ya nyongeza yanayofanana na hili, labda niongeze maelezo ya ziada kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi shilingi bilioni 15 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, tayari Hazina wameshatupatia shilingi bilioni 10.1 na tumenunua magari 30 kwa ajili ya *OCDs* lakini tumenunua magari kwa ajili ya *RPCs* wa mikoa 12 na mengine ya kuongozea misafara. Mara magari haya yatakapotolewa, nataka niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge, Wilaya zote ambazo hazina magari, zitapata magari. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Matiko.

Na. 78

**Tofauti ya maslahi kati ya Askari wa Jeshi la Polisi na Askari wa Jeshi la Magereza**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, nini kinasababisha tofauti ya maslahi kati ya Askari wa Jeshi la Polisi na Askari wa Jeshi la Magereza?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza yanafanana kwa mujibu wa taratibu za Utumishi wa Umma na kama ilivyofafanuliwa kwenye sheria zilizoanzisha majeshi haya (Sheria Na. 1 ya mwaka 1939, Sura ya 322 na Sheria Na. 34 ya mwaka 1967 Sura ya 58 iliyorejewa mwaka 2002). Maslahi hayo ni pamoja na kupatiwa na kuboreshewa makazi, vitendea kazi, mishahara na posho, sare za kazi, ofisi na vituo vya kutolea huduma, udhibiti wa nidhamu pamoja na utoaji adhabu, utoaji na upandishaji wa vyeo, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ila nasikitika kwa sababu majibu ya Serikali hayana uhalisia. Jinsi alivyoainisha, mathalani *Assistant Inspector of Police* anapewa mshahara *basic salary* ya shilingi 950,000, wakati *Assistant Inspector* of *Prison,* anapewa shilingi 857,000, kuna tofauti ya takribani shilingi 100,000 na wote wako Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na wana cheo kimoja. Ni nini kinapelekea utofauti wa mshahara huu, kinyume

na majibu yako ambayo umeyatoa katika swali langu la msingi? *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelezea kuhusu vitendea kazi na maslahi mengine; Askari wa Jeshi la Polisi wanakuwa na stahiki zao kwa wakati, mathalani, fedha za uhamisho, usafiri, maji na umeme na *night allowances na* Askari Magereza unakuta hawapati, wanatumia fedha zao na wamekuwa wanadai haya madeni kwa takribani zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Askari Magereza hawapewi stahiki zao kwa wakati na pale wanapotumia fedha zao hawalipwi madeni kwa wakati, kinyume na vile ambavyo Jeshi la Polisi na wengine wanapewa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza maelezo kwamba hayana uhalisia, ninaomba kama utaridhia baada ya hapa tuonane nikupe viwango vinavyoonesha kwamba mshahara wa Inspekta wa Polisi na Inspekta wa Jeshi la Magereza, mshahara ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unachoweza kusema ni ngazi za mshahara kwa maana tangu huyu ameanza kazi lini, Mheshimiwa naomba usitikise kichwa…*(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kama ulivyoshauri utakutana naye utamalizana naye huko huko.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya, nitakutana naye ili niweze kumuelewesha jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilijibu swali la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la madai kwa Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kupata kwa viwango tofauti, hii ninakiri *it is across Government* kwamba maeneo mengi wakati mwingine unaweza ukakuta haki za watumishi, hasa stahiki za uhamisho na kwenda likizo, siyo wote wanapata kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuhakikishia kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mara inapopata taarifa za uwepo wa madeni hayo huwa wanalipa wakiwemo watu wa Magereza, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed.

Na. 79

**Kudhibiti ajali za bodaboda nchini**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti ajali za bodaboda zinazogharimu maisha ya wananchi wengi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Shaurimoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati inayotumiwa na Serikali kupitia Jeshi la Polisi ili kudhibiti ajali za bodaboda ni pamoja na kutoa elimu juu ya matumizi bora ya barabara pamoja na uendeshaji vyombo vya moto kwa waendesha bodaboda kwa kushirikisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA),* Mashirika ya Bima, Taasisi na Makampuni binafsi kama *Bet Power,* Ammend, Mabalozi wa Usalama Barabarani *(RSA)*, Kiwanda cha Bia cha Serengeti, shule na vyuo vya udereva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine ni kuchukua hatua za kisheria dhidi ya madereva wa vyombo vya moto wanaovunja sheria ya usalama barabarani pamoja na kushirikiana na TAMISEMI kuunda vikundi vya waendesha bodaboda ili kuhamasisha na kuheshimu sheria za usalama barabarani, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mohamed.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa vile sasa hivi ajali za bodaboda zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku, kwa nini Serikali isiboreshe sasa mfumo wa usafirishaji katika miji yetu ili kupunguza matumizi ya mfumo wa usafirishaji usio rasmi? *(Makofi)*

Swali la pili, ninataka nifahamu Serikali inatumia utaratibu gani sasa kuwapa leseni madereva wa bodaboda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, Ali Mohamed, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya utaratibu na mapendekezo ya kuboresha mfumo wa usafiri ili kuwa na mfumo rasmi, tunachukua pendekezo lako na tutawasiliana na mamlaka ya utoaji wa leseni kwa maana ya *LATRA* wa usafirishaji abiria waweze kulizingatia katika uboreshaji wa mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji wa leseni, matakwa ya sheria yanataka Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *TRA* waweze kutoa leseni kwa mtu ambaye amefuzu mafunzo ya udereva kwenye vyuo na taasisi zinazotambuliwa na Serikali, huo ndiyo mfumo. Kwa hiyo, yeyote aliyepata leseni nje ya utaratibu huo ikibainika leseni hiyo hufutwa na hatua za kisheria huchukuliwa dhidi yake, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri suala la bodaboda ni kero kubwa sana hasa kwenye utumiaji wa Sheria za Barabara. Mimi ni mtetezi mkubwa sana wa bodaboda lakini matumizi yao kwenye barabara yanakatisha tamaa. Lazima muwe na mkakati maalum wa kudhibiti ajali ambazo wanazifanya na lazima muwe na sheria kali za kuwadhibiti na hata kuwasimamisha. Kwa sababu, ukienda Muhimbili pale *MOI* sasa hivi asilimia 90 ni vijana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Shangai. *(Makofi)*

Na. 80

**Kukamilisha Mradi wa Maji wa Mageri – Ngorongoro**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kumalizia Mradi wa Maji wa Mageri utakaohudumia vijiji nane Wilayani Ngorongoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha za utekelezaji wa Mradi wa Maji Mageri utakaohudumia vijiji nane vya Tinaga, Oloirien, Ng'arwa, Yasi, Mdito, Mageri, Mugongo na Magaiduru, ambapo hadi sasa jumla ya shilingi 2,264,520,000 zimetolewa. Fedha hizo zimesaidia kukamilisha utekelezaji wa Banio la Chanzo cha Maji Orkanjor, ulazaji wa bomba kuu kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tenki umbali wa kilometa tatu na ununuzi wa pampu mbili zenye uwezo wa kusukuma maji lita milioni 2.05 kwa Siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na ujenzi wa matenki tisa yenye jumla ya ujazo wa lita 2,000,000 na uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba ya usambazaji umbali wa kilometa 80. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2024. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangai umeridhika? Mheshimiwa Lemburis.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Arumeru Magharibi, baadhi ya miradi mingi ya maji imesimama kwa Wakandarasi kukosa malipo; je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka fedha kwa ajili ya miradi ya maji ikiwemo Mradi wa Olmulo katika Kata ya Oljoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lemburis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa Wakandarasi, tayari tumeanza kuwaondoa Wakandarasi kwenye foleni ya malipo mara baada ya kupatiwa fedha za Desemba na Januari. Kwa hiyo, hata kwa mradi huu kwenye Jimbo lake naye, Mkandarasi huyu atalipwa ili aweze kuendelea na kazi ili amalize kazi hii kwa wakati, wananchi wapate maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itachimba visima kwenye maeneo ambayo hakuna vyanzo vya maji katika Mkoa wa Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Agnes Hokororo, ameshafuatilia mara nyingi na kuelezea namna wanawake wa Mkoa wa Mtwara, baadhi ya maeneo wanavyopata shida, lakini tumeshaanza kuchimba visima. Maeneo mengine ambayo bado yana uhitaji wa kuchimbiwa visima yapo kwenye mkakati. Nimwambie Mheshimiwa Hokororo, tutakutana na kuona kwamba tunapanga ratiba nzuri ya kuweza kufika maeneo haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan. Wewe ni Mheshimiwa nani?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu ni Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Nanyumbu tuliingia Mkataba na Mkandarasi kwa ajili ya usambazaji wa maji kutoka Bwawa la Maratane katika vijiji vinne. Sasa hivi ni mwaka mmoja Mkandarasi hayupo *site* na hajaanza kazi, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala naomba niwe nimelipokea na nitalifuatilia Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha hii kazi inakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Sigula.

Na. 81

**Kuwezesha wavuvi Ziwa Tanganyika**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, Wavuvi wangapi Ziwa Tanganyika wamewezeshwa na shilingi ngapi zimetumika kuwawezesha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza mradi wa kukopesha vyombo vya uvuvi kwa wananchi wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi katika maeneo yote yenye uvuvi nchini ikiwa ni pamoja na Ziwa Tanganyika. Mradi huu unalenga kuwawezesha wavuvi boti za kisasa na vifaa vyake ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi, kipato chao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza ya mradi huo, kwa upande wa Ziwa Tanganyika, makundi yaliyowezeshwa boti za kisasa ni vyama vya ushirika viwili vyenye idadi ya wanachama 169, vikundi viwili vyenye idadi ya wanachama 17 na wavuvi binafsi watano ambapo wamekabidhiwa jumla ya boti tisa zenye thamani ya shilingi 596,762,192.72.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia. Wote ni mashahidi, tumeona juzi amefanya kazi kubwa sana ya kukabidhi boti zaidi ya 160, haijawahi kutokea! Hakika hii ni kubwa na Mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri utaona kabisa Ziwa Tanganyika wamewezeshwa boti tisa, na Ziwa Tanganyika linahudumia mikoa mitatu; Kigoma, Katavi na Rukwa. Uwiano huu ni mdogo sana: Je, nini mkakati wa Serikali wa kuongeza boti katika ukanda wa Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Ziwa Tanganyika tuna uhaba wa vizimba; je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuwapatia

wavuvi wa Ziwa Tanganyika vizimba ili kuboresha Sekta ya Uvuvi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na hili la mpango wa Serikali wa kuongeza vizimba na maboti yote yanakwenda kwa pamoja. Ni kweli kwamba Ziwa Tanganyika ni Ziwa kubwa linalohudumia mikoa mingi na idadi ya boti zilizotoka mpaka sasa ni chache. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshatoa maelekezo kwamba wale wote wanaohitaji boti na vizimba waendelee kuomba na Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo waendelee kuomba Wizarani na Wizara iko tayari kuwahudumia, kuwagawia boti hizo kupitia benki yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale wenye uhitaji, wanahamasishwa kwenda kuonana na Maafisa Uvuvi, wawasaidie kuandika maandiko mazuri yatakayowawezesha kupata hiyo mikopo ili waweze kujiendeleza kwenye Sekta yao ya Uvuvi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Maboto.

Na. 82

**Kumaliza Uvuvi Haramu Ziwa Victoria**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza changamoto ya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imedhamiria kumaliza kabisa changamoto za uvuvi haramu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza mchakato wa kuanzisha chombo maalumu kitakachokuwa na jukumu la kulinda rasilimali za uvuvi katika maeneo yote ya uvuvi ikiwemo Ziwa Victoria. Chombo hicho kitakuwa na jukumu la kudhibiti uvuvi haramu na kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinakuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Kilimo *(TADB)* imeanzisha mpango maalum wa mikopo isiyo na riba ya boti za kisasa za uvuvi na vifaa vyake vikiwemo nyavu halali nchi nzima ili kuwawezesha wavuvi kutumia vifaa vinavyokubalika kisheria, kufanya uvuvi wenye tija na kuachana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huo, Wizara imeanza kutoa boti hizo ambapo boti za kisasa 55 pamoja na vifaa vyake zimetolewa kwa Kanda ya Ziwa Victoria. Aidha, Serikali imekuja na mpango mahsusi wa kuhamasisha ufugaji samaki kwenye vizimba ambapo kwa kuanzia jumla ya vizimba 222 vimetolewa kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa Victoria ili kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye maji asilia *(fishing effort)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Robert.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwenye sekta ya uvuvi. Hata

hivyo nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Kata yangu ya Nyatwali na Bunda kwenye suala la ufugaji wa samaki wa vizimba? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tayari imesharuhusu waombaji waendelee kuomba vizimba na hata maboti. Kwa hiyo, kwa kesi ya Mheshimiwa Maboto, nimshauri awahamasishe Wavuvi wake waonane na Maafisa Uvuvi, wawasaidie kuandika maandiko mazuri yatakayowasaidia kupata mikopo hiyo ili waweze kupata hizo nyenzo za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Maboto, baada ya Bunge hili tuonane nimwelekeze, nimpe mawasiliano ya wanaohusika na habari hii ili waweze kumsaidia kuandika maandiko mazuri yatakayomsaidia kupata mkopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uvuvi haramu katika Wilaya ya Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali inakusudia kuanzisha chombo maalum kitakachosimamia, kwa sababu habari hii ya uvuvi haramu imekuwa ni suala mtambuka, kila maeneo, kila sehemu uvuvi haramu umetamalaki, sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tumekuja na mkakati maalum wa kuanzisha chombo maalum kitakachosimamia wavuvi na shughuli zote za uvuvi ikiwa ni pamoja na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye eneo la Wilaya hiyo, Serikali itakapoanzisha chombo hiki kitakuwa na mamlaka ya kusimamia maeneo yote nchi nzima yanayohusiana na masuala ya uvuvi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kwangu Wilaya ya Rorya tayari zaidi ya vikundi nane vimeshaandika andiko kwa ajili ya kupewa vizimba na boti; je, ni lini vikundi hivi vitapatiwa mahitaji haya?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama vikundi hivyo tayari vimeshaomba na tayari vimeshafanyiwa *assessment,* awamu ya kwanza alifanya Mheshimiwa Rais hivi majuzi, awamu ya pili tunaenda. Kama tayari wameshakidhi vigezo watapatiwa vizimba hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama ambavyo amezungumza Naibu Waziri kuhusiana na suala la kuomba vizimba na maboti, sisi kama Jimbo la Mchinga, tumeshaomba vizimba na tumeshaomba maboti; je, Serikali inatuambiaje juu ya jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo ambayo tayari wavuvi wameshaomba vizimba, sasa tunakwenda kwenye mgao wa awamu ya pili ambao hivi karibuni tutaanza mgao huo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama vikundi vyake tayari vimekidhi vigezo na masharti yaliyowekwa na Benki yetu ya Kilimo, tutaenda kuwapatia vizimba hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Furaha.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo kwa vikundi vya *BMU (Beach Management Unit)* kwa ajili ya kuwa na nguvu ya kuzuia uvuvi haramu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeshaanza kutoa mafunzo kwenye vikundi vya *BMU*. Kama Mheshimiwa Mbunge ana kikundi ambacho pengine kinahitaji mafunzo hayo, tuko tayari kwenda kumfundisha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri kwenye mgao wa boti Dar es Salaam, *Ferry* ukumbuke.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maelekezo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kigua.

Na. 83

**Usambazaji wa dawa kwa kutumia *drones***

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatumia *drones* kusambaza dawa katika Zahanati zetu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimia Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishakamilisha mfumo ambao unahifadhi taarifa zote za vituo kuanzia ngazi ya zahanati hadi Taifa. Mfumo huu utasaidia kupata taarifa za kijiografia *(Geo coordinates)* za vituo vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tupo kwenye hatua ya kuingiza vituo vyote kwenye mfumo huu ili kuufanyia majaribio na pia kutazama gharama za usafirishaji dawa kupitia mfumo huo wa ndege maalum *(drone)* ukilinganisha na usafirishaji kwa njia ya magari ili maamuzi sahihi yafanyike katika kutekeleza wazo hili zuri la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa maelezo mazuri tu kwamba ndege hizi zisizokuwa na rubani ni muhimu kwa ajili ya kutoa huduma za kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ambayo Watanzania tumeipata ya Mvua za *El Nino* ni dhahiri kwamba utaratibu huu ni mzuri na unatija kwa Serikali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, mko tayari kuhakikisha kwamba mfumo huu wa kupeleka dawa vijijini unaharakishwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuko tayari na kweli kwa wakati kama huu njia hiyo ni mkombozi hasa ndani ya Wilaya bila kuzungumzia kwa maana ya kutoka Taifa kwenda

kwenye Wilaya, lakini kutoka ndani kwenye Wilaya kwenda kwenye vituo utaokoa sana. Tutaendelea kuharakisha tuone tutafika mahali gani, lakini nisiahidi kwamba kwa kipindi gani, ila tunaendelea, kwa sababu *coordinate* ni muhimu ili kuongoza lile jambo la *network*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, niliomba nafasi kwenye swali Na. 85.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 84

**Hitaji la meli za abiria Tanga, Unguja, Pemba na Mtwara**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, lini Serikali itanunua meli za abiria zitakazorahisisha usafiri kwa wananchi kati ya Pemba, Tanga, Mtwara na Unguja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli Tanzania *(MSCL)* imetenga kiasi cha fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili kujua aina ya meli zitakazojengwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wananchi wa mikoa ya Tanga, Mtwara, Lindi, Pemba na

Unguja ambapo zitatoa huduma kwa njia ya maji katika mwambao wa Bahari ya Hindi kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi katika ukanda huo. Matokeo ya utafiti huo ndiyo yatakayobainisha aina na ukubwa wa meli itakayojengwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko Mikoa ya Pemba, Tanga, Mtwara na Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mikakati ya Serikali ya kununua meli kwa ajili kutoa huduma katika mwambao wa Bahari ya Hindi, hata hivyo kutokana na fursa za kibiashara zilizopo katika mikoa ya Tanga, Unguja, Mtwara, Lindi na Pemba, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa hiyo kuwekeza kwa kununua meli za biashara ili kuhudumia hilo soko ambapo kutachochea ukuaji wa uchumi katika mikoa hiyo na kuongeza pato la Taifa kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, na pia napongeza kwa majibu haya ya Serikali. Naomba kupata ufafanuzi kwa maswali mawili. Moja, nilitaka kujua kwa sababu uchumi wa watu wa kwenye ukanda huu wa bahari hususan Pemba, Unguja, Tanga, Mtwara na Lindi wanategemea sana upatikanaji wa usafiri wa baharini. Ni lini fedha hizi zitapatikana ili kwenda kufanikisha upatikanaji wa Meli hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili; kwa kuwa Ilani ya CCM inahimiza zaidi kwenye ushirikiano baina ya taasisi ambazo siyo za Muungano, ni maeneo yapi ya ushirikiano ambayo Kampuni hii ya Meli ya Tanzania inashirikiana na Shirika la Meli la Zanzibar? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu ni lini mchakato utakamilika wa upembuzi yakinifu, tumeshaingiza kwenye bajeti katika mwaka huu wa fedha 2023/2024. Tunategemea kabla hatujakamilisha mwaka huu, tutakuwa tumeshakamilisha upembuzi yakinifu kwa kujua lini, kiasi gani, na kwa namna gani pengine inapaswa ifanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ameuliza swali kuhusu ushirikiano kati ya Kampuni ya Meli ya Tanzania *(ATCL)* pamoja na ile ya *SHIPCO* (Shirika la Meli la Zanzibar). Tumeshaanza katika hatua za awali ushirikiano kati ya pande hizi mbili na yapo maeneo makuu matatu ambayo tunaweza kuyatazama katika hatua za kuanzia. Moja, tunaangalia ushirikiano katika taarifa na wataalam; pili, tunaangalia uwezo na kuwajengea uwezo wataalam wetu katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabaharia, TEHAMA, mipango, utafiti, rasilimali watu pamoja na masoko; tatu, tutaongeza zaidi kwenye eneo la kubadilishana uzoefu katika pande zote mbili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Hassan Mtenga.

Na. 85

**Mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na wananchi Mtwara**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi baina ya Jeshi la Wananchi na Wananchi California Mtaa wa Mbae Mashariki, Mkoani Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linalozungumziwa lipo katika Kikosi cha Jeshi cha 665 kilichopo Naliendele Mkoani Mtwara. Eneo hilo linalokizunguka Kikosi hicho lilivamiwa na wananchi na mwaka 2014 wananchi walifungua shauri Mahakamani wakidai kumiliki eneo hilo. Hukumu ya shauri hilo ilitolewa mwaka 2021 ambapo Mahakama ilitupilia mbali madai hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba wananchi kuelewa umuhimu wa maeneo ya jeshi kwa maslahi mapana ya ulinzi na usalama wa Taifa na kutoa ushirikiano. Aidha, naomba wananchi walio ndani ya eneo hilo la jeshi waweze kuondoka kwa kuzingatia taratibu na sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri. Nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo tajwa, lina wanajeshi zaidi ya 10 wapo kwenye maeneo hayo na wamejenga nyumba na wana hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu, ni lini Serikali itakwenda kufuta hati zile, kwa sababu wanajeshi wale wanakuwa wanawapiga wananchi kwenye maeneo mengine na kuwavunjia nyumba ambazo zimejengwa na wanajeshi pale ambazo zina hati kwenye eneo la Jeshi, bado wanaendelea kukaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini Mheshimiwa Waziri tutaongozana kwenda kwenye eneo husika na wewe ukajionee hali halisi ili tuweze kutatua mgogoro huo kidiplomasia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa vile Mheshimiwa Mbunge ameomba tuongozane nikaone hali halisi basi haya yote nitayaona tutakapotembelea eneo hilo na nakubaliana kuongozana naye. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali la nyongeza; je, ni lini Serikali itatatua migogoro iliyopo katika Wilaya ya Nachingwea kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania JKT pamoja na wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoeleza huko nyuma Wizara inayo mpango wa miaka mitatu ambayo inaendelea kuutekeleza na katika mpango huo tayari kulikuwa na maeneo yenye migogoro 87 tumekwishatatua migogoro 78. Kwa hiyo, kwa Eneo la Nachingwea bado tunaendelea kulishughulikia na tutaendelea kulishughulikia ili tuweze kukamilisha, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba migogoro hii yote inatatuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwenye Kata yangu ya Makoko pamoja na Buhare kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya Jeshi la Wananchi pamoja na wale raia wa pale na Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Innocent Bashungwa aliahidi kwenda na mimi kwa ajili ya kwenda kutatua huo mgogoro.

Je, sasa ni lini Mheshimiwa Waziri uliyepo sasa utaandamana na mimi tukamalize huo mgogoro wa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliyenitangulia alikwishatembelea eneo hilo na amekwishanipa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa. Kwa hiyo, tunaendelea hapo alipofikia na kama itahitajika twende tena basi tutafanya hivyo, lakini nafikiri tuna imani kwamba kwa ripoti aliyoitoa tutaweza kukamilisha tatizo hili na mgogoro huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kawawa.

Na. 86

**Kukamilika miundombinu ya Chuo cha *VETA*-Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo ya Chuo cha *VETA* Namtumbo yakiwemo mabweni, bwalo la chakula pamoja na *Lecture Hall*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitenga na kupeleka shilingi milioni 600 katika Chuo cha *VETA* cha Namtumbo ikiwa ni bajeti ya awali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabweni mawili moja la wanafunzi wa kiume na moja la wanafunzi wa kike, bwalo la chakula na jiko pamoja na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo unatekelezwa kwa awamu ambapo kwa awamu ya kwanza ujenzi wa mabweni mawili umefikia hatua ya kuezeka na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu iliyosalia ambayo inajumuisha ujenzi wa nyumba za watumishi, jiko pamoja na bwalo la chakula ambalo litatumika kwa matumizi mbalimbali ikiwamo shughuli za mihadhara, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kwanza kwa ruhusa yako niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kutuletea fedha

nyingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya yetu ya Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali; kwa kuwa mradi huu wa majengo yale ya mabweni ukikamilika katika Chuo chetu cha *VETA* utaweka wanafunzi wengi pale katika Chuo cha *VETA* na watahitaji maji ya kutosha; je, Serikali katika *component* ya bajeti inayokuja inaweza ikaweka mradi wa kuchimba kisima kwa ajili ya matumizi ya chuo kile pale cha *VETA* Namtumbo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikalini kuna magari ambayo yamepata ajali yanaweza kutengenezeka Serikalini na Taasisi za Serikali na yanakaa tu bila kufanyiwa maamuzi yanaharibika; je, Serikali inaweza ikafanya uamuzi wa kupeleka katika Vyuo vya *VETA* yakawa magari hayo ni ya kufundishia wanafunzi wanaofanya ufundi wa utengenezaji magari katika maeneo ya *panel beating*, urekebishaji wa muundo wa ufundi wa umeme wa magari lakini pia na ufundi wa injini na vifaa vinginevyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali hasa hasa Serikali hii ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba huduma zote muhimu zinakuwepo katika vyuo vyetu vile vya zamani, lakini pia hivi vipya ambayo tunavyovijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba tayari Wizara imeshawasiliana na wenzetu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira kule Namtumbo na *UWASA* na kuwaomba watuletee

bajeti ya uchimbaji wa kisima hicho na tayari wameshatuletea bajeti hiyo ambayo inagharimu shilingi milioni mia moja, laki mbili na arobaini na nane laki tano na sabini na sisi pasipokuwa na shaka tutaweza kuingiza sasa katika bajeti inayokuja 2024/2025 ili wakati majengo haya yakikamilika basi na hiki kisima kiweze kuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili amezungumza suala la magari. Mheshimiwa Mbunge naomba nikuhakikishie na Bunge lako Tukufu kwamba Wizara inayo utaratibu huu, ina utaratibu wa kupeleka magari haya yaliyochakaa, lakini vilevile hata magari mapya na kwa vile amezungumzia habari ya magari hapa utaratibu huo upo na magari haya hupatikana kutoka taasisi mbalimbali zikiwemo zile za *TASAF, TANROADS* na taasisi nyingine za Serikali. Kwa hiyo, tutafanya kwa kadri itakavyokuwa imewezekana, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mama Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha zaidi katika Chuo cha *VETA* cha Urambo ili tupate majengo zaidi tuongezee stadi zaidi za ufundi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo chetu kile cha *VETA*, Urambo katika mwaka wa fedha ule uliopita tulipeleka fedha pale kwa ajili ya kuongeza baadhi ya miundombinu lakini vilevile kufanya ukarabati. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Margaret Sitta

kwamba katika mwaka huu tena unakuja wa 2024/2025 tutatenga fedha kama tulivyofanya mwaka uliopita kwa ajili ya kuongeza miundombinu lakini vilevile kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii tunaifanya kwa Vyuo vyote pale Urambo tumefanya, lakini Wanging'ombe pale tumepeleka fedha, Newala kule napo vilevile tumepeleka kwa hiyo tutafanya kama tulivyofanya mwaka uliopita wa fedha, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, ajiandae Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi; je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa bweni la *Songwe Girls Secondary School* ambayo inachukua wanafunzi wa majimbo sita ndani ya Mkoa wa Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya shule na ujenzi wa bweni kidogo naomba nilichukue hili la Mheshimiwa Sichalwe kwa sababu ni ujenzi wa bweni katika shule ya sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Wewe mjibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna utaratibu wa ujenzi wa mabweni katika shule zetu na tunafahamu kwamba tuna mradi wetu mkubwa sana wa *SEQUIP* ambao ni mradi ambao una zaidi thamani ya zaidi ya trilioni 1.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa vile mgao wa awamu inayofuata bado haujafika nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ugawaji huo tutazingatia mahitaji ya bweni hilo pale na mimi bahati nzuri nilifanya ziara nikaenda nikaona nimhakikishie kwamba tutajitahidi kuweza kuweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imewekeza kwenye ujenzi wa Vyuo vya *VETA,* lakini kwa uzoefu nimeona masomo mengi yanayotolewa ni yale masomo ambayo ni ya ushonaji, ujenzi na ufundi seremala; lakini ni upi mkakati wa Serikali kuongeza idadi ya masomo yenye soko la sasa kama ufundi wa magari ya umeme, ufundi wa mabomba *plumbing* na mambo mengine ili iweze kusaidia Watanzania walio wengi na vijana waweze kupata soko kwenye Taifa letu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna *course* zile ambazo ni za *general course* ambazo katika kila chuo kinatoa, lakini mpango wetu wa sasa kama Serikali tumewaagiza wenzetu wa *VETA* kuhakikisha kwamba tunakwenda ku-*customize* zile *course* kulingana na shughuli za eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpango huo tunao na hivi sasa au tuko mbioni kuhakikisha kwamba tunaandaa mitaala ambayo inaendana na shughuli za jamii mahali vyuo vilipo, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni leo hii; wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni watano kutoka Bunge la Zambia wakiongozwa na Katibu wa Bunge la Zambia Bwana Roy Ngulube kwa ajili ya mafunzo, yupo pia Dkt. Mweemba Muungo, Mkurugenzi wa Fedha; Bwana Thokozani Kamanga, Mratibu wa Mikakati na Utafutaji wa Rasilimali; Bwana Sage Samuwika, Msaidizi Mkuu wa Spika wa Bunge; na Bwana Dominic Mwinamo, Kaimu Msaidizi Mkuu wa Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Watumishi kumi kutoka Bunge la Uganda wakiongozwa na *Kaboggoza Herman, Assistant Sergeant-At-Arms; Komugisha Anita - Senior Front Desk Officer; Orishaba Enid - Nursing Officer; Mubunza Eliod - Nursing Officer; Mukanza Damielie Eva - Assistant Officer Supervisor; Naisanga Joan - Office Supervisor; Akera Alex - Office Supervisor; Ongee David Doctor - Engineering Officer; Engwau Ojakol Gabriel - Assistant Door Keeper;* na *Mukubahu Robert - Office Supervisor,* karibuni Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Ummy Ndarienanga, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ndugu Shafii Rajabu ambaye ni *President of the Student's Organization of the Institutes of Accountancy Arusha;* na Edna Melody Yohazi, *Minister of Health and Environmental Conversation of the Student's Organization at the Institute of Accountacy Arusha. (Makofi)*

Wageni 49 wa Mheshimiwa David Kihenzile, wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(SONIT)*. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, rafiki yake mwanafunzi wa Chuo cha Dodoma Ndugu Ramadhani Hassan Mdoe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembeela Bunge kwa ajili ya mafunzo; wageni 43 wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kutoka kwenye vikundi mbalimbali vilivyo chini ya Mradi wa *DREAMS (Determened, Resilient, Emporement, Aids Free, Mentored and Safe)* ambao unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)*. *(Makofi)*

Wanafunzi 150 kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali vya nchini *(Mutual Generation International)*. *(Makofi)*

Yupo pia ndugu Goodluck Urio mfanyabiashara kutoka Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti leo umetoka kivingine. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya bunge ya Kudumu ya bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2023. Sehemu ya kwanza ni utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati ya mwaka 2023 na nafanya hivyo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Taarifa. Maudhui ya taarifa hii yaliwezesha Bunge kuhakiki na kuzifikia Taasisi za Serikali ili kukidhi matarajio ya wananchi kwa sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Kwa madhumuni ya kubainisha mtiririko wa maudhui, naomba kueleza mpangilio wa Taarifa hii ambayo imegawanyika katika sehemu nne, sehemu hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika na orodha ya shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Sehemu ya pili inayoeleza shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji.

(iii) Sehemu ya tatu inayoonesha maoni ya jumla na mapendekezo kwa lengo la kuliwezesha Bunge kuamua; na

(iv) Sehemu ya nne; inayohitimisha ili Bunge liijadili na hatimaye kupitisha mapendekezo kama yalivyo au kwa kuyarekebisha kwa kadiri itakavyofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge, kifungu cha 7(1) nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta, ikiwemo Kamati hii. Majukumu hayo ni: -

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazozisimamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia msingi huo, Kamati imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(a) Kupata mafunzo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kujiandaa kwa pamoja kulingana na wigo wa majukumu ya Kamati;

(b) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023. Lengo ni kufuatilia utekelezaji wa bajeti;

(c) Kutembelea na Kukagua miradi ya maendeleo katika sekta ya ujenzi, sekta cha uchukuzi na sekta ya mawasiliano iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kukidhi masharti ya Kanuni ya 142 Kanuni za Bunge naomba kulijulisha Bunge njia zilizotumika wakati wa utekelezaji wa njia hizo ni kama ifuatavyo; -

(i) Kujadili masuala ya sekta na kuibua ajenda ya kamati;

(ii) Kuhoji na kujadiliana na Mawaziri kuhusu mambo yaliyojitokeza kwa ajili ya taarifa zilizowasilishwa;

(iii) Kutumia matokeo ya ziara ya kamati yaliyoainishwa na mawasiliano kwa ujumla juu ya kamati; na

(iv) Kujumlisha mambo yaliyobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano na kuorodhesha mambo makuu kutolewa maoni juu ya ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge kuwa, njia hizo zimefanikisha matokeo ya kuaminika na kujenga uthabiti wa mapendekezo. Bila shaka Bunge litakapojadili Taarifa hii na kupitisha mapendekezo yaliyomo, Serikali itaboresha shughuli za umma kwenye sekta zinazosimamiwa na Kamati. Matokeo yake yatakuwa ni kufanikisha lengo la Serikali la ustawi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa matokeo. Ufafanuzi; shughuli za Kamati zililenga kubaini iwapo shughuli za umma katika sekta za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano zinaongeza tija katika maisha ya watu na kwamba zinakidhi matarajio ya wananchi kulingana na Ilani ya uchaguzi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

Kwanza ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Taarifa ya mwaka 2023; shughuli hii ilihusisha kutafakari hali halisi ya sekta zinazosimamiwa na Kamati. Tafakari hiyo, ilioanishwa na taarifa za Serikali kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Shughuli za Kamati wa mwaka 2022. Lengo la shughuli hii ni kulisaidia Bunge kufuatilia hali ilivyo na kuwa katika nafasi ya kusimamia Serikali inavyostahili. Matokeo ya shughuli hiyo yaliidhinisha hatua iliyofikiwa dhidi ya matarajio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia; tarehe 21 – 30 Machi, 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti wa Mwaka 2022/2023 kupitia makadirio ya mapato na matumzi ya Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Shughuli hiyo ilifanyika baada ya kutembelea na kukagua miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/2023 na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi katika sekta zinazohusika…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** … Maoni ya Kamati kuhusu mambo hayo yalitolewa wakati wa mkutano wa bajeti mwezi Aprili hadi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kushughulikia Taarifa za Utendaji; mwaka 2023 Kamati ilipokea na kujadili taarifa zilihusu sekta ya uchukuzi, sekta ya ujenzi na sekta ya mawasiliano. Uchambuzi wa taarifa hizo ulidhihirisha picha halisi ya hali ya sekta na uendeshaji wa taasisi za umma kwenye sekta hizo. Kufuatia utekelezaji unaofanywa na Wizara, ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulihusisha mambo yafuatayo: -

(i) Kubaini mambo yanayougusa umma ambayo yanafaa kupata ufafanuzi wa Serikali na kuyaweka kwenye ajenda;

(ii) Kuiomba Serikali iwasilishe Taarifa maalumu ya ufafanuzi kuhusu mambo yaliyobainishwa na Kamati; na

(iii) Kurejesha Ilani ya CCM ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Sera zinazoongoza sekta hizo na miongozo mingine ya utekelezaji wa shughuli za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo Kamati iliweza kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kupendekezwa kwake hatua za kuchukuliwa na Bunge. Bila shaka mapendekezo hayo yatakuwa nyenzo muhimu kwa Bunge kutetea madaraka yake katika sekta ya uchukuzi, ujenzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa hali ya kutokana na shughuli za Kamati. Kama tunavyofahamu, taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati zinawasilishwa ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo yanayohitaji hatua za Kibunge. Hatua hizo zinaweza kuwa ni pongezi, msisitizo au mapendekezo ya kufanyiwa

kazi na kubainisha mambo yaliyoainishwa kutokana na uchambuzi uliofanyika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya *LATRA* yamebainika kuwa muingiliano wa majukumu ya Jeshi la Polisi yanayohusu udhibiti wa Usalama barabarani, hivyo hali hiyo inastahili kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi. Taarifa zilizochambuliwa na Kamati zimeonesha upungufu wa watumishi kwenye Taasisi za *LATRA, TAA, MSCL, TANROADS, TTCL* na *TBA*. Upungufu huo unahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuepuka athari za kwenye ufanisi na tija ya taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu ufanisi wa Mamlaka ya Bandari *(TPA);* ufanisi wa *TPA* pamoja na mambo mengine unategemea matumizi ya mifumo bora wa TEHAMA na fedha zinazopatikana kutokana na tozo za gati. Ufuatiliaji wa Kamati umeonesha kukosekana kwa mifumo ya TEHAMA inayounganisha wadau wa hali isiyoridhisha ya miundombinu ya bandari. Mambo hayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Mfano, iwapo *TPA* itawezeshwa kubakia na shilingi bilioni 35 kila mwezi kutokana na makusanyo ya *wharfage,* uwezo wake wa kuendeleza miundombinu utaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tija na muafaka ya *MSCL; MSCL* imebainika kuwa na upungufu wa fedha kulinganishwa na majukumu yake na gharama za uendeshaji wake kuzidi mapato yanayokusanywa. Aidha, taarifa za Wizara zimeonesha kuwa meli nyingi zinazo milikiwa na *MSCL* zipo kwenye matengenezo kwa muda mrefu. Mambo hayo yasipofanyiwa kazi itakuwa vigumu kupata manufaa na kampuni hiyo katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania; Taarifa zilizofanyiwa kazi na Kamati zinaonesha kuna uchakavu wa miundombinu ya viwanja vya ndege na changamoto ya kukosekana kwa sheria mahsusi ya usimamizi wa

viwanja wa ndege. Ili kuongeza ufanisi wa *TAA* changamoto hizo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri; *TANROADS* imebaini kuwa inakabiliwa na ufinyu wa bajeti wa changamoto ya kutokupokea fedha kwa wakati. Hali hiyo inasababisha kuchelewa kulipa madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri. Kwa mfano, hadi kufikia mwezi Disemba 2023, jumla ya miradi 94 imekamilika na wakandarasi wanadai jumla ya shilingi bilioni 386 kwa miradi hiyo. Wakati huo huo kuna miradi 69 inayoendelea ambayo wakandarasi wanadai jumla ya shilingi bilioni 392 kwa hatua hiyo iliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa mwaka 2024 umeanza *TANROADS* ikiwa inadaiwa na Wakandarasi na Wahandisi Washauri jumla ya shilingi bilioni 778. Deni hilo linazidi kuongezeka kwa utaratibu wa riba katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ndogo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano na changamoto ya uhalifu wa kimtandao. Katika utekelezaji wa shughuli za Kamati imebainika kuwa ujenzi wa minara ya mawasiliano chini ya *UCSAF* unaendelea kwa kasi ndogo hali hiyo inatokana na mchakato mrefu wa kiutaratibu ukiwemo mchakato wa ununuzi na upatikanaji wa fedha. Aidha, taarifa za Serikali zimeonesha kuwepo kwa utapeli wa uhalifu wa kimtandao jambo ambalo ni ishara ya mahitaji ya kuimarika kwa udhibiti na usalama wa kimtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Shirika la Posta Tanzania; Shirika la Posta Tanzania limebainika kukabiliwa na madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 26.8. Madeni hayo yanatokana na kuchelewa kuwasilisha makato mbalimbali yatokanayo na mishahara kama vile *payee* na michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Aidha, sehemu ya madeni hayo inatokana na kutokulipa *VAT* na *SVL* kwa muda mrefu. Vile vile Shirika limebaini kuwa na mtaji

usiotosha, hali inayoathiri utendaji wake wa kibiashara licha ya umuhimu wa huduma zake katika shughuli za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendekezo; baada ya maelezo niliyoyatoa sasa naliomba Bunge lako Tukufu lizingatie ufafanuzi nilioutoa na maoni ya Kamati, lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Hoja hii inaliwezesha Bunge kusimamia shughuli za umma kwenye sekta ya uchukuzi, sekta ya ujenzi na sekta ya mawasiliano. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja katika maeneo matano kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi; Mgongano wa Majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*,

Kwa kuwa, mgongano wa majukumu baina ya Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Aridhini umebainika kuwa miongoni mwa changamoto, na kwamba, matumizi ya mifumo ya TEHEMA isiyosomana katika udhibiti wa shughuli za uchukuzi inasababisha usumbufu na kero kwa wananchi;

Na kwa kuwa, mgongano huo wa majukumu na changamoto hizo za mifumo - zinaathiri ufanisi katika usimamizi wa sekta ya uchukuzi ni kero katika shughuli za umma kwenye sekta ya Uchukuzi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba;

(a) *LATRA,* kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi, *TANROADS* na *TABOA* ifanye mapitio ya kanuni zilizopo;

(b) Serikali isimamie uboreshaji wa Mifumo ya *TEHAMA* inayotumiwa na *LATRA*; na

(c) *LATRA* na Jeshi la Polisi washirikiane kuhakikisha kuwa mifumo ya *TEHAMA* inayotumika kwenye vyombo hivyo

inaoanisha na kuwianishwa kwa lengo la kuondoa tofauti zisizostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi Ikilinganishwa na mahitaji ya ufanisi wa *LATRA;*

Kwa kuwa, *LATRA* yenye dhima ya kusimamia huduma za usafiri ardhini ili kuwezesha huduma zilizo salama na za uhakika, inakabiliwa na upungufu wa watumishi;

Na kwa kuwa, upungufu wa watumishi unakwamisha uwezo wake wa kutoa leseni, kuzifuatilia na kukuza ushindani kwa ajili ya ustawi wa watanzania;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa *LATRA* inaajiri watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko kuhusu ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)*;

Kwa kuwa, yapo malalamiko kuhusu ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania kutokana na:

(i) Kutokamilika kwa mifumo ya TEHAMA inayopaswa kuwaunganisha wadau; na

(ii) Hali isiyoridhisha ya miundombinu inayowezesha uchukuzi wa shehena kutoka bandarini.

Na kwa kuwa, Hali hiyo inayolalamikiwa, inaweza kusababisha mlundikano wa shehena bandarini na kukwama kwa azma ya kuongeza uboreshaji wa huduma zinazotolewa na mamlaka ya bandari;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia Kwamba: -

(a) Mamlaka ya Bandari Tanzania iongeze kasi ya kuboresha miundombinu ya barabara na njia ya reli inayoingia na kutoka bandari ya Dar es Salaam;

(b) Serikali ikamilishe mchakato wa ujenzi wa reli ya Kisasa kutoka Mtwara – *Mbambabay* na ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao Mkoani Mtwara;

(c) Serikali ikamilishe mifumo ya TEHAMA ili kuunganisha wadau wote bandarini; na

(d) Serikali ijenge gati 2 za dharura (kwenye eneo la gati 0) katika Bandari ya Dar es Salaam ambazo zitakuwa na uwezo wa kubeba mzigo mkubwa uliopo bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania Kutobakiziwa Sehemu ya Fedha Inazokusanya Kutokana na Tozo za Gati.

Kwa kuwa, taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kwamba, mapato yanayokusanywa na *TPA* kutokana na tozo za gati yanachukuliwa na Serikali bila *TPA* kubakiziwa kiasi chochote;

Na kwa kuwa, utaratibu huo unaminya uwezo wa *TPA* kufanya maboresho ya miundombinu katika magati hayo, jambo linaloweza kupunguza ufanisi wa huduma za bandari katika magati hayo na kuipunguzia Serikali uwezekano wa kupata mapato zaidi kutokana na huduma za bandari.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwape *TPA* kiasi cha shilingi Bilioni 35 kwa kila mwezi, kutoka kwenye makusanyo ya *wharfage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za uendeshaji wa huduma za meli – *MSCL*.

Kwa kuwa, Kampuni ya Huduma za Meli - *MSCL* inakabiliwa na changamoto kama vile, upungufu wa fedha, ukosekana kwa uhalisia wa gharama za mapato na uendeshaji na Meli nyingi kuwa matengenezo kwa muda mrefu;

Na kwa kuwa, Changamoto hizo zInaathiri huduma muhimu zinazotolewa na Kampuni ya Meli *(MSCL)*.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iongeze fedha kwa *MSCL* ili iimarike na ijiendeshe kibiashara;

(b) Serikali iharakishe matengenezo ya Meli mfano ya MV. Lihemba na MV. Mwongozo;

(c) *MSCL* ijipange kuleta meli itakayoweza kubeba mzigo utakaoletwa na reli ya kisasa *(SGR)* pindi itakapoanza kutoa huduma; na

(d) Serikali iisaidie *MSCL* kupeleka Meli ya Uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)*.

Kwa kuwa, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inakabiliwa na changamoto za upungufu wa Watumishi, Wakandarasi kutokulipwa kwa wakati, uchakavu wa miundombinu, Majengo, Mitambo, Miradi yake kutekelezwa kwa namna isiyokuwa na ufanisi jamii kwa utaratibu wa taasisi kurejesha fadhira kwa jamii yaani *CSR* na kukosekana kwa Sheria inayoweka mfumo wa uendeshaji wa mamlaka.

Na kwa kuwa, hali hiyo inakwamisha ufanisi wa uendeshaji wa mamlaka na kupunguza kasi ya uendelezaji wa Viwanja vya Ndege nchini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba; -

(a) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iwezeshwe kuajiri watumishi na kuongeza idadi ya watumishi;

(b) Serikali iiwezeshe Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kifedha ili iweze kurekebisha miundombinu na kuwalipa Wakandarasi kwa wakati;

(c) Serikali iweke utaratibu wa mikataba ya watoa huduma na Wakandarasi kutekeleza wajibu wa kurudisha fadhila kwa jamii *(CSR);*

(d) Serikali iongeze kasi ya kukamilisha mchakato wa kuwa na Sheria mahsusi inayohusu uendeshaji, usimamizi na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege;

(e) Serikali iibakizie *TAA* angalau asilimia 40 ya makusanyo ya tozo kwa wasafiri *(Passenges Services Charge)* katika Viwanja vya Ndege; na

(f) *TAA* ihakikishe kuwa Viwanja vyote vya Ndege nchini vinakuwa na hati miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za Usimamizi wa Barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

Kwa kuwa, usimamizi na ujenzi wa barabara nchini unakabiliwa na ufinyu wa bajeti ya ujenzi na matengenezo, uvamizi wa maeneo ya barabara nchini na upungufu wa watumishi wa kutosha kuwezesha tija iliyokusudiwa kwa kuanzisha *TANROADS*.

Na kwa kuwa hali hiyo inakwamisha dhamira ya kuanzisha *TANROADS* na kupunguza manufaa ya matengenezo na ukarabati wa Barabara;

Kwa hiyo basi, hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba; -

(a) Serikali iongeze fedha za ujenzi na ukarabati wa barabara ikiwemo madaraja;

(b) Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi na Waandishi Washauri kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosabishwa na riba;

(c) Serikali iisaidie *TANROADS* kuingia mikataba ili mikataba iwe katika mfumo wa kutobadilika *(fixed amount)* ili kuepusha kupanda kwa gharama wakati wa utekelezaji wa miradi;

(d) *TANROADS* idhibiti wizi na uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara;

(e) Serikali iwahi kufanya tathimini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi, pia maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe; na

(f) Serikali itumie ujenzi wa barabara za mchepuo *(bypass),* pamoja na kuweka alama za biconi kwenye mipaka ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ndogo ya uwekezaji katika majengo chini ya Wakala wa Majengo *(TBA)*.

Kwa kuwa, Wakala wa Majengo Tanzania imebainika kuwa na kasi ndogo ya uwekezaji kutokana na upungufu wa mtaji, wapangaji kutokulipa kodi kwa wakati na upungufu wa watumishi;

Na kwa kuwa, hali hiyo inaweza kuathiri uwezo wa Wakala kutekeleza agizo la ujenzi wa nyumba 10,000 jambo linalokwamisha manufaa ya nyumba hizo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali: -

(a) Itenge fedha za kutosha kuiwezesha *TBA* kufanikisha azma ya ujenzi wa majengeo ya makazi na ofisi;

(b) Iweke msukumo unaoisaidia *TBA* kulipwa madeni ya pango zinazodaiwa taasisi za Serikali;

(c) Isimamie *TBA* ipasavyo ili iajiri watumishi wanaohitajika; na

(d) Iwezeshe na kuisimamia *TBA* ili iendelee kutumia ubunifu zaidi wa kujenga majengo na kuingia mikataba yenye tija na Sekta binafsi katika uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao.

Kwa kuwa, suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linapaswa kupatiwa ufumbuzi na *TCRA* kwani linaendelea kuwepo;

Na kwa kuwa, suala hili linalotokana na maendeleo ya TEHAMA linaathiri uchumi, jamii, ustawi na maadili;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali iimarishe udhibiti wa uhuru wa mitandao kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia na uhuru wa kuzingatia mipaka; na

(b) *TCRA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi iweke mikakati madhubuti inayozihusisha kampuni za simu kukabiliana na uhalifu wa kimtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania *(TTCL),* kushindwa kujiendesha kwa biashara.

Kwa kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inayopaswa kujiendesha kibiashara inashindwa kutokana na taratibu za ajira ya watumishi wake kufungwa, taratibu za sekta ya umma isiyoongozwa na misingi ya kibiashara, upungufu wa fedha kwa ajili ya uwekezaji katika biashara ndani ya sekta na uwezo mdogo wa kampuni kuunganisha wateja;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inawezesha kifedha ili iweze kuwa na mtaji wa kujiendesha kibiashara;

(b) Mfumo wa Sheria za ajira Serikalini uangaliwe ili kuruhusu kampuni zinazojiendesha kibiashara kuwa na taratibu za ajira zinazoruhusu kuunda ushindani; na

(c) Kampuni ya Simu Tanzania iongeze uwezo wa kuwa na kasi ya kutosha kuunganisha wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzigo wa madeni na mtaji mdogo wa Shirika la Posta Tanzania.

Kwa kuwa, Shirika la Posta Tanzania limebainika kuwa na mzigo mkubwa wa madeni na mtaji mdogo wa kuweza kujiendesha;

Na kwa kuwa, licha ya Serikali kufanya jitihada kubwa ya kufufua Shirika hilo, bado changamoto hizo zinakwamisha maendeleo ya Shirika kibiashara;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia Kwamba: -

(i) Serikali ibebe deni inalodaiwa na Shirika la Posta Tanzania la Shilingi bilioni 26.8 ili kusafisha mizani ya Shirika na ili kuliwezesha kukopesheka;

(ii) Shirika libuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiendesha kibiashara;

(iii) Serikali iendelee kuisaidia Posta ili iweze kulipwa madeni wanayodai kwenye Taasisi za Serikali; na

(iv) Serikali iongeze mtaji kwa Shirika la Posta na kuhakikisha linapata kamisheni kwa kila mzigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ndogo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano.

Kwa kuwa, ujenzi wa minara ya mawasiliano umebainika kuwa na kasi ndogo kutokana na mchakato mrefu wa kiutaratibu;

Na kwa kuwa hali hiyo inakwamisha lengo la Serikali kufikisha mawasiliano nchini kinyume na matarajio ya wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge inaazimia kwamba, Serikali: -

(i) Kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote iongeze kasi ya kutekeleza ujenzi wa minara ya mawasiliano;

(ii) Iharakishe ujenzi wa chuo cha TEHAMA Dodoma na kutengeneza *ICT hubs* nchini; na

(iii) Ifanye mapitio ya taratibu za mchakato wa zoezi la ujenzi wa minara ili kuboresha taratibu hizo kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho la hoja. Naomba kuhitimisha taarifa hii kwa kutambua utaratibu uliowekwa na Bunge wa kuzitaka Kamati za Kudumu za Bunge kuripoti shughuli zake kwa kipindi cha mwaka. Utaratibu huu unalitaja Bunge kuwa katika nafasi ya kutambua hali ilivyo katika sekta mbalimbali. Ushauri huu wa Bunge kwa Serikali unaweza kufanyiwa kazi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa maelezo haya ya ufafanuzi nilioutoa, utaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili na kutoa ushauri kwa Serikali ili kuboresha shughuli na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Innocent Bashungwa (Mbunge), Waziri wa Ujenzi akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Msongwe Geofrey Kasekenya (Mbunge), na Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Mbunge), Waziri wa Uchukuzi akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Nape Moses Nnauye – Mbunge, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Kundo Andrea Mathew -Mbunge, kwa kuipa Kamati ushirikiano stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuwawezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoa ushirikiano kwenye Kamati.  Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa niaba ya Sekretarieti na

Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kujituma wakilenga kutoa ushauri unaofaa kwa Bunge. Kufanya hivyo kutaiwezesha Serikali kuboresha maeneo mbalimbali na kuendelea kukidhi matarajio ya wananchi kwa Serikali yao, kwa kutambua mchango wao naomba majina yao yote yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili taarifa ya mwaka ya Shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari, 2024 ili hatimaye kupitisha mapendekezo ya Kamati yawe ushauri wa Bunge kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Mwaka 2023. Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Lengo ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na Mapendekezo ya Kamati kwa kuzingatia ufafanuzi unaotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Mjadala wa Taarifa hii utaliwezesha Bunge kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za umma katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Aidha, maudhui ya Taarifa hii

yanaweza kulifaa Bunge katika uhakiki wa hatua zinazofikiwa na Serikali ili kukidhi matarajio ya wananchi kwa sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni ya kubainisha mtiririko wa maudhui, naomba kubainisha mpangilio wa Taarifa hii. Kimuundo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne kama ifuatavyo: -

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa maelezo ya jumla, ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, njia na mbinu zilizotumika na orodha ya shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Sehemu ya pili inayoeleza shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Aidha, sehemu hii inabainisha mafanikio yaliyobainika na changamoto zinazojitokeza;

(iii) Sehemu ya tatu inayoonesha maoni ya jumla na mapendekezo kwa lengo la kuliwezesha Bunge kuamua; na

(iv) Sehemu ya nne inayohitimisha ili Bunge liijadili na hatimaye kupitisha mapendekezo kama yalivyo au kwa kuyarekebisha kwa kadiri itakavyufaa.

## 1.3 Msingi wa Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli zilizotekelezwa na Kamati zilihusu ufuatiliaji wa majukumu yanayotekelezwa na Wizara inazozisimamia. Msingi wa shughuli hizo unaanzia kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 Ibara ya ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaitambua Serikali kuwa chombo chenye mamlaka ya Utendaji na Bunge ni chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za

umma. Aidha, Ibara ya 8 (1) (b) inatambulisha lengo kuu la Serikali la kuwezesha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 96 ya Katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Vilevile, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Katika utekelezaji wa madaraka ya Bunge, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimebainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za kisekta, ikiwemo Kamati hii. Majukumu hayo ni: -

(i) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara inazozisimamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia msingi huo, Kamati imetekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kupata mafunzo kuhusu muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kujiandaa kwa pamoja kulingana na wigo wa majukumu ya Kamati;

(ii) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023. Lengo ni kufuatilia utekelezaji wa bajeti;

(iii) Kutembelea na Kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara inazozisimamia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha

2023/2024. Lengo ni kuoanisha na mwenendo wa jumla wa utekelezaji wa bajeti; na

(iv) Kuchambua Taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2022/2023 na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2023/2024 za Wizara inazozisimamia.

**1.4 Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kulijulisha Bunge njia zilizotumika wakati wa utekelezaji. Njia hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kujadili masuala ya sekta na kuibua ajenda ya kuwekwa kwenye ratiba;

(ii) Kuwapatia wajumbe mafunzo ili kuwawezesha kuwa katika muktadha wa majukumu yao;

(iii) Kutoa fursa kwa Mawaziri kufafanua maudhui ya Taarifa zilizowasilishwa;

(iv) Kuhoji na kujadiliana kuhusu mambo yaliyojitokeza kwenye taarifa zilizowasilishwa na pia kwenye ufafanuzi wa serikali;

(v) Kutumia matokeo ya ziara za Kamati na kuyaoanisha na mawasilisho kwenye Kamati; na

(vi) Kujumuisha mambo yanayobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano na mahojiano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulihakikishia Bunge kuwa, njia hizo zimefanikisha matokeo ya kuaminika na kujenga uthabiti wa mapendekezo. Bila shaka Bunge litakapojadili Taarifa hii na kupitisha mapendekezo yaliyomo, Serikali itaboresha shughuli za umma kwenye sekta zinazosimamiwa na Kamati. Matokeo yake yatakuwa ni kufanikisha lengo la Serikali la ustawi wa watu kama lilivyofafanuliwa kwenye Katiba.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA MATOKEO

## 2.1 Ufafanuzi wa Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyotangulia kusema, Kamati hii inasimamia Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Usimamizi huo unajikita katika kubaini iwapo shughuli za umma chini ya Wizara hizo zinaongeza tija katika maisha ya watu na kwamba, zinakidhi matarajio ya wananchi kulingana na Ilani ya uchaguzi inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi wa shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika Taarifa ya Mwaka 2023

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli hii ilihusisha kutafakari hali halisi ya sekta zinazosimamiwa na Kamati. Tafakari hiyo, ilioanishwa na taarifa za Serikali kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya shughuli za Kamati wa mwaka 2022. Lengo la shughuli hii ni kulisaidia Bunge kufuatilia hali ilivyo na kuwa katika nafasi ya kusimamia Serikali inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji uliofanywa na Kamati uligusa sekta ya uchukuzi, sekta ya ujenzi na sekta Mawasiliano. Taarifa za sekta hizo zilibainisha hali ya utekelezaji ambapo udadisi ulitumika wakati wa majadiliano. Matokeo ya shughuli hiyo yalidhihirisha hatua iliyofikiwa dhidi ya matarajio.

### 2.1.2 Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 21 - 30 Machi, 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti wa mwaka 2022/2023

na kupitia makadirio ya mapato na matumzi ya Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Shughuli hiyo ilfanyika baada ya kutembelea na kukagua miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/2023 na kufanya ulinganisho na makadirio ya matumizi katika sekta zinazohusika. Maoni ya Kamati yalitolewa wakati wa mkutano wa bajeti Mwezi Aprili hadi Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa bajeti za sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zinaendelea kutekelezwa, naliahidi Bunge lako tukufu kuwa Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji huo. Matokeo ya ufuatiliaji yataripotiwa utakapofika wakati kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge. Kwa sasa Kamati inasisitiza kuwa Serikali iendelee kutekeleza bajeti kama ilvyokasimiwa na kupitishwa na Bunge.

**2.1.3 Kushughulikia Taarifa za Utendaji na Kufuatilia Utekelezaji wa Mipango ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia umuhimu wa Taarifa za utendaji, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za sekta inazozisimamia. Taarifa hizo zilihusu shughuli za umma katika sekta ya Uchukuzi, sekta ya ujenzi na sekta ya mawasiliano. Uchambuzi wa taarifa hizo uliiwezesha Kamati kupata picha halisi ya hali ya sekta na uendeshaji wa taasisi za umma kwenye sekta hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ulihusisha mambo yafuatayo: -

(i) Kubaini mambo yanayougusa umma ambayo yanafaa kupata ufafanuzi wa Serikali na kuyaweka kwenye ajenda;

(ii) Kuiomba Serikali iwasilishe Taarifa maalumu ya ufafanuzi kuhusu mambo yaliyobainishwa na Kamati; na

(iii) Kurejea Ilani ya CCM ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Sera zinazoongoza sekta hizo na miongozo mingine ya utekelezaji

wa shughuli za umma. Lengo lilikuwa ni kulionesha Bunge msingi wa mapendekezo ya Kamati kwa kila sekta.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kufanya hivyo, Kamati italisaidia Bunge kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kushauri Serikali ipasavyo. Bila shaka mapendekezo kutokana na shughuli hizo yatakuwa nyenzo muhimu kwa Bunge kutekeleza madaraka yake katika sekta ya uchukuzi, ujenzi na habari na mawasiliano.

**2.2 Uchambuzi wa Hali kutokana na Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kama tunavyofahamu, Taarifa za Utekelezaji wa Shughuli za Kamati zinawasilishwa ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo yanayohitaji hatua za kibunge. Hatua hizo zinaweza kuwa pongezi, msisitizo au mapendekezo ya kufanyiwa kazi. Naomba kubainisha mambo yaliyobainika kutokana na uchambuzi uliofanyika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

**2.3 Yatokanayo na Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**UTEKELEZAJI UNAORIDHISHA SEKTAYA UCHUKUZI**

**2.3.1 Utekelezaji wa Maazimo ya Bunge kuhusu Uhaba wa Watumishi na Vitendea Kazi**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanyika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake, ulibainisha uhaba wa watumishi katika sekta ya Uchukuzi. Taarifa za Serikali kuhusu taasisi za umma katika sekta ya uchukuzi zilionesha kuwa, sekta hii inahitaji watumishi **18,435**. Kwa mujibu wa taarifa hizo, hali halisi ya idadi ya watumishi inaonesha kuwa sekta hii ina jumla ya watumishi **12,151** kwa sasa, baada ya kutekeleza maazimio ya Bunge na kuajiri watumishi 1.975 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Idadi ya watumishi kwa sasa inaonesha upungufu wa watumishi 6,284. Hatua zilizoripotiwa na Serikali ili

kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na kushikiza jumla ya watumishi 1,067 kwenye baadhi ya taasisi kwa muda.

### 2.3.2 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Kuhusu Changamoto ya Kisheria kwa Shirika la Reli

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zilionesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwenye eneo la changamoto ya kisheria kuhusu shirika la Reli. Taarifa hizo zilionesha kuwa, Serikali ilitekeleza maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa changamoto ya kisheria kwa shirika la reli.

**Mheshimiwa Spika**, Hali halisi iliyoripotiwa, inaonesha kuwa, changamoto hiyo ilifanyiwa kazi kwa Muswada wa Sheria uliofanya marekebisho ya Sheria Namba 10 ya mwaka 2017 kwa kuongeza kifungu mahsusi kinachoruhusu sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli. Muswada wa marekebisho ya Sheria ulipitishwa na Bunge tarehe 13 Juni, 2023 na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Julai, 2023. Sheria hiyo ilitangazwa kwenye Gazeti, Toleo Namba 28 la tarehe 14 Julai, 2023.

### 2.3.3 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Utatuzi wa Changamoto ya Vitendeakazi kwa NIT

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu vitendeakazi, Serikali imeripoti jitihada inazochukua kuwezesha vitendea kazi vinavyohitajika. Mfano wa jitihada zilizoripotiwa ni hatua za Serikali kuiwezesha *NIT* kununua ndege mbili (2) kwa ajili ya mafunzo ya urubani na vifaa vya mafunzo ya uhandisi na matengenezo ya ndege. Mfano mwingine *TRC* kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi kama vile vichwa vya treni, mitambo na mabehewa kwa reli zote, yaani MGR na SGR.

**SEKTA YA UJENZI**

**2.3.4 Wapangaji wa Nyumba za TBA Kushindwa kulipa kodi kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika**, TBA kwa kumtumia Dalali wa Mahakama inaendelea na zoezi la ukusanyaji wa madeni. Taarifa zilionesha kuwa, baada ya Maazimio ya Bunge kuhusu ukusanyaji wa madeni ya pango, TBA imekusanya madeni katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Katavi. Jumla ya Shilingi **bilioni 7.628** zilipatikana kati ya Shilingi **bilioni 25.465** zilizokuwa zinadaiwa. Deni hilo limepungua na kufikia Shilingi **bilioni 17.838**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitahada za kuiwezesha TBA kukusanya baadhi ya madeni na inaendelea kusisitiza kuwa, Taaasisi za Serikali zilipe madeni yao kwa wakati.

**2.3.5 TBA Kuchelewa Kulipwa Fedha za Ujenzi wa Miradi kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeripoti kuwa, katika Mwaka wa fedha 2023/24, TBA imetengewa **Shilingi 26,762,580,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi. Hadi kufikia Disemba, 2023, jumla ya **Shilingi 9,550,000,000.00** sawa na asilimia **35.68,** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Aidha, Taarifa zimeonesha kwamba, ulipaji madeni kwa baadhi ya washitiri umekuwa na changamoto. Ufafanuzi umebainisha hatua zilizochukuliwa ni kulipa kiasi cha Shilingi **13,052,510,000.47** baada ya kuhakikiwa na kukidhi vigezo vya kulipwa.

**2.3.6 Kanuni Zinazoendesha TBA Kutoruhusu Uwekezaji Mkubwa**

**Mheshimiwa Spika**, Suala la Kanuni zinazoendesha TBA kutoruhusu uwekezaji mkubwa, lililolokuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge mwezi Februari, 2023, limetekelezwa na Serikali. Maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati yanaonesha kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na TBA, imefanya mapitio na kuhuisha Hati ya Uanzishwaji wa Wakala *(Establishment Order)* ya TBA. Kwa sasa, Hati

ya Uanzishwaji wa TBA iliyohuishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 595 la tarehe 25 Agosti, 2023. Tangazo hilo, limeruhusu Wakala kushirikiana na Sekta binafsi katika ujenzi wa majengo na uendelezaji wa milki.

**2.3.7 Kuchelewa Kulipwa Fidia katika Ujenzi wa Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda - Lusitu-Mawengi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetekeleza maazimio ya Bunge kuhusu fidia katika ujenzi wa barabara ya Itoni – Ludewa - Manda – Lusitu - Mawengi. Serikali ilieleza kuwa, Wananchi wote wa Kijiji cha Mawengi ambao ardhi yao imetwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara wamelipwa fidia. Aidha, wananchi ambao hawajalipwa ni wale waliopo ndani ya eneo la nyongeza la mita 7.5 (kati ya mita 22.5 na 30) ambapo Serikali haijalipa fidia kwa nchi nzima.

**2.3.8 Miradi kutokamilika kwa wakati na kuongezeka kwa gharama za miradi**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za utekelezaji zinabainisha kuwa, TANROADS inaendelea kusimamia miradi mbalimbali ya barabara na madaraja ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati ili kuondokana na changamoto ya kuongezeka kwa gharama za miradi kunakosababishwa na kuongezeka kwa bei za vifaa na kuchelewesha malipo ya Wakandarasi wakati wa utekelezaji wa miradi.

**SEKTA YA MAWASILIANO**

**2.3.9 Kuchelewa kukamilika kwa mikataba na taratibu za manunuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kusimamia ukamilishwaji wa mikataba na taratibu za manunuzi ya vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo kwa sasa vifaa vyote vya mradi vimewasili nchini na utekelezaji uko katika hatua mbalimbali.

### 2.3.10 Miradi kutekelezwa chini ya Kiwango Ikiwemo Ujenzi wa Minara

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeripoti kuwa, inaendelea kuwasimamia watoa huduma wote kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakuwa ya viwango vinavyokubalika. Suala hili linahitaji kupewa mkazo zaidi ili kuzuia madhara yake kwenye miradi inayohusika.

### 2.3.11 Kutenga Fedha Zaidi kwa Ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Kuisimamia Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL) Kukamilisha Ujenzi wa Minara

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji unaendelea, katika Mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imetenga jumla ya Dola za Kimarekani **milioni 30** kupitia fedha za mradi wa Tanzania ya Kidigitali ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ili kutekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/23, TTCL imekamilisha ujenzi na kuwasha jumla ya minara 72 kati ya minara 117 ambayo ni sawa na asilimia **62.**

### 2.3.12 TCRA Kuendelea Kushirikiana na Jeshi la Polisi Kukabiliana na Tatizo la Uhalifu wa Kimtandao

**Mheshimiwa Spika**, TCRA inaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuwezesha udhibiti wa uhalifu mtandaoni, kwa kuwezesha mafunzo kwa Jeshi la Polisi yanayohusu uchambuzi wa taarifa za mitandao na kusimamia matumizi ya namba maalumu 15040 kwa ajili ya watumiaji wa huduma za mawasiliano, kutoa taarifa ya matukio ya utapeli kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) kwa mitandao yote ya simu nchini. Mpaka kufikia Disemba, 2023 jumla ya namba za simu 8,117 zilibainika na kufungiwa. Aidha TCRA imebadilisha kanuni na kuongeza kipengele kwa watoa huduma kuwajibika kwenye kesi za uhalifu wa Mitandao.

### 2.3.13 Serikali Kuiwezesha Kampuni ya (TTCL) Kulipwa Madeni na Kukamilisha Kanuni za Uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha uhamishwaji wa Mkongo kwenda TTCL. Kwa sasa Mkongo unasimamiwa na kanuni zilizowekwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Serikali imeisimamia TTCL kupewa fedha kiasi cha Sh. **58,039,000,744.71** kwa ajili ya uendelezaji wa Mkongo.

### 2.3.14 Upungufu wa Mapato ya Serikali Unaotokana na Shirika la Posta

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wake ni kwamba, Shirika kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari limefanikiwa kukusanya **Shilingi 2,555,944,486** kati ya **Shilingi 4,498,934,931** kutoka katika taasisi za Serikali zinazodaiwa ndani ya kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi June 2023. Hata hivyo, Shirika la Posta Tanzania bado linadai Shilingi **1,942,990,446** kutoka katika taasisi za Serikali. Ufuatiliaji wa deni hili unaendelea. Aidha, Shirika la Posta limeingia mashirikiano na watoa huduma binafsi katika usafirishaji wa bidhaa za Posta na lipo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano.

### 2.3.15 TBC Kuajiri Wasanii wenye Vipaji

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zinaonesha kuwa Ofisi ya Rais (UTUMISHI) imetoa kibali maalum cha ajira kwa watumishi 11 wenye sifa na vipaji vya kipekee kuendana na mahitaji ya soko la utangazaji waliokuwa katika ajira za mkataba.

### UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO USIORIDHISHA
### 2.3.16 Utekelezaji katika Sekta ya Ujenzi

**Mheshimiwa Spika**, Kwenye sekta ya ujenzi, kuna upungufu wa fedha za miradi ya maendeleo hasa katika ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja. Barabara nyingi nchini ni mbovu na

nyingine zimeisha muda wa matumizi na zinahitaji kujengwa upya. Mfano ni barabara ya Dodoma – Iringa, Dodoma - Mwanza, Dar es Salaam – Mtwara na nyinginezo.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Shilingi Trilioni **1.4** iliyopitishwa na Bunge haitoshelezi kukabiliana na matatizo yaliyopo katika miradi ya ujenzi wa barabara kwa nchi nzima. Aidha, upungufu mkubwa wa fedha za matengenezo na ukarabati wa barabara na madaraja unaendelea kuiathiri sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa tathimini iliyofanyika kabla ya mvua zinazoendelea kuanza kunyesha ilionyesha kuwa, kiasi cha fedha zilizokuwa zinahitajika katika ujenzi wa barabara na matengenezo kwa nchi nzima ni Shilingi Trilioni tano (**5**) (ujenzi wa barabara na madaraja ni Trilioni tatu (**3**) na matengenezo ni Shilingi Trilioni mbili **(2)**).

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mvua za masika zinazoendelea ni dhahiri kuwa fedha hizo bado hazitoshelezi.

**UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI**

**2.3.17 Maazimio kuhusu Changamoto ya Kuchelewa kwa Kuanza kwa Utekelezaji wa Mradi wa Reli ya kisasa**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ilibainika kuwa, Sekta ya uchukuzi inakabiliwa na changamoto ya kuchelewa kwa kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro tofauti na malengo. Kamati inasisitiza kuwa Serikali iondoe hayo mapungufu yaliyopo ili mradi uweze kuanza kwa manufaa ya nchi na wananchi.

**UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO**

**2.3.18 Utekelezaji wa Maazimio kuhusu mradi wa Tanzania ya Kidigitali utekelezaji wake unategemea fedha za nje**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mradi wa Tanzania ya Kidigitali, unategemea fedha za nje kwa asilimia mia moja. Kutokana na umuhimu wa mradi huo kwa maendeleo ya taifa, Serikali inapaswa kutenga kiasi cha fedha katika mapato yake ya ndani yatakayowezesha kutekeleza mradi huo. Aidha, suala la ujenzi wa minara linahitaji kuongezewa msukomo ili kasi iongezeke na fedha zipatikane kwa wakati.

**2.4 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao cha Kamati cha tarehe 16 – 26 Januari, 2024 ilipata taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa miradi ya maendeleo kama ifuatavyo: -

**2.4.1 Wizara ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024 ni Shilingi **1,417,143,057,000**. Kati ya hizo, Shilingi **1,081,966,369,000** ni fedha za ndani na Shilingi **335,176,688,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha kuwa, fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2023 ni Shilingi **901,702,353,608.75** sawa na asilimia **64** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/24. Hali hiyo inaweza kuwa kuwa dalili nzuri ya utekelezaji kwa kuwa kipindi cha utekelezaji kilichobaki kinaweza kutumika kukamilisha upatikanaji wa fedha iliyosalia.

**2.4.2 Wizara ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara hii, iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **trilioni 2.08** kwa ajili ya bajeti. Kati ya fedha hizo, Shilingi **trilioni 1.97** ni fedha za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi trilioni **1.86** ni fedha za ndani, sawa na asilimia **94.42** na Shilingi bilioni **107.26** ni fedha za nje, sawa na asilimia **5.58**.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimetolewa ni Shilingi **trilioni 1.44,** sawa na asilimia **73.09** ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, Shilingi trilioni **1.37** ni fedha za ndani sawa na asilimia **95.14** ya fedha zilizotolewa na Shilingi bilioni **63.59** ni fedha za nje sawa na asilimia **4.86** ya fedha zilizotolewa.

**2.4.3 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/24 iliidhinishiwa kutumia Shilingi **212,457,625,000.** Kati ya fedha hizo Shilingi **181,953,940,333** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **146,777,440,000** ni fedha za ndani na Shilingi **35,176,500,000** ni fedha za nje. **Shilingi 102,311,156,120.50** sawa na asilimia **56** ya lengo kimepokelewa. Kati ya fedha hizo Shilingi **67,912,303,911.60** ni fedha za ndani na Shilingi **34,398,852,208.90** ni fedha za nje.

**2.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ya Taarifa inaonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza na kubainisha mafanikio na changamoto. Lengo ni kuhakiki shughuli za umma zilizotekelezwa katika sekta ya Ujenzi, Uchukuzi Habari na Mawasiliano kwa kuzingatia matarajio ya wananchi kama ifuatavyo: -

**2.5.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika**, sekta hii ikiboreshwa itapunguza gharama za usafirishaji wa watu, mizigo na bidhaa na hatimaye kuboresha kiwango na ubora wa maisha ya watu. Kwa msingi huo, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:

**(a) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini – LATRA Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 09 Septemba, 2023 Kamati ilifanya ziara katika Taasisi ya LATRA na kubaini mafanikio yafuatayo:-

(i) Mapato ya Mamlaka yameongezeka kutoka **bilioni 25.95** mpaka **bilioni 34.17** sawa na **asilimia 32** kwa mwaka 2020 – 2023;

(ii) Kuunganishwa kwa Mfumo wa Vehicle Tracking System (VTS), Hadi mwishoni wa mwezi Juni, 2023 jumla ya mabasi 8,734 na vichwa vya treni 18 vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huu;

(iii) Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)* imeendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni kwa kujenga mfumo mpya ujulikanao kama "*Railways and Roads Information Management System (RRIMS)";*

(iv) Kuboresha mfumo huu (RRIMS) ambao pia umeunganishwa na mifumo ya wadau mbalimbali wa Serikali ikiwemo TRA, TIRA, BRELA na NIDA; na

(v) Kufanya uchunguzi wa matukio ya ajali kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Mheshimiwa Spika**, LATRA inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Mgongano wa kisheria baina ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168. Eneo la mgongano lipo kwenye utekelezaji wa jukumu la ukaguzi wa ubora wa vyombo vya moto vinavyoendeshwa kibiashara na kudhibitiwa na LATRA;

(ii) Kutokuwa na muunganiko wa mifumo na wadau wengine kama jeshi la Polisi na TCRA; na

(iii) Upungufu wa watumishi.

**(b) Uboreshaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA**

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya tarehe 11- 19 Novemba, 2023 ukaguzi wa bandari ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara ulifanyika, mafanikio yafuatayo yalibainika: -

(i) Kuanza kupokea meli kubwa zaidi kutokana na kukamilika kwa miradi ya maboresho katika bandari za DSM, Tanga na Mtwara;

(ii) Shehena iliyohudumiwa na bandari za TPA iliongezeka kwa asilimia **17.5** kutoka tani 5.81 milioni hadi tani 6.83 milioni;

(iii) Mapato yaliyokusanywa kupitia Bandari za TPA yaliongezeka kwa asilimia **17** kutoka Shilingi **bilioni 310.78** hadi Shilingi **bilioni 365.12** yaliyokusanywa kipindi hiki cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24;

(iv) Kasi ya utekelezaji wa miradi imeongezeka ambapo baadhi ya miradi mikubwa kama vile *DMGP* awamu ya kwanza na maboresho ya bandari ya Tanga awamu zote mbili zimekamilika na sasa ziko katika hatua za matazamio;

(v) Bandari ya Mtwara imeendelea kupokea na kuhudumia meli kwa kipindi chote cha mwaka baada ya kuanza kupokea meli za moja kwa moja na shehena ya makaa ya mawe; na

(vi) Soko la DRC limeendelea kuimarika kuongoza katika shehena ya nje ya nchi *(transit)* inayohudumiwa kwa asilimia **42.** Serikali kupitia TPA imefungua Ofisi mpya ya kimasoko katika mji wa Kalowezi baada ya ile ya Lubumbashi.

**Mheshimiwa Spika**, Huduma za bandari nchini zinakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Kasi ndogo ya ushushaji wa shehena katika bandari ya DSM yanayosababisha msongamano mkubwa wa shehena bandarini ikiwemo meli za mafuta katika boya la SPM ambazo hutumia wastani wa zaidi ya siku 10;

(ii) Mifumo ya TEHAMA isiyotosheleza.

(iii) Upungufu wa fedha za uendeshaji, watumishi na vitendea kazi;

(iv) Kutokuwepo kwa meli ya abiria katika bahari ya hindi itakayotoa huduma DSM – Zanzibar – Mtwara – Comoro;

(v) Mamlaka kushindwa kulipa vyeti vya malipo kwa Mkandarasi/Mshauri (vilivyoiva) kwa ajili ya mpango wa kuendeleza miundombinu ya bandari; na

(vi) TPA inakosa udhibiti wa mapato yanayotokana na tozo za huduma ya matumizi ya Gati zake *(Wharfage)* ambayo yangewezesha maboresho ya miundombinu.

**(c) Kampuni ya Huduma za Meli - MSCL**

**Mheshimiwa Spika,** MSCL inaendelea na mkakati wa kukarabati meli 13 na kujenga meli mpya tisa (9) ifikapo mwaka 2025. Mpango huo utawezesha lengo la kukamata masoko ya kusafirisha abiria na mizigo katika nchi za DRC, Uganda, visiwa vya Comoro na Shelisheli kupitia ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto kama zifuatazo: -

(i) Upungufu wa fedha;

(ii) Mapato yanayozalishwa kutolingana na gharama za uendeshaji wa Taasisi;

(iii) Meli nyingi zipo kwenye matengenezo kwa muda mrefu na kutokuwa na meli ya uvuvi katika Bahari ya Hindi; na

(iv) Upungufu wa Watumishi.

**(d) Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, TAA imepiga hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) TAA imetunukiwa tuzo ya Kimataifa yenye hadhi ya Nyota Nne (4) iliyotolewa na *Skytrax* kwa Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere katika kutekeleza itifaki ya udhibiti wa usambaaji wa UVIKO19 kwa nchi za Afrika;

(ii) Imewezesha nchi kushika nafasi ya nne (4) Afrika katika ubora wa usalama wa usafiri wa anga kwa kupata alama 86.7;

(iii) Kuweza kuboresha miundombinu katika viwanja vya ndege na kutoa huduma bora kwa abiria na mashirika ya ndege;

(iv) Imetengeneza fursa mbalimbali za ajira kwa wazawa '*Local Content*' kupitia makampuni mbalimbali yanayopata kandarasi za kutoa huduma;

(v) Kuimarika kwa huduma za uendeshaji, ulinzi, usalama na uzingatiaji wa masuala ya afya katika Viwanja vya Ndege nchini; na

(vi) Mashirika mawili mapya ya ndege ya kimataifa yameanzisha safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ambayo ni Saudia Airlines na Air France.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto zifuatazo katika Shirika: -

(i) Ufinyu wa bajeti;

(ii) Uchakavu na ufinyu wa miundombinu, majengo, mitambo na mifumo katika Viwanja vya Ndege;

(iii) Wakandarasi kuchelewa kulipwa kwa wakati na kusababisha kupanda kwa gharama zitokanazo na riba;

(iv) Baadhi ya jamii kutonufaika na miradi inayoendelea kutokana na kukosekana kwa utekelezaji wa dhana ya wajibu wa kampuni kurejesha fadhila kwa jamii (CSR). Mfano, ujenzi wa Zahanati, shule, visima n.k;

(v) Kutokuwepo kwa Sheria mama na mahsusi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege Tanzania Bara;

(vi) Kutokuwepo kwa ruti za ndege za ATCL kwa baadhi ya mikoa mfano, mkoani Mtwara na kukosekana kwa fensi katika uwanja wa Ndege wa Mtwara;

(vii) Baadhi ya Viwanja vya Ndege nchini havina hati miliki; na

(viii) TAA kutokuachiwa na Serikali mapato ya uendeshaji katika Viwanja vya Ndege (passenger services charge).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa maboresho makubwa katika masuala ya uendeshaji, usimamizi na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege.

**2.5.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ujenzi**

**(a) Wakala wa Barabara Tanzania - TANROADS na Mfuko wa Barabara - RFB**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana ni kama yafuatayo: -

(i) Uzinduzi wa barabara ya Mianzini - Ngaramtoni – Arusha (km 18), barabara ya Mtwara – Mnivata – Newala, Tandahimba – Masasi (km 210);

(ii) Kumiliki Mfumo wa Usimamizi wa Rasirimali za barabara (RAMS);

(iii) Kupungua kwa magari yanayozidisha uzito barabarani hii ni baada ya kutoa elimu kwa wasafirishaji juu ya madhara ya kuzidisha uzito wa mizigo;

(iv) Kufunga CCTV kamera kwenye vituo vyetu vya mizani nchi nzima kwa ajili ya kudhibiti mianya ya rushwa;

(v) Kupungua kwa foleni kwenye baadhi ya maeneo ya mizani kutokakana na matumizi ya mizani ya upimaji wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM); na

(vi) Serikali kupitia TANROADS ilisaini mikataba saba ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa KM 2035 kwa kiwango cha lami kwa njia ya *EPC+F* kwa gharama ya Sh Trilioni **3.775** bila VAT.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo na fedha za matengenezo. Mpaka Disemba 2023 fedha za ukarabati/matengenezo zilizopokea ni Sh. Bilioni **369.** Kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha fedha hizo hazitoshelezi**;**

(ii) Ucheleweshaji wa kulipa madeni ya Wakandarasi na Waandisi Washauri kwa wakati kwenye miradi, na kusababisha kuongezeka kwa gharama. Hadi Disemba 2023, Miradi iliyokamilika ni **94** na Wakandarasi wanadai Shilingi Bilioni. **386.36**. Pia Miradi ya barabara inayoendelea ni **69** deni la Wakandarasi ni Shilingi Bilioni. **392.608** hivyo jumla ya deni lote la Wakandarasi mpaka kipindi hicho ni Shilingi Bilioni **778** na linaweza kuongezeka kwa utaratibu wa riba katika miradi;

(iii) Uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara hususan uzidishaji wa mizigo, uharibifu wa samani za barabara/wizi wa alama za barabarani utupaji wa taka kwenye mifereji ya maji ya mvua na kadhalika;

(iv) Kuchelewa kwa tathmini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi inayosababishwa na Sheria ya fidia. Hadi Disemba 2023, fidia inayohitajika kwenye maeneo yote nchini kwa barabara za kuu na za mikoa inakadiriwa kufikia Shilingi Trilioni **5,588,658,067,710.69;**

(v) Uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya barabara hasa kwa wafanya biashara, mamlaka zinazohusika na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya huduma kama vile maji, umeme, mkongo wa simu n.k; na (v) Upungufu wa Watumishi.

(b) Wakala wa Majengo Tanzania - TBA

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatayo: -

(i) Wakala ulifanikiwa kukamilisha ujenzi wa jengo la kibiashara eneo la Sekei (Simioni) jijini Arusha;

(ii) Ajira mpya za watumishi wa wakala uliajiri watumishi wapya 18 na kufanya jumla ya watumishi wa wakala kuwa 454;

(iii) Imekamilisha miradi sita (6) ya Washitiri na kuikabidhi, ambapo, miradi mitano (5) ni ya Ushauri na mmoja (1) wa Ujenzi; na

(iv) Kuhuishwa kwa sheria iliyoanzisha Wakala kupitia GN 595 ya Agosti 25, 2023 ambayo inayoruhusu TBA kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza miliki nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini changamoto kama vile upungufu wa fedha ya mtaji, wateja kutolipa kodi kwa wakati, upungufu wa watumishi na kutofanya uwekezaji wa kutosha.

### 2.5.3 Sekta ya Mawasiliano

### (a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikiwa katika mambo yafuatayo: -

(i) Kutumia mfumo wa teknolojia unaowezesha kutambua mapato na takwimu za miamala mitandao ya fedha kama vile Vodacom (MPesa), Tigo (Tigo Pesa), TTCL (T-Pesa), Viettel (Hallo Pesa), Airtel (Airtel Money), na Zantel (Ezy Pesa);

(ii) Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Mawasiliano na kuwezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za kifedha kwa kutumia mfumo wa *Telecommunication Traffic Management System* (TTMS);

(iii) Kuboresha Usimamizi wa Mfumo wa Uhakikisho wa Mapato ya Mawasiliano ya Simu na usimamizi wa kanzidata kuu ya usajili wa laini za simu; na

(iv) Kudhibiti simu za ulaghai kutoka nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Wamiliki wa mitandao ya kijamii duniani kutokuwa na leseni ya TCRA, matumizi ya Intaneti kutokuwa na mipaka, usalama, usiri wa mawasiliano mtandaoni;

(ii) Utapeli/wizi kwa kutumia majina ya watu maarufu kwa maslahi binafsi, jumbe fupi (SMS) na sauti kwa kulaghai wananchi watume pesa kwenye namba fulani; na

(iii) Kutokuwa na vituo vya kuendeleza vijana katika masuala ya TEHAMA (ICT *hubs*) nchini.

**(b) Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuhamishiwa kwa shughuli za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Taifa cha kutunza Data kutoka Wizara ya Habari¸ Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WHMTH) kuja Shirikani. Aidha, umiliki wake bado unasubiri waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM);

(ii) Shirika limefanikiwa kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati mpya wa mwaka 2022/23 hadi 2026/27 wenye mwelekeo wa uchumi wa kidijitali na kuongeza mauzo ya data na intaneti ndani na nje ya nchi;

(iii) Shirika limefanikiwa kufikisha mawasiliano ya intaneti ya kasi (faiba) katika vijiji vipya vya Msomera na Kwala juu na kilele cha Mlima Kilimanjaro inayotarajiwa kuhudumia watalii wote wanaopanda mlima kwa mwaka;

(iv) Shirika limefanikiwa kuboresha mfumo wa utendaji na wa fedha kwa kuanza kutumia Enterprise Resources Management System (ERMS); na

(v) Shirika limefanikiwa kupanua wigo wa intaneti kupitia mkongo wa baharini wa EASSY na SEACOM kwa asilimia **286** kutoka 17.5 Gbps hadi 67.5 Gbps Upanuzi huu inatoa hakikisho la upatikanaji wa intaneti).

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Ukosefu wa mtaji umelifanya Shirika kutofikia malengo ukilinganisha na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na kampuni nyingine za simu hapa nchini hasa Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel;

(ii) Sheria na kanuni zisizo rafiki kibiashara kama vile za manunuzi ya umma na ajira kwa watumishi ambapo kwa sasa Shirika halina maamuzi ya mwisho na uwezo wa kuajiri wafanyakazi wapya; na

(iii) Kasi ndogo ya kuunganisha wateja.

**(c) Shirika la Posta – TPC**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya shirika ni kama yafuatayo: -

(i) Katika kipindi hiki Shirika limefanikiwa kuzalisha mapato ya jumla ya Tshs. **33,728,128,020** sawa na asilimia **82.38** ya lengo na faida ya jumla ya Tshs. **2,078,611,054** sawa na asilimia **69.29** ya lengo.

(ii) Tanzania kupitia Shirika la Posta imefanikiwa kuwa mwenyeji wa mikutano mikubwa miwili ya Umoja wa Posta Duniani;

(iii) Shirika limefanikiwa kununua magari mapya 14 kwa ajili ya kuimarisha jukumu la usafirishaji wa nyaraka, barua, vifurushi, vipeto na mizigo;

(iv) Shirika limefanikiwa kushiriki katika kufanikisha zoezi la sensa ya watu na makazi kwa kusafirisha na kusambaza vishikwambi na vifaa vingine;

(v) Shirika linatarajia kufanya uwekezaji wa kumilikisha baadhi ya viwanja vyake ili kupata mtaji;

(vi) Kuwa mshindi wa kwanza wa sekta ya usafirishaji *(courier)* katika maonesho ya kitaifa ya 46 sabasaba mwaka 2022; na

(vii) Shirika limeanzisha vituo vitatu vipya navyo ni Tanga, Mbeya na Mwanza ambapo kupitia vituo hivi, zaidi ya wananchi 100,000 wamepata huduma za NIDA, RITA, UHAMIAJI, TRA, BRELA, NHIF, NSSF, PSSF, POLISI n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto zilizobainika ni: -

(i) Shirika linalemewa na deni la jumla ya shilingi **bilioni 26.8** kutokana na kushindwa kuwasilisha kodi, riba mbalimbali kwa wakati (*PAYE, SDL,* na *VAT*) kati ya mwaka 2007 na mwaka 2016; na

(ii) Shirika kuwa na mtaji hasi wa uendeshaji (working capital) wa shilingi **bilioni 35.2** kwa hesabu za mwaka wa Fedha 2021/22.

**(d) Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano Inayotekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF**

**Mheshimiwa Spika,** (UCSAF) inatekeleza miradi Sita (6) ya usambazaji wa huduma za mawasiliano katika jumla ya Kata 247 zinazojumuisha vijiji 371. Mradi utagharimu jumla ya Shilingi bilioni **83.85** utakapokamilika. Kati ya fedha hizo, ruzuku ya Serikali kupitia UCSAF ni Shilingi bilioni **61.05** sawa na asilimia **72.8** ya gharama za miradi, Shilingi bilioni **22.8** sawa na asilimia **27.2** kinachangiwa na Shirika kupitia vyanzo vya ndani vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kasi ndogo katika ujenzi wa minara nchini katika utekelezaji wa mradi. Mkataba uliosainiwa unaonesha kata 713 zitajengwa minara 758. Hadi kufikia Disemba 2023, minara 15 tu sawa na asilimia **2** imejengwa ambapo minara 6 tayari imekamilika na imeanza kutoa huduma za mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa maoni kuwa, kasi ya utekelezaji wa minara ni ndogo hivyo inasisitiza kuongeza nguvu zaidi ili kuwezesha vijiji vingi kupata minara.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inabainisha mtazamo na maoni ya jumla kutokana na matokeo ya Shughuli zisizotekelezwa na Kamati. Lengo lake ni kujulisha masuala mbalimbali yaliyobainika kwa kipindi cha mwaka mzima na kuonesha maoni ya jumla. Aidha maoni hayo yanajenga msingi wa hoja ya Kamati kuhusu mambo ya kufanyiwa kazi iwapo Bunge litaridhia.

### 3.2 Mtazamo na Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi uliofanyika, mambo mbalimbali yaliyobainika yamefafanuliwa ndani ya Taarifa hii. Kwa kuzingatia ufafanuzi huo Kamati ina mtazamo na maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

(i) Suala la LATRA na Jeshi la Polisi kuwa na mgongano wa kimajukumu linalostahili kupatiwa ufumbuzi

(ii) Upungufu wa Watumishi kwa LATRA, TAA, MSCL, TANROADS, TTCL na TBA unahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuepuka athari zake kwenye ufanisi na tija ya taasisi hizo.

(iii) Changamoto za TPA zinazohusu kukosekana kwa mifumo ya TEHAMA inayounganisha wadau na hali isiyoridhisha ya miundombinu ya bandari zinastahili kutatuliwa

(iv) TPA isipowezeshwa kubaki na sehemu ya fedha inayokusanya kwa kutoza huduma za gati, inaweza kuendelea kuwa na uwezo mdogo kifedha. Hali hiyo itaathiri fursa ya Serikali kuongeza mapato kutokana na miundombinu ya bandari kuwa na uchakavu;

(v) Tija ya MSCL na manufaa ya kuwa na kampuni hiyo ni mambo yanayoweza kuongezwa na kuimarishwa kwa kutatua changamoto ya upungufu wa fedha na uwezo wa kampuni hiyo kukarabati meli zake kwa wakati;

(vi) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ni taasisi inayohitaji kuongeza ufanisi na kuchangia uchocheaji wa shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, kutokutatuliwa kwa changamoto za uchakavu wa miundombinu ya viwanja vya ndege na changamoto ya kukosekana kwa sheria mahususi ya usimamizi na uendeshaji kunaweza kuwa kikwazo cha ufanisi wa mamlaka hiyo.

(vii) Dhamira ya kuanzishwa kwa TANROADS na manufaa ya ujenzi na ukarabati wa barabara ni mambo yanayohitaji kutiliwa mkazo kwa kutatua tatizo la ufinyu wa bajeti ya TANROADS na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya barabara nchini.

(viii) Kutokutatua changamoto za TBA kuhusu upungufu wa mtaji na tatizo la wapangaji wengi wa TBA kutokulipa kodi ni jambo linalochangia kasi ndogo ya uwekezaji wa TBA kwenye majengo.

(ix) Suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linastahili hatua madhubuti za kudhibiti. Kutokudhibiti uhalifu huo ni jambo linalosabisha madhara kwa jamii, ustawi na maadili.

(x) Suala la mzigo wa madeni kwa shirika la Posta, kasi ndogo ya ujenzi wa minara ya mawasiliano na TTCL kushindwa kujiendesha kibiashara yanastahili kauli madhubuti ya Bunge kwa lengo la kuboresha sekta ya mawasiliano.

### 3.3 Mapendekeo

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo niliyoyatoa, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie ufafanuzi nilioutoa, na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Miundombinu. Hoja hii inaliwezesha Bunge kusimamia shughuli za umma kwenye sekta ya Uchukuzi, Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Mawasiliano. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja katika maeneo matano kama ifuatavyo: -

**SEKTA YA UCHUKUZI**

**3.3.1 Mgongano wa Majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)**

**KWA KUWA**, Mgongano wa majukumu baina ya Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Aridhini umebainika kuwa miongoni mwa changamoto, na kwamba, matumizi ya mifumo ya TEHEMA isiyosomana katika udhibiti wa shughuli za uchukuzi inasababisha usumbufu na kero kwa wananchi**,**

**NA KWA KUWA**, Mgongano huo wa majukumu na changamoto hizo za mifumo –

(i) Zinaathiri ufanisi katika usimamizi wa Sekta ya uchukuzi; na

(ii) Ni kero katika shughuli za umma kwenye sekta ya Uchukuzi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,**

(i) LATRA, kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi, TANROADS na TABOA ifanye mapitio ya kanuni zilizopo;

(ii) Serikali isimamie uboreshaji wa Mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na LATRA; na

(iii) LATRA na Jeshi la Polisi washirikiane kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inayotumika kwenye vyombo hivyo inaoanisha na kuwianishwa kwa lengo la kuondoa tofauti zisizostahili.

### 3.3.2 Upungufu wa Watumishi Ikilinganishwa na Mahitaji ya Ufanisi wa LATRA

**KWA KUWA**, LATRA yenye dhima ya kusimamia huduma za usafiri ardhini ili kuwezesha huduma zilizo salama na za uhakika, inakabiliwa na upungufu wa watumishi,

**NA KWA KUWA**, Upungufu wa watumishi unakwamisha uwezo wake wa kutoa leseni, kuzifuatilia na kukuza ushindani kwa ajili ya ustawi wa watanzania,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa LATRA inaajiri watumishi wa kutosha.

### 3.3.3 Malalamiko Kuhusu Ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

**KWA KUWA,** yapo malalamiko kuhusu ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania kutokana na:

(i) Kutokamilika kwa mifumo ya TEHAMA inayopaswa kuwaunganisha wadau; na

(ii) Hali isiyoridhisha ya miundombinu inayowezesha uchukuzi wa shehena kutoka bandarini,

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo inayolalamikiwa, inaweza kusababisha –

(i) Mlundikano wa shehena bandarini; na

(ii) Kukwama kwa azma ya kuongeza uboreshaji wa huduma zinazotolewa na mamlaka ya bandari,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia Kwamba,

(i) Mamlaka ya Bandari Tanzania iongeze kasi ya kuboresha miundombinu ya barabara na njia ya reli inayoingia na kutoka bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Serikali ikamilishe mchakato wa ujenzi wa reli ya Kisasa kutoka Mtwara – Bambabay na ujenzi wa bandari ya Kisiwa Mgao mkoani Mtwara;

(iii) Serikali ikamilishe mifumo ya TEHAMA ili kuunganisha wadau wote bandarini; na

(iv) Serikali ijenge gati 2 za dharura (kwenye gati 0) katika Bandari ya Dar es Salaam ambazo zitakuwa na uwezo wa kubeba mzigo mkubwa uliopo bandarini;

**3.3.4 Mamlaka ya Bandari Tanzania Kutobakiziwa Sehemu ya Fedha Inazokusanya Kutokana na Tozo za Gati**

**KWA KUWA,** Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zinaonesha kwamba, mapato yanayokusanywa na TPA kutokana na tozo za gati yanachukuliwa na Serikali bila TPA kubakiziwa kiasi chochote,

**NA KWA KUWA,** Utaratibu huo unaminya uwezo wa TPA kufanya maboresho ya miundombinu katika magati hayo, jambo linaloweza–

(i) Kupunguza ufanisi wa huduma za bandari katika magati hayo; na

(ii) Kuipunguzia Serikali uwezekano wa kupata mapato zaidi kutokana na huduma za bandari,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwape TPA kiasi cha shilingi **Bilioni 35** kwa kila mwezi, kutoka kwenye makusanyo ya *wharfage.*

**3.3.5 Changamoto za Uendeshai wa Huduma za Meli - MSCL**

**KWA KUWA**, Kampuni ya Huduma za Meli - MSCL inakabiliwa na changamoto kama vile –

(i) Upungufu wa fedha;

(ii) Kukosekana kwa uhalisia wa gharama za mapato na uendeshaji; na

(iii) Meli nyingi kuwa matengenezo kwa muda mrefu,

**NA KWA KUWA,** Changamoto hizo zInaathiri huduma muhimu zinazotolewa na Kampuni ya Meli (MSCL),

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iongeze fedha kwa MSCL ili iimarike na ijiendeshe kibiashara;

(ii) Serikali iharakishe matengenezo ya Meli mfano ya MV. Lihemba na MV. Mwongozo;

(iii) MSCL ijipange kuleta meli itakayoweza kubeba mzigo utakaoletwa na reli ya kisasa (SGR) pindi itakapoanza kutoa huduma; na

(iv) Serikali iisaidie MSCL kupeleka Meli ya Uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

**3.3.6 Changamoto Zinazoikabili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA)**

**KWA KUWA**, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inakabiliwa na changamoto za:

(i) Upungufu wa Watumishi;

(ii) Wakandarasi kutokulipwa kwa wakati

(iii) Uchakavu wa miundombinu, Majengo, Mitambo

(iv) Miradi yake kutekelezwa kwa namna isiyonufaisha jamii kwa utaratibu wa CSR;

(v) Kukosekana kwa Sheria inayoweka mfumo wa uendeshaji wa mamlaka,

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo inakwamisha ufanisi wa uendeshaji wa mamlaka na kupunguza kasi ya uendelezaji wa Viwanja vya Ndege nchini,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iwezeshwe kuajiri watumishi na kuongeza idadi ya watumishi;

(ii) Serikali iiwezeshe Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kifedha ili iweze kurekebisha miundombinu na kuwalipa Wakandarasi kwa wakati;

(iii) Serikali iweke utaratibu wa mikataba ya watoa huduma na Wakandarasi kutekeleza wajibu wa kurudisha fadhila kwa jamii (CSR);

(iv) Serikali iongeze kasi ya kukamilisha mchakato wa kuwa na Sheria mahsusi inayohusu uendeshaji, usimamizi na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege;

(v) Serikali iibakizie TAA angalau asilimia **40** ya makusanyo ya tozo kwa wasafiri (*Passengers Services Charge)* katika Viwanja vya Ndege; na

(vi) TAA ihakikishe kuwa Viwanja vyote vya Ndege nchini vinakuwa na hati miliki.

### 3.3.7 Changamoto za Usimamizi wa Barabara zilizo chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mfuko wa Barabara - RFB

**KWA KUWA**, usimamizi na ujenzi wa barabara nchini unakabiliwa na–

(i) Ufinyu wa bajeti ya ujenzi na matengenezo;

(ii) Uvamizi wa maeneo ya barabara nchini; na

(iii) Upungufu wa watumishi wa kutosha kuwezesha tija iliyokusudiwa kwa kuanzisha *TANROADS*.

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo inakwamisha dhamira ya kuanzisha TANROADS na kupunguza manufaa ya matengenezo na ukarabati wa barabara,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iongeze fedha za ujenzi na ukarabati wa barabara ikiwemo madaraja;

(ii) Serikali ilipe madeni ya Wakandarasi na Waandishi Washauri kwa wakati ili kuondoa ongezeko la gharama zinazosabishwa na riba;

(iii) Serikali iisaidie TANROADS kuingia mikataba uwe katika mfumo wa kiasi cha fedha kutobadilika wakati wa mradi *(fixed amount)* ili kuepusha kupanda kwa gharama;

(iv) TANROADS idhibiti wizi na uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara;

(v) Serikali iwahi kufanya tathimini za mali na ardhi kwa ajili ya kupisha ujenzi, pia maeneo ambayo yanaonekana hayahitajiki kwa sasa yaachwe kwa wananchi ili yaendelezwe; na

(vi) Serikali itumie ujenzi wa barabara za mchepuo *(bypass)*, pamoja na kuweka alama za biconi kwenye mipaka ya barabara.

### 3.3.8 Kasi Ndogo ya Uwekezaji katika Majengo chini ya Wakala wa Majengo (TBA)

**KWA KUWA**, Wakala wa Majengo Tanzania imebainika kuwa na kasi ndogo ya uwekezaji kutokana na:

(i) Upungufu wa mtaji;

(ii) Wapangaji kutokulipa kodi kwa wakati; na

(iii) Upungufu wa watumishi.

**NA KWA KUWA,** Hali hiyo inaweza kuathiri uwezo wa Wakala kutekeleza agizo la ujenzi wa nyumba 10,000 jambo linalokwamisha manufaa ya nyumba hizo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,** Serikali -

(i) Itenge fedha za kutosha kuiwezesha TBA kufanikisha azma ya ujenzi wa majengeo ya makazi na ofisi;

(ii) Iweke msukumo unaoisaidia TBA kulipwa madeni ya pango zinazodaiwa Taasisi za Serikali;

(iii) Isimamie TBA ipasavyo ili iajiri watumishi wanaohitajika; na

(iv) Iwezeshe na kuisimamia TBA ili iendelee kutumia ubunifu zaidi wa kujenga majengo na kuingia mikataba yenye tija na Sekta binafsi katika uwekezaji.

### 3.3.9 Utapeli na Uhalifu Mwingine wa Kimtandao

**KWA KUWA**, Suala la utapeli na uhalifu mwingine wa kimtandao linapaswa kupatiwa ufumbuzi na TCRA linaendelea kuwepo,

**NA KWA KUWA**, Suala hili linalotokana na maendeleo ya TEHAMA linaathiri uchumi, jamii, ustawi na maadili,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iimarishe udhibiti wa uhuru wa mitandao kwa kuzingatia umuhimu wa demokrasia na uhuru wa kuzingatia mipaka; na
(ii) TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi iweke mikakati madhubuti inayozihusisha kampuni za simu kukabiliana na uhalifu wa kimtandao.

### 3.3.10 Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL), kushindwa kujiendesha kwa biashara

**KWA KUWA**, Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inayopaswa kujiendesha kibiashara inashindwa kutokana na:

(i) Taratibu za ajira ya watumishi wake kufungwa na taratibu za Sekta ya umma isiyoongozwa na misingi ya kibiashara;

(ii) Upungufu wa fedha kwa ajili ya uwekezaji katika biashara ndani ya Sekta; na

(iii) Uwezo mdogo wa kampuni kuunganisha wateja

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ihakikishe kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania inawezesha kifedha ili iweze kuwa na mtaji wa kujiendesha kibiashara;

(ii) Mfumo wa Sheria za ajira Serikalini uangaliwe ili kuruhusu kampuni zinazojiendesha kibiashara kuwa na taratibu za ajira zinazoruhusu kuunda ushindani; na

(iii) Kampuni ya Simu Tanzania iongeze uwezo wa kuwa na kasi ya kutosha kuunganisha wateja;

**3.3.11 Mzigo wa Madeni na Mtaji Mdogo wa Shirika la Posta Tanzania**

**KWA KUWA**, Shirika la Posta Tanzania limebainika kuwa na mzigo mkubwa wa madeni na mtaji mdogo wa kuweza kujiendesha,

**NA KWA KUWA**, Licha ya Serikali kufanya jitihada kubwa ya kufufua Shirika hilo, bado changamoto hizo zinakwamisha maendeleo ya Shirika kibiashara,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali ibebe deni inalodaiwa Shirika la Posta Tanzania la Shilingi **bilioni 26.8** ili kusafisha mizani ya Shirika na kuliwezesha kukopesheka;

(ii) Shirika libuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiendesha kibiashara;

(iii) Serikali iendelee kuisaidia Posta ili iweze kulipwa madeni wanayodai kwenye Taasisi za Serikali; na

(iv) Serikali iongeze mtaji kwa Shirika la Posta na kuhakikisha linapata kamisheni kwa kila mzigo.

**3.3.12 Kasi Ndogo ya Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano**

**KWA KUWA**, Ujenzi wa minara ya Mawasiliano umebainika kuwa na kasi ndogo kutokana na mchakato mrefu wa kiutaratibu,

**NA KWA KUWA**, Hali hiyo inakwamisha lengo la Serikali kufikisha mawasiliano nchini kinyume na matarajio ya wananchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge inaazimia kwamba, Serikali –

(i) Kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote iongeze kasi ya kutekeleza ujenzi wa minara ya mawasiliano;

(ii) Iharakishe ujenzi wa chuo cha TEHAMA Dodoma na kutengeneza *ICT hubs* nchini; na

(iii) Ifanye mapitio ya taratibu za mchakato wa zoezi la ujenzi wa minara ili kuboresha taratibu hizo kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA HOJA

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha Taarifa hii kwa kutambua utaratibu uliowekwa na Bunge wa kuzitaka Kamati za Kudumu za Bunge kuripoti shughuli zake kwa kipindi cha mwaka. Utaratibu huu unalitaka Bunge kuwa katika nafasi ya kutambua hali ilivyo katika sekta mbalimbali. Ushauri huu wa Bunge kwa Serikali unaweza kufanyiwa kazi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika**, naamini kwa maelezo haya na ufafanuzi nilioutoa, utaliwezesha Bunge kujadili inavyostahili na kutoa ushauri kwa Serikali ili kuboresha shughuli na kuongeza tija katika sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kumshukuru kwa dhati Mhe. Innocent Bashungwa (Mb), Waziri wa Ujenzi akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Eng. Msongwe Geofrey Kasekenya (Mb), pia Mhe Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi akishirikiana na Naibu Waziri Mhe David Mwakiposa Kihenzile. Vile vile Mhe. Nape Moses

Nnauye (Mb) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Eng. Kundo Andrea Mathew (Mb) kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati katika kutimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuwawezesha Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kutoa ushirikiano kwenye Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa niaba ya Sekretarieti na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kujituma wakilenga kutoa ushauri unaofaa kwa Bunge. Kufanya hivyo kutaiwezesha Serikali kuboresha maeneo mbalimbali na kuendelea kukidhi matarajio ya wananchi kwa Serikali yao. Kwa kutambua mchango wao, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb - **M/ Mwenyekiti**
3. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb – **Mjumbe**
4. Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb "
5. Mhe. Mbarouk Juma Khatibu, Mb "
6. Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb "
7. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb "
8. Mhe. Angelina Malembeka, Mb "
9. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb "
10. Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb "
11. Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb "
12. Mhe. Amina Ali Mzee, Mb "
13. Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb "

14. Mhe. Mwantumu Dau Haji, Mb "
15. Mhe. Santiel Erick Kirumba, Mb "
16. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb "
17. Mhe. Abubakari Damian Assenga, Mb "
18. Mhe. Slyvia Francis Sigula, Mb "
19. Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge "
20. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb "
21. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby Mb "
22. Mhe. Fredrick Lowassa, Mb "

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada yakusema hayo, naliomba Bunge lako tukufu lipokee na kuijadili Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Januari 2024, ili hatimaye kupitisha mapendekezo ya Kamati yawe ushauri wa Bunge kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
**5 FEBRUARI, 2024**

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono, ahsante Mwenyekiti kwa kusoma vizuri. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza michango. Tutaanza na Mheshimiwa Mama Kilango, ajiandae Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ajiandae Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa hiyo, nimeiangalia vizuri naomba kuchangia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kutoa pole kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba, imejenga barabara nchi nzima lakini tumepata *El Nino* ambayo imevuruga barabara pamoja na mengi makubwa lakini lazima tujue kwamba, sisi tunapanga Mwenyezi Mungu ndiye anayepanga vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia upande wa *TANROADS*. Kama Mheshimiwa Mwenyekiti alivyosoma taarifa ya Kamati, utaona kwamba changamoto kubwa waliyonayo *TANROADS* ni fedha za ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja, ukiangalia bajeti ya 2023/2024 *TANROADS* amepewa pesa trilioni 1.4 tu kwa kujenga barabara, madaraja na matengenezo ya barabara ambazo zilikwishajengwa kwa nchi nzima, sasa naomba nitoe picha ya changamoto ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, *TANROADS* ina mzigo mkubwa wa barabara zilizoisha muda wa matumizi. Mfano wa barabara hizo ni kama Barabara ya Dodoma – Iringa, Barabara ya Dodoma – Mwanza, Dar es Salaam - Mtwara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS* ina tatizo kubwa la barabara ambazo zimekwisha muda wa matumizi. Nikisema zimekwisha muda wa matumizi ni kwamba, barabara hizi zinakuwa zimejengwa zitumike mfano kwa miaka 20 lakini miaka 20 imefika barabara hazifanyiwi matengenezo. Barabara hizo ziko 71. Barabara 71 ambazo gharama yake ni 3,026,007,076,000. Naomba kurudia, barabara ambazo zimekwisha muda wake ni barabara 71 ambazo zilibidi zitengenezwe kwenye bajeti ya 2023/2024 na barabara hizo zina gharama ya 3,026,007,076,000. Urefu wa barabara hizo 71 zina urefu wa kilometa 2840.68. Barabara hizi 71 hazina hali nzuri kabisa kimatumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ambacho kinaikwaza sana *TANROADS* ni ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi na wahandisi. Miradi 94 imekamilka, wakandarasi wanadai shilingi bilioni 386.608. Pili, miradi ya barabara

inayoendelea ipo 69 yenye urefu wa kilometa 4291.61 gharama ni bilioni 392.68. Kwa haya niliyoyazungumza na bajeti iliyotolewa ya trilioni 1.4 ni dhahiri kabisa kwamba *TANROADS* wanashindwa kufanyakazi inavyostahili. Kwa hivyo basi, Kamati na kama alivyoongea Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa muone umuhimu wa kuifanya *TANROADS* ifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kama ingeweza kupewa trilioni tano ambazo trilioni tatu ziende kwenye ujenzi wa barabara na trilioni mbili ziende kwenye matengenezo ya barabara hasa tukiona ni jinsi gani ambavyo mvua za *El-Nino* zimeharibu barabara za nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijitahidi tukamwita mpaka Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndani ya kikao chetu, tukamweleza vya kutosha ili aone umuhimu wa kuiangalia *TANROADS*. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja upande wa *TPA*. Upande wa *TPA* napo kuna matatizo. Tuchukue mfano wa *TPA* ni kama ng'ombe ambaye anatoa maziwa mengi sana, hata hivyo, ng'ombe anayetoa maziwa mengi anahitaji apewe chakula cha kutosha, anahitaji apewe virutubisho ili ng'ombe yule aweze kutoa maziwa ya kutosha. *TPA* inachangia asilimia 15 ya pato ghafi kila mwezi kwenye Pato la Taifa, *TPA* inachangia asilimia 70 ya faida yake kwa mwaka kwenye Pato la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye utendaji kazi wa *TPA*, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita 2020/2021, 2021/2022, 2022/2023; idadi ya meli zilizohudumiwa zimekuwa zikiongezeka kwa asilimia 15.8. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 idadi ya meli zilizopokelewa ni sawa na asilimia 118.1 ya lengo la mwaka. Tuende kwenye mapato ya *TPA*. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023 mapato ya *TPA* yameongezeka kwa wastani wa asilimia 24.72 kwa mwaka kutoka shilingi bilioni

896.952 zilizopatikana kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi trilioni 1.390 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hayo ni mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa Serikali ikaona kwamba, *TPA,* kweli ni kama ng'ombe anayetoa maziwa, anapeleka asilimia 15 na asilimia 70 ya ziada yake kwa mwaka kwenye Mfuko wa Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina. Sasa ni vema Serikali ikaona kwamba, huyu ng'ombe anayetoa maziwa akikamuliwa moja kwa moja bila kupewa majani ya kutosha na virutubisho, atakufa na hataisaidia hii Serikali. Sisi tunapendekeza hivi, Serikali ione umuhimu wa kumpa *TPA* bilioni 35 kila mwezi kwa ajili ya kujenga na kuboresha miundombinu ya Bandari za Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtaturu, ajiandae Mheshimiwa Mlaghila.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye taarifa ya Kamati yetu ya Miundombinu ambayo tunayo mezani ambayo kimsingi ni taarifa ya Serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja. Nami na–*declare* kwamba ni Mjumbe wa Kamati nasi tulipata taarifa hizi na tulisomewa. Tuliihoji Serikali kwenye Kamati yetu kama ambavyo ulitupata ruhusa ili tuweze kupitia taarifa za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi kwenye taasisi zetu ambazo leo zimetoa huduma mbalimbali katika maeneo ya wananchi. Taarifa ambayo imetajwa, pamoja na changamoto lakini kuna fedha zimekwenda za kutekeleza miradi mbalimbali, tunaipongeza Serikali na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa utayari wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha taarifa nitaanza kwenye eneo la Mamlaka ya Bandari Tanzania. Kama ambavyo wote tunajua Mamlaka ya Bandari ya Tanzania kwa maana ya

bandari ndiyo lango kuu la Uchumi, tumekuwa tukitegemea kukusanya fedha nyingi kupitia bandari yetu. Katika kipindi cha taarifa tumejulishwa kwamba tumeweza kuhudumia nyongeza ya tani kwa maana ya asilimia 17.5 kuacha ile ya nyuma ambayo ilikuwepo kwa mwaka uliopita. Tumeweza kuhudumia kutoka tani milioni 5.81 kwenda mpaka tani milioni 6.83. Maana yake ni kwamba pamoja na yote kuna hatua kubwa tumepiga katika kuhudumia shehena katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Kama haitoshi, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 310.78 hadi bilioni 365.12 katika hiki kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zote hizi na kwa sababu asilimia 90 ya mzigo wote unaosafirishwa unatoka kwenye Bandari ya Dar es Salaam, maana yake Bandari ya Dar es Salaam ikiboreshwa tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuingiza mapato ya Serikali. Kwa hiyo, kama ambavyo Mheshimiwa Mwenyekiti amesoma kwenye taarifa yetu, tumegundua baadhi ya mambo mbalimbali ambayo yanakwamisha suala hili la usafirishaji wa mizigo ikiwemo kuwepo kwa foleni kubwa ya meli katika Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili pamoja na juhudi zote bado tumeona kuna tatizo kubwa la ushushaji wa mizigo kwa kasi. Kwanza, lazima tukubali kwamba Bandari ya Dar es Salaam imekuwa kivutio kikubwa cha ukanda huu wa nchi nane. Ndiyo maana katika kipindi hiki wanakuja wateja wengi, kipindi hiki cha Desemba kuanzia Novemba mpaka Januari kumekuwa na mizigo mingi inapokelewa kwa sababu ya msimu, kwanza ni msimu wa kilimo, nchi yetu imekuwa ikihamasisha wakulima kutumia mbolea katika suala la kilimo. Pili, tumekuwa tukitumia mbegu bora maana yake zikitoka nje ya nchi, kuleta katika nchi yetu zinakuja kwa njia ya meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuona meli nyingi pia ni mafanikio kwa sababu watu wameona *destination* ya Dar es

Salaam ni nzuri katika kushushia mizigo yao, hayo ni mafanikio makubwa sasa lazima yazae changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tuliposikia taarifa tuliwahoji wenzetu wa *TPA* wakatuambia kwamba wao wanatakiwa waongeze gati 12 mpaka 15 ili kuoongeza uwezo wa ushushaji wa meli nyingi kwa wakati mmoja, hivyo kazi hii inahitaji uwekezaji. Kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia kwamba, kama unataka kumkamua ng'ombe basi lazima umlishe chakula cha kutosha ambacho ni majani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala pia la ushushaji mafuta. Katika gati ile ya mafuta ya *KOJ*, eneo lile ni dogo na meli za mafuta pia zimekuwa zikisubiri. Utatuzi wake ni kwamba lazima ujenge eneo lingine la kuhifadhia mafuta mbayo ni *Single Receiving Terminal* ambayo wanaita *(SRT)*. Ukijenga hii *Single Receiving Terminal* utasaidia kuongeza kasi ya ushushaji wa mafuta lakini pia unaweza ukafanya *storage* wakati unasubiri wateja ambao wameagiza mafuta hayo kuyapokea, pia itapunguza gharama ya mafuta nchini katika soko la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka niseme kama walivyosema wenzangu kwamba, lazima Serikali ione namna ya kuongeza fedha kwa ajili ya kusaidia hii miradi ambayo tumeisema ili *TPA* waweze kujenga gati za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi tumeomba kwamba *wharfage* hii ambayo inatajwa, huko nyuma *TPA* walikuwa wanaachiwa na Serikali. Hii ni kama vile kodi tu ya kufanya *packing* ya meli katika eneo la bandari na wala haihusiani na mapato ya *TRA*. Huko nyuma walikuwa wanafanya wenyewe, wanakusanya hizi fedha na wanafanya miradi mbalimbali ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maana yake Serikali inavyokusanya hela yote inapeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, inaifanya *TPA* ishindwe hata kutaka kununua chochote mpaka

iiombe kwanza Hazina. Kwa hiyo, niombe kama ilivyosemwa kwenye taarifa *wharfage* irudi waachiwe *TPA* waweze kukusanya na wakikusanya watakuwa na uwezo wa kuendeleza miundombinu ya bandari na kuvutia zaidi ushushaji wa mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, tuwaachie asilimia 30 ambayo itabaki kwenye bandari ili iwasaidie, kwa sababu hauwezi kuwa na ushindani kama hauna fedha. Kwa hiyo, ninaomba sana jambo hili lizingatiwe ili tuweze kuondokana na changamoto ambayo wanayo wenzetu wa mamlaka ya bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la *SGR*. *SGR* itakuwa ni *support* kubwa ya kuondoa mzigo bandarini, *SGR* haijakamilika kwa muda mrefu, ninaomba kwamba wakikamilisha *SGR* watakuwa na uwezo wa kutoa tani zaidi ya milioni 17 kwa wakati mmoja kwa mwaka. Kwa hiyo, watapunguza msongamano wa Dar es Salaam, malori mengi pia hata kuharibu barabara zetu ambazo zinajengwa. Kwa hiyo, ninaomba sana kama inawezekana wenzetu wa *SGR* waharakishe ili waweze kukamilisha uwezekano wa kuanza kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni upande wa *TANROADS*. Imeelezwa sana hapa kwamba *TANROADS* wamekuwa wanasaidia sana barabara zetu, kama haitoshi Serikali inategemea sana miundombinu ili iweze kupeleka huduma katika nchi hii. Kama miundombinu siyo imara hakuna kitakachofanyika, watu hawatasafiri, uchumi hautakwenda mbele. Ombi langu ni kwamba tujitahidi sana wenzetu wa *TANROADS* waongezewe fedha ambazo wanaziomba zitakazosaidia kwenda kuboresha barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zilizopitishwa na Bunge zimesainiwa kupitia mradi ule au utaratibu wa *EPC+F,* barabara zenye urefu wa kilometa 2,035 mpaka leo barabara hata moja haijaanza kazi, haijaanza kujengwa na tumebakiza miezi sita ya bajeti hii kukamilika lakini changamoto iliyopo ni kwamba, wenzetu wanahitaji fedha zaidi ya trilioni 3.75 bila *VAT* ili waweze kuanza

miradi hii. Miradi hii ni pamoja na barabara yenye urefu wa kilomita 460 kutoka Singida – Kwa Mtoro kwenda mpaka kule Tanga. Barabara hii ni miongoni mwa barabara saba zilizopitishwa katika kujengwa. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu miundombinu ni uchumi ninaiomba sana Serikali iweke jicho katika kuhakikisha kwamba barabara hizi zinakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ninaunga mkono hoja ya Kamati yetu ili iweze kupita katika Bunge hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Mlaghila jiandae Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, jiandae Mheshimiwa Kalogeris.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nami kupitia Bunge hili Tukufu nipaze sauti ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa miradi mikubwa anayoifanya Wilayani kwangu na kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichangie kwenye eneo la bandari na hasa eneo ambalo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii, nayo ni kwenye upakuaji. Ili bandari ifanye kazi vizuri ni lazima Watendaji na Watumishi wa Bandari wawe *committed* na wafanye kazi vizuri sana. Hili nataka niseme kwa watumishi wetu na viongozi wetu walioko pale bandarini wanafanya kazi nzuri ndiyo maana mpaka sasa tunalalamika kwamba meli ni nyingi sana, haya hayajatokea hivi hivi, ni kwa sababu watumishi wetu wakiongozwa na Mkurugenzi wa *TPA* wamejitahidi kuvutia wawekezaji wengi, wafanyabiashara wengi, lakini pia wamehakikisha *shipping lines* nyingi zimeongezeka kuja Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu nilikuwa naangalia taarifa ya habari wanatuambia wamepata *shipping line* ambayo inatoa mzigo China moja kwa moja mpaka Dar es Salaam bila kupitia bandari yoyote ile. Haya ni mafanikio makubwa sana. Tunataka

tuseme Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri sana mpaka tunapata mafanikio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuendelee na ufanisi huu, ni lazima *TPA* wajiendeshe kibiashara. Makampuni mengi ambayo yanafanya biashara ya upakuaji kwenye bandari zikiwemo hata *DP World* ni makampuni ambayo yana asilimia kubwa ya Serikali kama ilivyo *TPA,* lakini kwa sababu Serikali zao ziliwawezesha na kuwapatia fedha wajiendeshe kibiashara, ndiyo maana wameweza mpaka kuvuka kwenda bandari nyingine na sasa hivi wanaonekana ni wakubwa. Nasi tunataka tufike huko, *TPA* nayo ianze kuvuka mipaka, ifanye kwa ufanisi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mfano, tukiwapatia fedha hasa za *wharfage* hata shilingi bilioni 35 mpaka 40, wanao uwezo wa kuanza sasa kujiendesha kibiashara, benki zikawaamini wakaweka fedha kwenye benki zikaanza kufanya kazinao kwa ujumla mpaka wakaweza kuwekeza kujenga magati mengine na kuhamisha eneo lile la Kurasini kwenda Kigamboni halafu hapa tukajenga magati mawili mpaka manne ili meli ziweze ku-*park* pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali hili ilifanyie kazi. Kwa vile tumeshaomba lifanyiwe kazi, ninafikiri sasa ni wakati sahihi wa kufanyia kazi na *TPA* kuanza kufanya kwa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwa upande wa *TANROADS.* Wenzangu wote wameongelea kwamba tayari tunajiona tuna pesa kidogo kwenye bajeti za uendeshaji wa *TANROADS.* Naomba nikumbushe kwamba pamoja na ndege na reli, lakini uchumi wa nchi hii, mshipa ambao unafanya kazi kuilisha nchi hii ni barabara. Hatuna namna ya kukwepa ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kuna upungufu mkubwa. Ili tujenge barabara hizi, tunahitaji shilingi trilioni tano na hizi

tungeziomba kwa mwaka huu bajeti inapokuja angalau ifike kwenye shilingi trilioni tano ili tuweze kufanya matengenezo na kujenga barabara ambazo ziko kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ubunifu uwe mkubwa sana katika kutafuta mapato hasa kwenye Mfuko wa Barabara. Tumezoea kwenye mafuta tu, naomba twende mbali tuangalie vyanzo vingine kama wenzetu wanavyofanya. Kuna *distance tolling,* nayo ni nzuri sana, inao uwezo wa kuongeza mapato. Pia tunao uwezo wa kutengeneza barabara za kulipia ambazo zitaenda kuongeza malipo kwenye Serikali na kufanya mfuko wetu utune. Tunaomba Serikali ihakikishe inakuja na vyanzo vya kutosha ambavyo vitafikia shilingi trilioni mbili ili tuweze kufanya matengenezo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la fidia za wananchi ambako barabara zinapita. Naomba katika hili nipaze sauti. Kuna wananchi wengi barabara zinapita kwenye maeneo yao lakini mpaka leo hii hawajapata malipo. Mfano mzuri ni barabara yangu ya Ibanda kwenda Kajunjumele. Wananchi wameendelea kusubiri malipo na wakati mwingine Serikali iliwapa matumaini kupitia Mkuu wa Wilaya, akasema tarehe tatu mwezi wa Kumi na Moja watapata fedha zao, lakini mpaka leo hawajapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali yetu inapambana na inatafuta fedha kuwalipa wananchi. Tunaomba sana mahali ambako hatuna nafasi ya kujenga kwa sasa tuwaache wananchi waendelee na shughuli zao. Tuwaache wananchi waendelee na shughuli zao kuliko kuwasimamisha huku wakitegemea watapata malipo halafu malipo hayafiki kwa wakati. Tunaomba sana haya mambo yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la fidia ambazo zilikuwa zimeahidiwa. Jumla ya fidia zote ili Serikali iweze kulipa ni shilingi trilioni saba. Hili ni jambo kubwa sana, tunaomba Serikali izipitishe zilipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni ujenzi wa barabara ambao umekuwa ukisuasua, tunaomba sana *TANROADS* na Serikali wasimamie vizuri mikataba iliyopo. Vilevile mikataba iliyopo kwa sasa ninasema haina ufanisi mzuri na haisimami kwa upande wetu. Mheshimiwa Waziri amelazimika kuwaita wakandarasi kuzungumzanao wakati mikataba ndiyo ilitakiwa izungumze. Naona kuna sehemu kuna matobo na upungufu na kuna uwezekano kuna sehemu meno yetu kwenye mikataba ni ya *plastic,* badala ya kuwa meno ya chuma. Naomba hili la mikataba lisimamiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru sana Serikali kupitia Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Fedha walipokuja Kyela kuwapa matumaini Wananchi wa Ikombe ambao hawajawahi kuona gari kwamba sasa wanaenda kutoa shilingi milioni 500 ili wananchi hawa waone gari. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba tuisimamie *TAZARA*. Hao wawekezaji wanaokuja, tunaomba waje na mkataba wetu na Zambia uangaliwe upya. Najua Wazambia wapo hapa, tunataka tuwaambie "*injanji, tuefwaya iyambe*." Hiki ni Kichina cha Zambia. Tunataka reli ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Ulenge, jiandae Mheshimiwa Kalogeris, jiandae Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunichagua katika mwaka huu wa 2024, nitaendelea kumkwepesha Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza wana Kamati wenzangu kwa ajili ya taarifa hii ya

mwaka na kipekee kabisa naipongeza Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa mikakati mizuri endelevu ambayo inaitaka Tanzania yetu kujikwamua katika sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tuliona wiki iliyopita wakati tunachangia ile Miswada mitatu ya Sheria za Uchaguzi na kadhalika, tuliona mijadala ile namna gani ambavyo ilitekwa na suala zima la jinsia na ukatili wa kijinsia na usawa wa kijinsia. Vivyo hivyo sasa hivi hakuna namna ya kurudi nyuma, dunia imeshatekwa katika suala zima la TEHAMA na teknolojia ya habari. Kwa hiyo, nasi kama Tanzania tumeshaingia huko na napongeza Bunge letu hili, tulipitisha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Lengo la sheria ile ni kuhakikisha mwananchi mmoja mmoja anakwenda kunufaika na uchumi wa kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya *initiatives* mbalimbali kuhakikisha nasi tunaingia huko, na hili la sheria ni mojawapo. Naiomba sana na kuishauri Serikali, ihakikishe lile suala la *digital identity* linakwenda kukamilika ili mwananchi mmoja mmoja aweze kunufaika. Hatuwezi kwenda kuingia katika ulimwengu wa kiteknolojia na kunufaika na uchumi wa kidigitali kama kila mwananchi hataweza kuwa na *digital identity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mipango katika hili, niwakumbushe kulisimamia kuhakikisha Watanzania mmoja mmoja wakakwenda kunufaika na uchumi wa kidigitali. Sheria tuliyotunga ya Ulinzi Binafsi, lengo lake kubwa ni kuhakikisha taarifa za mtu binafsi zilizopo sehemu mbalimbali zinaweza kuwa *accessed* pamoja na kuweza kumnufaisha Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sasa hivi unaweza ukaenda benki ukakopeshwa kulingana na kile ambacho tu kinaonekana kiko ndani ya benki, lakini benki inaweza vilevile kumkopesha Mtanzania kwa kutumia fedha zake zinazopita katika simu kila siku. Kwa hiyo, hiyo ndiyo maana halisi ya uchumi wa kidigitali, nasi Tanzania na wananchi mmoja mmoja tukanufaike na

uchumi wa kidigitali kwa kuhakikisha kwanza kabisa nilichokisema, *digital identity* inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ninaishauri Serikali, zipo nchi nyingi duniani ambazo zimeshanufaika na uchumi wa kidigitali. Tutafute *technical assistance*, tutafute ushauri au msaada wa kiufundi, msaada wa kitaalam ili nasi tuweze kunufaika na uchumi wa kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naipongeza tena Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyofanywa na *initiatives* nzuri iliyofanywa kwa kuanzisha Chuo Mahiri cha TEHAMA Jijini Dodoma. Hivi karibuni tumeshuhudia Serikali ikiingia makubaliano na wadau wale ambao watatusaidia kuhakikisha Chuo hiki cha TEHAMA kinakwenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mahali ambapo Serikali hii inafanya jambo kubwa na la maana kwa vijana wa Tanzania, basi ni Chuo hiki cha TEHAMA. Chuo hiki mahiri cha TEHAMA ni jambo moja kubwa sana ambalo Serikali hii inakwenda kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tunafahamu kwamba dunia inakwenda kwenye hiyo inayoitwa *artificial intelligence,* dunia inakwenda katika *robotic technology,* lakini kila mmoja wetu hapa haimaanishi kwa sababu siyo mtaalam wa *ICT* basi huwezi kwenda kusoma kupata uelewa kuhusiana na mambo kama hayo. Kwa hiyo, Chuo hiki siyo kama *Universities* nyingine ambazo zinafundisha labda *degree* ya *ICT* au *degree* ya *Computer Engineering* au *degree* ya *Information Technology,* bali chuo hiki kinakwenda ku-*bridge the gap*. *Gap* iliyokuwepo katika *ICT knowledge* ndiyo lengo la chuo hiki. Kwa hiyo, vyuo vingine vilivyopo nchini viangalie dhamira hii kama kuipa *support,* siyo kama *competitive* kwa vyuo vingine ambavyo vinatoa *course* na mijadala kama hii ya ki-TEHAMA nchini. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa dhamira yake hii kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa chuo hiki mahiri cha TEHAMA nchini, kunakwenda sambamba na kuanzishwa *ICT hubs* katika mikoa yetu, na tayari Mkoa wetu wa Tanga ni miongoni mwa mikoa ambayo inaenda kunufaika na *ICT hubs* kama ambavyo Mbeya itanufaika, Arusha itanufaika, Mwanza itanufaika, Zanzibar itanufaika na Lindi itanufaika. Naipongeza sana Serikali, hapa ndipo mahali ambapo tunaenda kutumia TEHAMA kuhakikisha vijana wetu wanazalisha ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali wote kwamba kuna watu milioni nane Tanzania wanatumia *smart phones,* lakini mafundi wote wanaorekebisha simu zetu zinapokuwa zimeharibika ni wapi hasa ambako wanaenda kujifunza? Hakuna mahali sahihi, wanafanya kama kwa kipaji, wanafanya kama kwa kubahatisha, lakini tukianzisha *ICT hubs,* hapa ndipo ambapo vijana wanaenda kujifunza na kupata uelewa mpana wa kuzalisha vifaa vya ki-TEHAMA na kufanya marekebisho ya vifaa vya ki-TEHAMA, na hapa ndipo ajira za vijana wengi zitazalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, jambo hili la kuanzisha *ICT hubs* kama ambavyo hizi kanda nane zilizochaguliwa zinaenda kutekelezwa, yale malengo Serikali iliyojiwekea kuhakikisha kwamba hivi *hubs* zinashuka kwenye kila wilaya nchini Tanzania, yatekelezwe *in a holistic approach,* ionekane kwamba ni jambo kubwa kwa manufaa ya vijana wa Kitanzania, kwa hiyo, tushirikiane kuanzia katika Wizara ya Mipango jambo hili liweze kusimama, kuliko kulilia minara ya simu ambapo kila siku tunakwenda kupoteza fedha nyingi kwa kutumia simu na hatuzalishi chochote. Hayo ndiyo mambo ambayo kama Taifa tunatakiwa tuyasimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili liangaliwe *in a holistic approach* ili liweze kutimia ndani ya muda mfupi katika Taifa letu, ili vijana wa Tanzania waweze kujiajiri wenyewe. Kwa hiyo ushauri wangu kwa Serikali ni kuhakikisha jambo hili linakwisha kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kuishauri Serikali, sasa hivi kumekuwa na tishio duniani la ku-*attack critical infrastructures.* Miundombinu mbalimbali ya ki-*ICT* inakuwa *attacked,* zile *cyber-attacks,* kama tulivyoona katika nchi ya Lesotho, Benki Kuu yao mfumo ulikuwa *hacked* ukawa ni shida katika suala zima la kifedha. Vilevile tuliona katika nchi ya *USA,* mifumo ya hospitali ilikuwa *attacked*. Kwa hiyo, ni lazima kama Taifa tutafute namna ya kuhakikisha *systems* zetu zinakuwa *resilient enough against cyber-attacks. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima mambo haya yafanyike leo, tusisubiri mpaka tunakuja kuwa *attacked* ndiyo tunatafuta namna ya kutoka. Mifano hai tumeiona, Sri Lanka na yenyewe mifumo yake iliweza kuvamiwa na kusababisha *chaos* kubwa. Hebu *imagine* sasa hivi unaenda Muhimbili, wagonjwa wote wakiwa wamelazwa, halafu mfumo wa Hospitali ya Muhimbili uwe umekuwa *attacked,* maana yake itakuwa ni *chaos* kubwa na watu wengi wanaweza kuharibu maisha yao au maisha yao kuweza kupotea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ione namna ya kuhakikisha mambo haya wanayasimamia ipasavyo na utekelezaji wake unakuwa ni wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili, ahsante.

Mheshimiwa Innocent, halafu jiandae Mheshimiwa Chaurembo na Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na kibali cha kuingia katika mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuiongoza kamati, hatimaye kuweza kuleta taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutiririsha fedha nyingi kwenye taasisi ambazo tunaziongoza. Kuna mahali tumeona wakati tunapitia taarifa za kazi, tumefika mahali ndani ya kipindi hiki cha robo mwaka wamefika zaidi ya asilimia 70. Tuna haja ya kumpongeza katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nami nitumie nafasi hii ku-*declare* kwamba mimi ni mjumbe katika Kamati ya Miundombinu na nianze kuchangia kwenye suala la *TPA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ndiyo lango la uchumi katika nchi hii, na ni imani yangu kwamba Mwenyezi Mungu sisi kama Watanzania ametupa baraka kupitia Bahari ya Hindi kuweza kufanya Taifa letu liwe na uchumi mkubwa. Katika kufuatilia nikwambie, Bandari ya Dar es Salaam ni Bandari ambayo ina sifa zote. Ina bandari ya uwezo wa kushusha na kupakia mizigo. Kwa hiyo, kiuhalisia kwenye meli na kwenye mizigo wanaweza kuitumia bandari hii na tukaweza kupata mapato makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wenzangu wamesema nami niendelee kusema, Kamati imeomba kupitia *wharfage* walau *TPA* waachie asilimia 30, lakini mimi naenda mbali zaidi. Duniani kote

kwenye Bandari *wharfage* inabakia ndani ya bandari yenyewe kwa ajili ya maboresho ya miundombinu ya bandari ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulichukua fedha hiyo ikaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Ombi langu na niombe Bunge, niwashawishi Wabunge wenzangu, tusiende kwenye asilimia 30, fedha ya *wharfage* irudi kwenye maboresho ya bandari zetu. Kwa nini nasema hivyo? Kazi ya *TRA* ni kukusanya kodi. Tumezungumza na wenzetu wa *TPA,* wametuambia gati moja kwa mwaka inaweza kuleta kodi kwenye Serikali kiasi cha shilingi bilioni 600. Wenzetu wa *TPA* wanataka kutengeneza magati mawili mpaka matano. Tukiwaachia hii fedha ya *wharfage* ambayo ni shilingi bilioni 50 wanapata kwa mwezi, kwa mwaka wanatakuwa wanapata shilingi trilioni 1.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekwenda mbali kuwauliza gati moja linatumia shilingi ngapi kwa matengenezo yake, wametuambia gati moja linatumia bilioni 130, nini maana yake? Ukiweza kuwaachia fedha hii hata pengine kwa miaka miwili tu watakuwa na uwezo wa kutengeneza zaidi ya magati 10. Wakitengeneza idadi ya magati 10 kama alivyosema Ndugu yangu Manjira tukaenda mpaka kule Kigamboni, kwa mwaka tutakuwa na uwezo wa kukusanya kodi trilioni sita. Trilioni sita itakuwa ni mapato makubwa kwenye Serikali na ikiingia kwenye mzunguko wa fedha itafanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kupitia Bunge lako tusipepese maneno tuielekeze Serikali kwamba fedha hii irudi na ibakie *TPA* ili iweze kufanya mambo hayo na kukamilisha. Mimi namwanini sana Mheshimiwa Waziri Mbarawa na msaidizi wake lakini tunamwamini kabisa Mtendaji wa *TPA*, Mdogo wangu Mbossa, wanafanya kazi nzuri. Shida inayowachanganya ni kwamba hawajapata fedha na kuweza kufanikisha katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hili mimi naomba tuende sambamba na kwenye *TAA*. Kuna kitu kinaitwa *passenger service levy*; *passenger service levy*, kazi yake ni kuboresha viwanja wa ndege, Serikali imekusanya imechukuwa imeingiza kwenye Mfuko Mkuu. Wanapotaka kufanya maboresho yoyote kwenye wwanja wa ndege lazima wakaombe Serikali hii siyo jambo jema, siyo jambo la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali kupitia Bunge lako tuiambie waache fedha za *service levy* ambazo zinakatwa kupitia viwanja vyetu vya ndege ili tuendelee kuboresha viwanja vya ndege. Kupitia fedha hizo tungeweza kufanya maboresho makubwa kwenye viwanja vyetu vya ndege na kuweza kusaidia usafiri wa anga ukawa mzuri katika nchi yetu *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu ambalo ningependa kusema na mimi niende kwenye *TANROADS*; ninaimani kubwa na wajina wangu, Waziri Bashungwa Innocent lakini nina Imani kubwa na Watendaji wa *TANROADS*. *TANROADS* inaweza na inaweza kufanya mambo makubwa katika Nchi hii tatizo ni fedha. Sisi kama Kamati tumegundua na tumeona, tunahitaji *hardly* trilioni tano kwa mwaka kuweza kufanikisha mambo yetu yote yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini angalia bajeti ya mwaka jana, *TANROADS* imetengewa trilioni 1.3 na visenti kidogo ambavyo havitoshelezi. Juzi tulimwita Waziri wa Fedha, tulimwita Waziri wa Ujenzi katika Bunge tulilomaliza, wamejipangaje katika bajeti iliyokwisha? Wametupa matumaini. Lakini niombe kupitia Bunge hili, tuiambia Serikali tunakwenda kwenye uchaguzi mwakani lakini wakati tunakwenda kwenye uchaguzi mwakani Mvua za *El Nino* zimefanya uharibifu mkubwa katika Nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano barabara ya Bigwa–Kisaki imekatika zaidi ya mara saba kuna mapungufu, kuna shida kubwa katika usafiri wa wananchi. vilevile tunakwenda kwenye uchaguzi, kuna miradi ambayo tumeiahidi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama

cha Mapinduzi. Mama Samia Suluhu Hassan amefanya mambo katika nchi hii, tuangalie tusiende tukampunguzia kura zake za Urais. Sasa niombe kupitia Bunge hili tuiambie Serikali tunataka:-

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, miradi 13 ambayo tayari imeshapata wakandarasi inasubiri uwekezaji, mmojawapo ukiwa Barabara ya Bigwa – Kisaki kilometa 78; Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere kilometa 11 itengewe fedha twende zikasainiwe ili kusudi tuone hayo mafanikio makubwa ambayo Serikali imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi niipongeze Serikali na nimpongeze Mama Samia Suluhu Hassan kwa nafasi yake ambaye ameiona. Juzi tarehe 21 Mwezi wa Kumi na Mbili kulikuwepo na Mkutano Mkubwa wa Wakandarasi pamoja na Serikali ambayo alikuwepo Waziri wa Fedha, alikuwepo na Waziri wa Ujenzi. Mama anataka wakandarasi wazalendo wajengewe uwezo na wafanye miradi mikubwa ili fedha ibaki Nchini, napongeza jitihada hizo. Sasa ndani ya kikao kile Mawaziri walijulishwa na Wakandarasi kwa sababu bahati nzuri na mimi na *declare interest* ni Mkandarasi, kuna suala ambalo Serikali imetueleza kwamba inatengeneza kiliometa 50, 50 miradi kama minne wapewe Wakandarasi wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali; moja, tutengeneze *JV* ya wakandarasi wazawa kuanzia *class one* mpaka *class five* ili waweze kujenga miradi hiyo. Vilevile, hawa wakandarasi wakubwa wawajengee uwezo makandarasi wadogo. Niiombe Serikali kupitia miradi hiyo wawatafutie washauri wa miradi ili miradi hiyo ikamilike kwa muda na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kuna suala la *withholding tax* ndani ya miradi kuna asilimia tano inayochukuliwa *withholding tax* inawaumiza wafanyabiashara na hasa wakandarasi wazawa. Tunaomba, tulipendekeza kuna kati ya asilimia mbili ibakie, ichukuliwe asilimia tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja zote za Kamati na niliombe Bunge tusipepese macho kama…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chaurembo, jiandae Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Kamati hii ya Miundombinu. Niseme ni miongoni mwa wajumbe katika Kamati hii ya Miundombinu, Kamati ambayo kila Mbunge hapa amekuwa akiangalia namna ambavyo tunaweza tukatekeleza wajibu wetu kuhakikisha miradi hasa ya barabara inatekelezwa kwa wakati na namna ambavyo imepangwa kwa mujibu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mama yetu Daktari Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa kusikiliza kilio cha wananchi wangu wa Mbagala hususan wakazi wa Kisewe, Mbande mpaka Msongola kwa maana tulikuwa na kilio cha muda mrefu katika ile Barabara ya Mbande – Kisewe mpaka Msongola. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, mambo yanaenda vizuri na wananchi wanafurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kwa dhati yangu ya moyo niwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati tukiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kakoso, kwa mapendekezo ambayo tumeyaleta kwenye Bunge hili. Mapendekezo ambayo tukiyasoma kwa kina yanaenda kuwa mwarobaini wa mambo tofauti tofauti katika idara zote ambazo zinasimamiwa na Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa baada ya Kamati kutoa mapendekezo haya, niwaombe Wabunge wote baada ya kuyasoma na kuyajadili hapa basi yawe ndio maazimio ya Bunge letu hili ili tuweze kuleta tija katika sekta mbalimbali ambazo zinasimamiwa na Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisoma kwenye taarifa yetu, zipo changamoto ambazo zimeonekana katika Mamlaka ya Bandari na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia sana. Changamoto zile tukiziwekea maazimio katika Bunge hili naamini tunaenda kurekebisa mambo mengi pale bandarini na mapato ya nchi yetu yatazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezitaja changamoto karibu zote zile za bandari na *a way forward* nini tufanye katika kutoa hizo changamoto. Katika taarifa pia tumeonyesha changamoto zinazowakabili wenzetu wa *TANROADS*. Naomba nijikite hapo katika mchango wangu wa leo baada ya pongezi hizi ambazo nimezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa tumeainisha, moja ya changamoto ni ufinyu wa bajeti na wenzangu hapa wamechangia na mimi nachangia, endapo Wizara hii au *TANROADS* wakipata trilioni tano kwa kila mwaka tunaamini tunaenda kutatua matatizo makubwa ya changamoto ya barabara zinazotukabili katika maeneo yetu. Barabara nyingi zimeharibika, barabara nyingi zinahitaji matengenezo, kitu ambacho kutokana na fedha ambazo TANROAD wanazo *1.3 trillion* hatuwezi kutoboa, hatuwezi kufika popote katika suala zima la barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakutolea mfano wa baadhi ya barabara, kwa mfano ile barabara inayotoka Mbagala Rangi Tatu – Kongowe mpaka kwenda Mwandege, barabara ile ni lango kuu la wenzetu wanaotoka mikoa ya kusini. Lakini barabara ile imekuwa haitengenezwi mara kwa mara kutokana na ufinyu wa bajeti, na hata inapotengewa bajeti kutokana na tatizo kubwa lililokuwepo la miundombinu tunajikuta fedha zile zinaweza ku-*service* maeneo mengine na hatimaye kila mwaka barabara ile imekuwa haitengenezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali endapo tutaongeza fedha mpaka kufikia trilioni tano basi changamoto nyingi za barabara zinaenda kutatuka katika maeneo mbalimbali, nilikuwa na mwenzangu Mbunge wa Kiteto naye ananikumbusha barabara zake kwa kunisogezea vi-*memo*. Hii itaonyesha ni jinsi gani changamoto ya barabara ilivyokuwa ni kubwa na hii inatokana na ufinyu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Kamati tumezungumzia sana kuhusiana na madeni ya wakandarasi. Unaweza ukaona suala la madeni ni suala dogo lakini athari zake linaenda kuongeza riba kitu ambacho fedha hizo tunazozipata nyingine badala ya kufanya maendeleo ya ujenzi wa barabara tunaenda kulipa riba kutokana na kuchelewesha kuwalipa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana maazimio tutakayofikia hapa na niwaombe Wabunge wenzangu watuunge mkono Kamati yetu. Serikali waende kutekeleza, tutaenda kuokoa mambo makubwa sana katika sekta nzima ya Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumezungumza suala la fidia, katika changamoto ya fidia hapa naomba tuelewane kidogo, *TANROADS* hawawezi kujenga barabara ambayo kuna migogoro ya fidia au maeneo ambayo hayajalipwa fidia. Zipo barabara nyingi watu wamesimamishwa kuendeleza na bajeti zinapangwa kila mwaka lakini kwenye suala la ulipaji wa fidia kumekuwa na changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii niliyoisema hapa ya kutoka Kongowe – Kokoto mpaka kwenda Mwandege ni zaidi ya miaka 10 sasa wananchi wameambiwa wasiendeleze maeneo yao kwa ajili ya kusubiri fidia na barabara hii nayo inazalisha riba. Sasa ndugu zangu niwaombe sana Serikali maeneo haya kama tuna mpango kweli wa kuyaendeleza na kuyajenga basi tulipe fidia kwa wakati ili tuondokane na riba. Wananchi wale wa kutoka Kokoto

mpaka Mwandege wanaendelea kukata tamaa siku hadi siku nyumba zao hazipangishiki, wananchi wanahama waliopanga katika nyumba zao, wanazidi kuwa maskini kadiri ya siku zinavyokwenda kwa ajili ya zuio lililofanyika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka nimalizie kwa ndugu zangu wa *TANROADS,* wanafanya kazi nzuri sana lakini yapo maeneo wanazusha taharuki zisizokuwa na msingi. Kwa mfano barabara ya kutoka Msongola kuja Mbande – Kisewe – Majiatitu- Rangi Tatu wameweka *X* kwenye *corridor* zote za barabara bila kutoa maelezo yoyote, bahati nzuri ni mzawa wa Mbagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapafahamu pale Majimatitu, eneo lile mwanzoni katika miaka ya 80 Kampuni ya *ABUCO* ililipa fidia upana wa barabara na wananchi wa pale wanajua barabara zilizolipwa zimelipwa upana gani na bahati nzuri miongoni mwa watu waliolipwa fidia alikuwepo pamoja na marehemu mzee wangu. Nimetafuta karatasi nimeona tumelipwa fidia mita 15 kutoka katikati ya barabara. Leo *TANROADS* wamekwenda kuweka *X* zaidi ya mita 30, wananchi wamekumbwa na taharuki, niwaombe sana *TANROADS* wakaondoe mgogoro ule kwa kuwaambia uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Amina Ali Mzee, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka na ajiandae Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba.

**MHE. AMINA ALI MZEE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nami sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi *Allah Subhana Wa Ta'ala,* lakini nichukue nafasi hii kumpongeza

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika bajeti ya Wizara hii ilitutengea jumla ya bilioni moja katika sekta ya uchukuzi katika ununuzi wa mitambo ndani ya Chuo cha *DMI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mama yetu Kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan ndani ya chuo hichi mtambo huu wa *scanner* umefika ndani ya chuo na tayari wanafunzi wanaendelea kufaidika na mtambo huu kwa ajili ya kujisomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite katika mchango wa kamati, changamoto ya kamati yetu zinaonyesha suala la madeni ndani ya taasisi za Serikali. Taasisi nyingi za Serikali zinaonyesha bado zina madeni. *TBA* inadai madeni mengi katika taasisi za Serikali, kupitia Wakala wa Madeni tuliweza kukusanya jumla ya trilioni saba kwa ajili ya ulipaji wa madeni. Jumla tulikuwa tuna deni la bilioni 25. Tuipongeze *TBA* kwa kuhakikisha kuendelea kulipa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutoe wito kwa Serikali kwa kupitia taasisi zake, Wizara mbalimbali za Serikali zinadaiwa na *TBA*. Kama sera yetu ya mashirika inavyosema tuhakikishe mashirika yanaendelea kujitegemea kiuchumi na kujiendesha kibiashara na faida. Taasisi za Serikali zijitahidi kulipa madeni ili kuhakikisha Shirika letu la *TBA* linaendelea kunyanyuka na kuendeleza biashara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto pia iliyoelezwa suala la upungufu wa watumishi; ndani ya sekta yetu ya uchukuzi tuna takribani upungufu wa watumishi 18,000 lakini mpaka sasa Serikali imeendelea kuajiri watumishi 12,000, tuna upungufu wa watumishi 6,000. Serikali yetu tukufu inayoongozwa na Mama yetu mpendwa, tunaiomba Serikali yetu upungufu wa watumishi 6,000 kuhakikisha kuziba *gap* ili watumishi wengi wazidi kupata nafasi. Sekta ya uchukuzi tunafahamu, tuna vyuo, tuna bandari, sekta tofauti tofauti lakini upungufu huu unasababisha kuzorotesha kazi zetu ndani ya

sekta yetu ya uchukuzi. Tunaiomba sana Serikali iweze kupunguza upungufu huo wa watumishi ili tupate watumishi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka, jiandae Mheshimiwa Santiel Kirumba, jiandae Mheshimiwa Chomete. Washa *mic*, Mzee vipi korosho hazijatoka bado? *(Kicheko)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Ziko tayari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi lakini vilevile nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mchana huu na kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoamua kuutembelea Mkoa wa Lindi alikuja Liwale pamoja na kwamba Liwale hakufikiki kwa barabara Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Wananchi wa Liwale aliamua kuja kwa chopa wana Liwale tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na hoja zote kwa maana ya Maazimio yote ya Kamati na niwapongeze Wanakamati na Mwenyekiti wao na maazimio yote nayaunga mkono lakini hapa na mimi naomba niongeze azimio moja. Kama ikikuridhia tuitake Serikali ipeleke fedha zote tulizozipitisha kwenye bajeti ya mwaka huu, hii tunayoitekeleza hasa kwa upande wa barabara kabla ya bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nijikite sana kwenye upande wa *TANROADS* na hapa ninapozungumza Wilaya ya Liwale iko kisiwani, hapa ninapozungumza Wilaya ya Nachingwea iko kisiwani. Wilaya

ya Nachingwea inafikiwa na barabara tatu; Masasi – Nachingwea, Ndanda – Nachingwea na Nanganga – Nachingwea. Hizo barabara zote tatu zimeharibika hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale inafikiwa na barabara mbili; Barabara ya Nachingwea – Liwale na Nangurunguru – Liwale, barabara hizo zote hazipitiki. Leo hii tunapozungumza Liwale hakuna mafuta kwa sababu malori yote ya mafuta yamekwama hayaendeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninapoongeza azimio la kuitaka Serikali ipeleke fedha zote zilizopitishwa na bajeti iliyopita kwa sababu kwenye Wilaya yetu ya Liwale barabara yetu ya Nangurunguru – Liwale tulikuwa tumetengewa kilometa 72. Kwa hiyo utekelezaji wa bajeti hii itatupa afueni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Juni, mwaka uliopita mimi ni miongoni mwa watu walioshiriki kwenda kushuhudia Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Masasi – Liwale kilometa 75 kwenye Mradi wa *EPC+F*. Leo maswali ni mengi kwa Wanaliwale; miradi hii inakwenda kutekelezwa lini? Kwa hiyo tunaiomba sana Serikali kuhakikisha bajeti iliyopitishwa hapa mwaka huu inatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema hivyo kwa kusisitiza zaidi nataka niwaambie Liwale hakufikiki. Hivi juzi kulikuwa na ratiba ya Mwenezi wetu Taifa, Ndugu Makonda, ilikuwa aje Liwale, lakini ratiba ile imefutwa anaishia Nachingwea kwa sababu Liwale hakufikiki kwa hiyo nataka muone namna Liwale ilivyo kisiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niendelee kuunga mkono Kamati, tunazungumzia Bandari ya Mtwara. Ni kweli mwaka huu Bandari ya Mtwara imefanya vizuri, korosho zote za Mkoa wa Lindi na Mtwara tumezisafirishia Bandari ya Mtwara lakini kizungumkuti kinakuja inapozungumzwa Barabara ya Reli kutoka *Mbamba Bay* kwenda Mtwara. Mara zote majibu ya Serikali wanasema

wanatafuta mbia. Mimi bado kichwani mwangu kuna maswali mengi ambayo hayana majibu. Kwa nini reli hii inatafutiwa mbia wakati kuna reli nyingine inayotoka Dar es Salaam mpaka Kigoma mpaka Burundi inajengwa na fedha zetu? Kwa nini miradi hii isiingizwe huko? Kwani Mtwara na Lindi kuna nini? Ni majibu ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti akija kuhitimisha hoja tutaomba Mwenyekiti naye utusaidie. Kwambakatika jambo hili shida ya Lindi na Mtwara ni nini? Kwa sababu kila mwaka tukiuliza tunaambiwa hii reli itajengwa tunatafuta mbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayo taarifa, na kwenye bajeti nilisema, kuna mbia mmoja alijitokeza lakini yule mbia mpaka leo ameandika barua Wizarani hajajibiwa; kwa hiyo kuna shida. Tunataka tujue reli hii itajengwa lini, sambamba na uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Mtwara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kanda ya Kusini tunautegemea sana Uwanja ule wa Mtwara kwa sababu ndio uwanja pekee unaokaribiana na maeneo ya kwetu. Hayo ndiyo mambo ya msingi nilikuwa niyazungumze kwenye hotuba hii ya Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi sana ambayo yanazungumzwa kwenye Kamati hii. Kwa mfano kama *TANROADS* wamesema wana tatizo la bajeti lakini tatizo siyo bajeti peke yake; hata hiyo bajeti kidogo je, inakwenda?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri sana kwenye hotuba ya Kamati tungeomba sana Mwenyekiti wa Kamati atuelezee, mpaka sasa hivi *TANROADS* wameshapokea fedha kiasi gani *versus* na bajeti tuliyowapitishia. Hii itatusaidia kuona ni namna gani utekelezaji wa bajeti kwenye Serikali yetu unavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninazungumzia kwenye upande wa mawasiliano. Upande wa mawasiliano natoa mfano

upande wa Liwale tulikuwa na minara iliyojengwa na *Halotel.* Ile minara imejengewa sasa hivi ina miaka mitatu yote haifanyi kazi kwa sababu inatumia *battery,* na *battery* zimekufa. Kwa hiyo mawasiliano sasa hivi unapata kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa 12 jioni, au pengine mpaka saa 10 jioni mawasiliano hakuna. Kwa hiyo tunaiomba sana Serikali kwenda kuboresha minara ile ili iweze kufikika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine ni *TBC*. Hii redio ya Taifa au hii *TV* ya Taifa; kwa upande wa *TV* hatuna wasiwasi lakini kwa upande wa redio Liwale tunapata Redio Ulanga, Redio Msumbiji lakini *TBC* hampo kabisa. Kwa hiyo mimi naiomba sana Serikali kuhakikisha sisi watu wa Liwale tunapata mawasiliano ya *TBC,* kwa sababu ndiyo *TBC* ya kwetu na sisi ndio walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, najua Mheshimiwa Mwenyekiti ndiye atakayekuja kuhitimisha hii; kwa hiyo nimuombe anisaidie kunipatia majibu ya haya na hili Azimio langu ninaloliongeza hapa akiridhia liingizwe; kwamba tuiombe Serikali, pamoja na bajeti ndogo wanayopata *TANROADS* basi miradi yote tuliyoipitisha hapa tuone inatengewa fedha kabla ya bajeti ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante mimi naunga mkono hoja zote za Kamati; ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Santiel, ajiandae Mheshimiwa Chomete, ajiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amekuwa kila mwaka akituidhinishia bajeti katika sekta hii ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais tangu ameingia madarakani kwa kipindi hiki kifupi ameweza kulipa hata madeni

ambayo yaliachwa 2015 mpaka sasa hivi. Licha ya kwamba madeni haya yamekuwa yakilipika lakini bado sekta hii ya miundombinu imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa sana ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hapa Bungeni imekuwa ikija tunawapitishia bajeti ya miundombinu, lakini cha kushangaza fedha zile zimekuwa hazifiki kwa wakati katika Wizara hii ya Miundombinu, na fedha zile zimekuwa pia zinacheleweshwa na kufikia hatua kwamba wakandarasi wengi wameshindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunajua kwamba ina mikakati mingi, lakini Serikali pia inabidi iangalie kwa wakati huu nini cha muhimu cha kufanya? Tunaelewa barabara ni siasa, na barabara hizi kama ni siasa kwenye kila mwaka tunapopitisha bajeti ni lazima tuangalie kipaumbele chetu ni kipi, lipi litakuwa ni la kimkakati kuliko hivi sasa hivi Serikali inachokifanya. Tunaidhinisha bajeti ya shilingi trilioni moja, haifiki; Waheshimiwa Wabunge wengi wanakuja hapa wanalalamika kuhusu Barabara, kwamba hatujafikiwa. Hii inakuwa inaleta sintofahamu katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifike mahali kama imeamua kutekeleza miradi ya barabara ilete fedha kwa wakati na iweze kutekeleza barabara hizi kwa kipindi cha bajeti ili iweze kutoa hizi sintofahamu. Kwa mfano, kwa mwaka jana mpaka Disemba miradi iliyokamilika ni 94 na miradi ambayo bado inaendelea ni miradi 69 na bado Serikali inadaiwa bilioni 796 mpaka kufikia Disemba. Kumbuka fedha hizi zinachajiwa na riba na hii kuifanya Serikali kuingia kwenye riba na kupoteza fedha nyingi zinazoenda kwenye riba. Kwa hiyo kama Serikali mimi ningeiomba ili tujisaidie tusiingie kwenye hizi changamoto tupitishe vile ambavyo tunaviweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo lingine katika *Road Fund*. Serikali inaidhinisha pia barabara mpya huku kuna barabara 71 zimebaki zikiendelea kuwa mbovu, ambazo ni barabara kongwe.

Sasa hivi nitamwona Waziri Bashungwa anahangaika mara utamwona Shinyanga, mara Dar es Salaam barabara zimekatika, na kuna tishio kubwa la mvua za *El-Nino* linaendelea na barabara madaraja yamekatika, zinahitajika fedha, lakini ukija kuangalia *Road Fund* yenyewe haina fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili *Road Fund* ijiendeshe inahitaji shilingi trilioni mbili na mpaka tunavyoongea hivi *Road Fund* yenyewe haina hiyo bajeti ya kuweza kutengeneza hizi barabara zilizokatika. *Road Fund* pia wana changamoto ile ile kama iliyoko *TANROADS,* fedha kutokufika kwa wakati. Tumeshaongea mara nyingi sana na Waziri wa Fedha, tumekuwa tukimwita aweze kuidhinisha fedha hizi kwa wakati. Siwezi kuelewa changamoto wanazozipitia Serikali labda kwamba hela hakuna kwenye kapu la Taifa, lakini lazima tuangalie. kwasababu barabara hizi zinapokatika, miundombinu hii inapokatika wananchi watashindwa kutoka kwenda kazini na pia Serikali itashindwa kupata mapato, kwa sababu barabara nayo ni mapato. Tutashindwa kusafirisha mazao, tutashindwa kufanya shughuli nyingine za kuingiza kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi pia nashauri, na hata Kamati pia imeshauri; *Road Fund* itengewe chanzo kingine cha mapato. Kwa mwaka *Road Fund* inahitaji shilingi trilioni mbili, na mpaka tunavyoongea sasa hivi kiasi kilichoidhinishwa ni bilioni 300. Kutoka kwenye trilioni mbili tunachokihitaji mpaka sasa hivi imeidhinishwa shilingi bilioni 300. Kwa jinsi gani utaona barabara nyingi zitabaki na mashimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara mpya, barabara zile za zamani zinaendelea kuwa chakavu. Kwa mfano ukiangalia hii Barabara ya Dodoma – Morogoro ina mashimo mengi nayo inahitaji hela; na hii barabara ni kubwa, lakini ukija kuiangalia hata sasa hivi bado tuna suasua kuitengea bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nipende kuishauri Serikali tunapoamua kuingiza barabara mpya kujenga barabara mpya; *TANROADS* kwa mwaka inahitaji shilingi trilioni tano. Hebu tuangalie tunaweza tukaipata shilingi trilioni tano au tupunguze barabara mpya tu-*deal* na hizi barabara za zamani 71 ili tuweze kuendelea kuunganisha hii mitandao na maisha ya wananchi yakaendelea kwa kawaida kuliko kuendelea kuingiza barabara mpya kwenye mtandao wa *TANROADS* ambazo hatutaweza kuzihudumia na hii ikawa ni changamoto katika Serikali yetu? Kwa sababu mwisho wa siku tutamaliza kutengeneza barabara mpya tutajikuta tunarudi kutengeneza hizi barabara za zamani ambapo na Serikali itakuwa imeingia hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo lingine ningependa kuishauri Serikali. Mnazuia maeneo ya wananchi, mnawataka wananchi wapishe yale maeneo kwa ajili ya kulipwa fidia lakini hapa imeshaonekana Serikali haina uwezo wa kulipa fidia kwa wakati. Kingine kwa mwaka jana wa fedha Serikali ilitakiwa kulipa shilingi trilioni saba fidia lakini *TANROADS* kama *TANROADS* wametengewa shilingi trilioni moja; utaona kwa namna moja tunapitisha mambo utelekezaji ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba kama yale maeneo Serikali inajua kabisa wameyapiga *X* ili wananchi wasiyatumie, na wameyazuia, waache wananchi kwa kipindi hichi waendelee kuyatumia maeneo yale kuliko kuendelea kuyazuia, hawawalipi fidia, wananchi wamewaondoa na haijulikani. Licha ya hivyo Serikali ikiwa inakuja kulipa fidia inailipa fidia ambayo haiendani na gharama ambazo zipo kwa wakati huo, na hii huwaletea wananchi changamoto sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nina imani na Serikali yangu na nina imani na jinsi ambavyo Mawaziri wanavyojituma katika kufanya kazi lakini tunapoelekea mwaka huu mwingine wa fedha kwa kweli tufanye pale ambapo tunahisi tunaweza; na tusiwe

na ahadi nyingi ambazo hazitekelezeki ambazo mwisho wa siku huko kwenye majimbo yetu ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hata mimi kwangu kuna Barabara ya Bulyankulu. Kila siku tunapewa ahadi tunaenda kusaini, tunaenda kusaini lakini mwaka wa fedha huu unaisha na wananchi wanaimani sana na Mheshimiwa Rais, wanaimani sana na Serikali na wanaimani na Chama Cha Mapinduzi; lakini wanavyoona ukimya kila siku kwamba wanakaa ahadi inatolewa hazitekelezeki imani ile inazidi kupotea, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante; Mheshimiwa Chomete ajiandae Mheshimiwa Kakoso, ajiandae Mheshimiwa Kabati.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika sekta hii ya miundombinu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na nimesimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu katika kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Kipekee pia niwapongeze sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wewe kwa jinsi mnavyoendesha Bunge letu Tukufu na kuhakikisha Bunge letu linaendelea kuimarika na kuendelea kuwa kidedea; hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende kuchangia kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Nimpongeze sana Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa na Naibu wake Mheshimiwa David Kihenzile na wafanyakazi wa Shirika hilo la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inamiliki au inahudumu viwanja vya ndege takribani 53. Katika viwanja hivyo 53 vipo viwanja vitano au havifiki vitano ambavyo ndivyo vinavyosimamia au vinavyohudumu vinavyovisaidia vile viwanja vingine ambavyo vinapelekea vile viwanja vya ndege au Mamlaka uchumi wake au jinsi ya uendeshaji unaendela kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema changamoto nyingi zilizopo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mimi nimeona pia nigusie changamoto moja. Tunatambua kwamba Serikali imeipa Mamlaka hiyo ya Viwanja vya Ndege kukusanya lakini pia na kupeleka gawio Serikalini. Makusanyo yale ya asilimia 70 ambayo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inakusanya, wao kama Mamlaka baada ya kukusanya na kupeleka Serikalini, wao wanarudishiwa asilimia 15. Hii asilimia 15 wanayorudishiwa ni ndogo sana; na baadaye pia wanaweza wasirudishiwe hiyo asilimia 15. Hii inapelekea utendaji wao wa kazi kushuka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ombi langu kwa Serikali, ninaomba Serikali iliangalie hili Mamlaka iweze kuongezewa kutoka asilimia 15 basi ifike hata asilimia 40 ili kusudi Mamlaka iweze kujiendesha vizuri. Sambamba na hilo basi nashauri asilimia hiyo iliyopangwa na Serikali irudi kwenye Mamlaka kwa wakati ili Mamlaka iweze kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Mheshimiwa Rais amelifungua anga, amewekeza fedha nyingi kwenye anga. Tunapoacha kuboresha viwanja vyetu sisi wenyewe kama Watanzania tunajishushia uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo naomba nichangie upande wa *TANROADS;* kwanza naomba nimpongeze sana Waziri pia mwenye dhamana Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya; hawa Wamekuwa ni viongozi wazuri wanaomsaidia sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule kwetu, nitolee mfano kule Mkoa wa Mara; tumepata miradi mingi ya barabara za lami; nampongeza sana sana Meneja wetu wa *TANROADS* Mkoa wa Mara, amekuwa ni Meneja mzuri anayesimamia miradi ya *TANROADS* vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua miradi ya barabara iliyoletwa; ulikuwepo Mradi wa Nata mpaka Sanzati kilometa 40; ule mradi ni wa muda mrefu, lakini Mheshimiwa Rais ametuletea fedha na ule mradi unaendelea mpaka sasa; tunamshukuru sana. Changamoto iliyopo pale ni ucheleweshaji wa fedha kwa mkandarasi. Naiomba Serikali ihakikishe inapeleka fedha zile kwa mkandarasi ili kusudi ule mradi uweze kumalizika kwa sababu ni wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepata mradi mwingine wa barabara mradi unaounganisha wilaya kwa wilaya lakini mpaka mkoa kwa mkoa; Mradi wa Tarime – Nyamongo mpaka Mugumu Serengeti kilometa 87. Mradi ule unaendelea mpaka sasa na fedha zimekwenda. Isipokuwa, mradi ulitakiwa kumalizika mwaka jana lakini mpaka sasa mradi haujamalizika. Changamoto iliyopo ni kusuasua kulipwa mkandarasi. Naiomba Serikali yangu iliangalie hili. Tunapochelewa kumlipa mkandarasi tunaenda kuongeza madeni zaidi na kuisababishia Serikali hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaelewa changamoto za wananchi wa Mkoa wa Mara, ameendelea kutupa Barabara. Tunatambua kwamba katika Bajeti ya 2023/2024 ametupa barabara ya Musoma - Busekera kilomita 92 lakini mpaka sasa ule mradi au ile barabara hakuna kinachoendelea mkandarasi hayupo. Kwa hiyo, naiomba *TANROADS* kupitia Serikali yangu iangalie ni namna gani mradi ule utaenda kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hajaishia hapo ametupa mradi wa Mika, Utegi mpaka Kirongwe kilomita 56, mpaka sasa wananchi wa Wilaya ya Rorya au Jimbo la Rorya wanatamani mradi ule uende kuanza ni kwa namna gani unaanza, wakitambua kwamba mradi ule umewekwa katika bajeti ya 2023/2024. Wananchi wanatamani kula matunda ya Serikali ya Awamu ya Sita, ninaiomba sana Serikali yangu iangalie ni kwa namna gani inaweza ikakamilisha au ikaanza pia na miradi hii ili kusudi sisi sote tuende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala zima la upande wa Shirika la Ndege. Tunatambua kwamba shirika la ndege Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amewekeza vizuri katika shirika hili la ndege na ameendelea kununua ndege nyingi katika nchi yetu, tulipokuwa siko tunakoenda, hii imeonesha ni jinsi gani Mama anaendelea kuchapa kazi. Kuna Mikoa ambayo inatamani kuiona ndege *Air Tanzania,* ndege yetu ya Serikali lakini mpaka sasa Mikoa hiyo ndege haijawahi kufika na wananchi wanasikia kila wakati kwamba Mama amenunua ndege. Wazo langu au ushauri wangu ni nini? Kamati ilitembelea Mkoa wa Mtwara ilikuta Serikali imewekeza pesa nyingi sana pale kwenye uwanja ule lakini ndege ya *Air* Tanzania haifiki pale, tatizo ni nini? Naiomba Serikali yangu iangalie kwa jicho la pili Mikoa ambayo *Air* Tanzania inaweza kufika ili kusudi wananchi wote tufaidike na hii keki ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso kaondolewa kwenye orodha. Sasa anaingia Mheshimiwa Kabati jiandae Mheshimiwa Mkundi na Mheshimiwa Stella ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu pia nawapongeza sana Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu kwa taarifa yao na ripoti yao nzuri ambayo wameiwasilisha hapa sasa hivi na sisi tunaweza kuiongozea nyama kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Mawaziri wote waliopo katika sekta hii ya miundombinu na Manaibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara zote ambazo zinaguswa na hii Kamati ya Miundombinu. Vilevile, naomba pia nimpongeze Spika na nikupongeze Naibu Spika kwa kazi nzuri inayofanyika katika Bunge letu hili la Muungano. Naendelea pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana ambayo amekuwa akiifanya pamoja na kuhakikisha kwamba pesa nyingi sana zinakwenda katika sekta hii ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sekta ya barabara na nianze kuchangia kuhusiana na barabara za kiuchumi zilizopo katika nchi yetu. Naiomba Serikali iangalie na iweke kipaumbele kikubwa kuhakikisha kwamba bajeti kubwa inawekwa kuhakikisha kwamba barabara za kiuchumi zinapitika wakati wote na hasa wakati huu wa mvua hizi za masika. Tunaona barabara nyingi sana wakati wa masika hazipiti na ni za kiuchumi na zinasababisha sasa uchumi kudorora au kupunguza uchumi katika nchi yetu. Kwa hiyo, naomba uwepo mkakati wa kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika wakati wote, na kwa sababu kuna baadhi ya barabara nyingine unakuta kwamba kuna eneo tu dogo ambalo linasababisha barabara ile isipitike. Kwa hiyo, hiyo barabara kama itatengenezwa vizuri basi unaona kwamba zinaweza zikapitika wakati wote na malori yanaweza yakapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa baadhi ya barabara ambazo hata katika Mkoa wetu wa Iringa zimekuwa za kiuchumi lakini hazipitiki. Kule Mafinga unakuta kuna Barabara ya

Kinyanambo 'C' - Mapanda - Mlimba hii inakwenda mpaka Morogoro ni muhimu sana ikawa inapitika wakati wote. Pia kuna barabara ya Nyololo – Mtwango hii ni ya kilomita 40, unaona kwamba hii barabara ni muhimu sana katika uchumi wa nchi hii. Tunayo pia barabara kwa mfano ya Ilula – Wotalisoli – Mlafu - Mkalanga na Kising'a hii inakwenda mpaka kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo lakini unakuta watu badala ya kupita hii, maana yake kuna Kilolo ya Chini na Juu badala ya kukatiza kupita mpaka kule Wilayani wanalazimisha sasa kupita mpaka Iringa Mjini ili waende Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni muhimu barabara kama hizi zikaangaliwa zina umuhimu wake ili kupunguza hata wananchi kuweza kufanya shughuli zao kwa wakati. vilevile, kuna hii barabara yetu ya Mlima Kitonga, hii barabara ni ya kiuchumi tena wa Kimataifa. Unakuta magari yanakwama hata siku mbili au siku tatu, barabara haipitiki kabisa lakini tunashukuru sasa hivi Serikali imeanza kweli tunashukuru Waziri alikuja katika ile barabara na tunaona sasa matengenezo yameanza ya upanuzi wa ile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba iwepo barabara mbadala kwa sababu bado matengenezo yake hayatachukua leo au kesho yatachukua muda mrefu sana, sasa tunaomba wakati hii barabara inafanyiwa matengenezo basi inapanuliwa basi ile barabara mbadala ya kutoka Mahenge kupitia Udekwa kutokea Ilula, hii barabara ingepewa kipaumbele ili kusiwepo na mkwamo wa magari kwa sababu hata wakati huu wa matengenezo magari yanakuwa hayapoiti kwa wakati, kwa hiyo hii ni muhimu sana Serikali ikaangalia barabara hizo za kiuchumi ziweze kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niendelee pia kuzungumzia kuhusiana na viwanja vya ndege. Mjumbe aliyepita amechangia vizuri sana kwamba tuna viwanja vingi sana vya ndege na vimekuwa vikipewa pesa kidokidogo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vinajengwa. Vingeangaliwa pengine hata vingefanyiwa

hata upembuzi yakinifu kweli ili vile viwanja vingine ambavyo karibu vinamalizikia, kwa mfano kwenye Mkoa wetu wa Iringa tuna Kiwanja cha Ndege cha Iringa, hiki kiwanja kimechukua muda mrefu sana kukamilika ilikuwa kikamilike tangu mwaka juzi na mwaka jana tunaongezewa tu muda, hiki kiwanja sasa hivi kwa uchumi wa Iringa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kilimo cha parachichi, tuna kilimo cha maua na tuna kilimo ambacho tunajua kwamba kama kiwanja hiki kingekamilika kingeweza kusaidia uchumi mkubwa sana wa Nyanda za Juu Kusini pamoja na kusafirisha mazao yake. Pia, zingetoa ajira nyingi sana kwa wananchi wa Iringana Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kwa kweli hiki kiwanja kimalizike sasa mana yake kila siku tunauliza mpaka tumechoka na naungana na mwenzangu kwamba ilikuwepo ndege ya *ATCL* inatua pale. Sasa tatizo lake ni nini kwa sababu barabara zile zimeshakuwa ziko tayari na tunaona viwanja vingine wakati vinaendelea kujengwa kuna ndege zinatua za *ATCL* ili kupunguza ile adha, tuna wagonjwa tuna nini kiasi kwamba ingeweza kusaidia. Kwa hiyo tunaomba basi wakati matengenezo kama yanachukua muda mrefu basi barabara zikikamilika basi ndege zile za *ATCL* zitue ili wananchi waweze kuwa na uhakika wa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, zamani zile kale wanasema hapo zamani za kale tulikuwa tunaweza kusafiri kwenda kuangalia miradi ya nchi nyingine nilikuwa Kamati ya Miundombinu tuliweza kusafiri kwenda Malaysia kuna mambo ambayo tulijifunza pengine Serikali pia ingeangalia. Kwanza kabisa tuliona wale wenzetu hii miradi mikubwa ya barabara kunakuwepo ile miradi ya *PPP (Private Sector Partnership)* ndiyo inayochukua. Inasaidia kwamba pesa za ndani zinatumika kwenye barabara ambazo zinazunguka katika nchi. Pengine hata Serikali sasa hivi ingeangalia iwepo hii miradi ya *private sector* kusaidia hii miradi mikubwa ya barabara. Pia, tuliona wenzetu wakandarasi wakubwa wanapokuja

kwenye nchi yao hawaruhusiwi kufanya ile miradi mikubwa mpaka waingie ubia na wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ingesaidia pia kuwajengea uwezo wakandarasi wetu wa ndani na vilevile hata wakiondoka vifaa vingi vinabaki kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, pia hili lingeangaliwa kwamba iwekwe sheria itakayosababisha hawa wakandarasi wanaotoka nje basi waingie ubia na wakandarasi wetu wa ndani ili kuwajengea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba wakandarasi wetu walipwe basi kwa wakati, kwa sababu tumeona wakandarasi wengi miradi inachelewa kuisha kwa sababu na gharama inakuwa kubwa kama ripoti ilivyosema kwa sababu hawalipwi kwa wakati na hiyo inasababisha kabisa wanashindwa kufanya kazi yao kwa wakati na gharama zinaongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Baada ya hapo nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu pia, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, jiandae Mheshimiwa Stella jiandae Naibu Waziri Kundo.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwa mara nyingine namshukru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kunipa fursa ya kutoa mchango wangu kwenye Taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Kwanza namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya kwenye sekta hizi za mawasiliano kwa sababu Taifa bila mawasiliano uchumi hautakuwa imara na mambo mengi na maendeleo ya wananchi yatakuwa duni, kwa hiyo, nampongeza sana kwa uwekezaji mkubwa anaoufanya kwenye sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati pia kwa taarifa nzuri na nami mapema kabisa nisema nakubaliana na taarifa yao na naunga mkono taarifa yao. Nitakuwa na mchango kwenye

maeneo kama mawili muda ukiruhusu maeneo matatu. Kwanza, ni eneo la sekta ya mawasiliano. Miezi kadhaa iliyopita tulishuhudia uzinduzi wa mradi mradi wa mawasiliano kupitia sekta hii ya mawasiliano na hasa taasisi hii ya *UCSAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa imefanyika naipongeza Serikali na naipongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Utakuwa ni shahidi mara kwa mara tunapokuwa Bungeni hapa kunakuwa bado na maswali mengi juu ya mawasiliano hasa kwenye eneo la minara, kwa mujibu wa Kamati yetu ya Miundombinu kasi ya utekelezaji wa miradi ya mawasiliano hasa kwenye ujenzi wa minara bado hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara tuangalie kama kuna changamoto yoyote, kama kuna shida ya uhaba wa fedha kwenye utekelezaji wa miradi yetu kupitia *UCSAF,* tuone nini tunaweza kufanya ili kuharakisha utekelezaji wa miradi hii ya mawasiliano ili wananchi wetu waweze kupata mawasiliano kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitolea mfano kwenye eneo langu la Ukerewe bado changamoto ni kubwa sana kwenye maeneo kama ya Bukiko na maeneo mengine kiasi kwamba bado wananchi wanahitaji kwenda kwenye maeneo yenye miinuko ili waweze kupata mawasiliano. Kwa hiyo, naiomba Wizara inayohusika na sekta hii ifanye kazi kubwa ili miradi hii ambayo inatakiwa kutekelezwa itekelezwe kwa haraka na wananchi waweze kupata mawasiliano katika mazingira yaliyo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo natamani kuchangia ni eneo la usafirishaji. Kupitia taarifa ya Kamati imeonesha kwamba bado kunahitajika pesa ili kuweza kusaidia kampuni ya usafirishaji wa meli *MSCL* iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Ni kweli kwamba Tanzania tuko kwenye eneo ambalo ni la kimkakati, tuna ukaribu na mahusiano na nchi za Jirani, nchi kama *DRC,* Uganda kuna Visiwa vya Ushelisheli, Visiwa vya Comoro na

mataifa mengine ya jirani na yote ni maeneo ya kimkakati kibiashara. Maeneo haya ili yaweze kufikika ni muhimu sana tukaimarisha kampuni yetu ya *MSCL* ili iweze kuwa na meli za kusafirisha mizigo na abiria kwenda kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna fursa kwenye nchi hizi za jirani ni fursa za kiuchumi kwa wananchi wetu, ni lazima tuwekeze kwenye kampuni hii ya *MSCL* iweze kufanya ukarabati na iweze kutengeneza meli ili meli hizi ziweze kufikia maeneo haya ya masoko na kufanya wananchi wetu waweze kuwa imara kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwa safari za nje tu hata kwa ndani bado tuna changamoto. Kwa mfano, kwenye Ziwa Viktoria tuna meli ambazo bado ziko kwenye matengenezo na wananchi wetu wanapata wakati mgumu sana kwenye huduma za kila siku kuweza kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Nitumie nafasi hii kwa sababu sisi kwa mfano kwenye eneo langu ninalotoka, Eneo la Ukerewe tunategemea usafiri wa meli. Sasa kunapokuwa na upungufu wa uwekezaji kwenye utengenezaji wa meli inakuwa ni changamoto kubwa ya usafiri kwa watu wanaotoka visiwani kama Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ikiwezekana inisaidie kutoa ufafanuzi. Siku za karibuni kumekuwa na utaratibu wa usafiri kwa mfano kutoka Ukerewe kwenda Mwanza. Meli zipo, napongeza kuna uwekezaji wa watu binafsi lakini wanapeana zamu kiasi kwamba badala ya meli kusafiri zote kwa wakati mmoja inasafiri meli moja au meli mbili wanapeana zamu jambo linalopelekea kunakuwa na mrundikano mkubwa sana wa wasafiri kwenye vyombo hivi vya usafirishaji, jambo ambalo ni *risk* kwa wananchi hawa, inaweza kutokea ajali halafu likawa jambo jingine kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali inaruhusu jambo hili badala ya kuruhusu vyombo vyote vikafanya kazi, vikasafirisha wasafiri katika mazingira mazuri lakini inapokwa wanaruhusu wanapeana zamu inakuwa ni *risk* kwa wasafiri wanaosafiri kupitia

vyombo hivi. Naiomba Serikali iwekeze itoe pesa iwasaidie *MSCL*. Bahati nzuri sana *MSCL* ina uongozi mzuri na imara ambao kama watapewa mtaji wanaweza kufanya mambo makubwa na kufanya shirika hili kuwa na nguvu kuweza kuvutia uwekezaji kwenye nchi zilizo jirani na kuimarisha uchumi wa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu na la mwisho ni eneo la *TANROADS,* wamesema wachangiaji wengi na Kamati imeeleza. Bajeti ya kuwezesha *TANROADS* kuweza kuimarisha barabara zetu ni karibu shilingi trilioni tano. Mwaka jana tumepitisha bajeti ya shilingi trilioni moja nukta kadhaa lakini siyo jambo la siri barabara zetu hivi sasa, hasa kutokana na mvua nyingi zilizonyesha barabara zetu zina matatizo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya *TANROADS* kujengewa uwezo ili waweze kuimarisha barabara zetu hasa zinazotuunganisha kutoka kwenye maeneo ya Mikoa na maeneo mengine yaliyo imara kiuchumi ili kusaidia kuimarisha uchumi wa watu wetu. Pamoja na kuongeza pesa hizi vilevile wale Wakandarasi wanaopewa miradi hii nashukuru Mheshimiwa Kalogeris amesema hapa kwamba ni dhamira ya Mheshimiwa Rais kuimarisha wakandarasi wetu wa ndani lakini bado nimekuwa nina mashaka sana na baadhi ya wakandarasi wetu. Mara kwa mara nimekuwa nasafiri kwa barabara kwenda Mwanza, kuna barabara ya kutoka Shinyanga Eneo la Hungumalwa kama sikosei kuja mpaka Mwanza, eneo lile linatengenezwa karibu kila mwaka lakini kila linapotengenezwa muda mfupi kunakuwa na matatizo kwenye barabara ile, sasa sijui tatizo ni wakandarasi au mazingira ya eneo lile lakini hoja yangu hapa naiomba Wizara iweze kuwasimamia wakandarasi wetu ili wanapopewa miradi hii thamani ya pesa vilevile iweze kuonekana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais lakini na Wizara, Mheshimiwa Bashungwa najua unafanya kazi kubwa sana, barabara yetu ya kutoka Nansio kuja Kisorya ilitengewa pesa mkandarasi amekwishapatikana lakini haijaanzwa kujengwa kwa

sababu ya changamoto za Wizara ya Fedha kupitia *TRA,* naomba sana utusaidie kuamua eneo hili ili barabara hii muhimu sana ianze kutengenewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Hospitali ya Saifee Tanzania wapo katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutoa ushauri na huduma za vipimo kwa maabara kuhusu afya ya moyo. Aidha, wapo madaktari wabobezi ambao pia watatoa ushauri kuhusu afya ya moyo na kutakuwa na upimaji wa vipimo vifuatavyo: *ECG, ECHO,* figo*, uric acid, cholesterol* na sukari. Pamoja na vipimo hivyo, watatoa ushauri kuhusu lishe. Zoezi hili linaanza leo tarehe 5 mpaka 9 Februari, 2024.

Aidha, huduma hii inapatikana nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge wote mnakaribishwa kutumia fursa hii.

Mheshimiwa Nyongo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kutakuwa na maonesho ya bidhaa mbalimbali za mikono zinazozalishwa na vikundi vya Wasichana Balehe na Wanawake Vijana wa mradi wa *Dreams* kutoka Mkoa wa Shinyanga. Mradi huo unalenga kuwakinga wasichana balehe na wanawake vijana dhidi ya mazingira hatarishi ya kupata virusi vya UKIMWI kwa kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kutembelea maonesho hayo yanayofanyika katika viwanja vya Bunge karibu na Ukumbi wa Msekwa ili kujionea shughuli zinazofanyika pamoja na kuwaunga mkono vijana hao kutokana na shughuli wanazozifanya kwa maana ya kutazama na kununua. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Kundo na Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Kamati hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kuchangia kwenye eneo la *TANROADS* hasa kwa kuwa ninatambua umuhimu mkubwa wa miundombinu ya barabara ndani ya Taifa letu katika kuchangia Pato la Taifa na kipato cha mtu mmoja mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto sana katika miradi ya barabara. Laiti kama kila Mbunge angesimama hapa, hata tukianza kumuuliza Mbunge mmoja mmoja hapa, kila mmoja atazungumza changamoto ya barabara kwenye eneo lake, kwa sababu hii imekuwa ni changamoto ya nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya asilimia 80 ya mizigo na abiria ndani ya nchi yetu wanatumia barabara. Hivyo, tunajua barabara ina mchango mkubwa katika kuchangia Pato la Taifa letu. Kama walivyozungumza Wajumbe wengine wa Kamati, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya fedha za miradi ya maendeleo ndani ya *TANROADS*. Changamoto hii imesababisha miradi mingi kutokukamilika kwa wakati, na miradi mingi haijatekelezwa kabisa kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha ndani ya *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii ya uhaba wa bajeti ya miradi ya maendeleo ndani ya *TANROADS,* imeleta athari kubwa. Athari hizi zinaonekana na tumeendelea kushauri kila tunaposimama kwenye Bunge hili. Athari kubwa ambazo tunaziona ni kuongezeka kwa gharama kubwa ya miradi. Miradi imekuwa ikiongezeka gharama kila kunapoitwa leo kutokana na ufinyu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023, madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri yalikuwa ni shilingi bilioni 701, lakini mpaka sasa ninavyozungumza madeni ya wakandarasi na Wahandisi Washauri ni shilingi bilioni 889. Yaani kila kunapoitwa leo, *figure* inaendelea kuongezeka, gharama ya miradi inaendelea kukua na mwisho wa siku tunatekeleza miradi kwa gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha ni kodi za Watanzania. Mimi nadhani hata Watanzania wanahuzunika wanaposikia hizi taarifa huko nje. Hali siyo nzuri. Kuna wakati lazima tujifunze hata kwa mataifa mengine, wanafanyaje katika kutekeleza hii miradi ya barabara? Mbona kuna maeneo gharama haziongezeki lakini sisi kwenye nchi yetu gharama zinazidi kuwa kubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza mwaka huu 2024, hii ni Februari, tusishangae kufika Desemba hii *figure* ikawa imeongezeka kutoka kwenye shilingi bilioni 889 huko tutaenda kwenye matrilioni. Hii hali ni mbaya mno! Kwa asilimia kubwa miradi inakwama, lakini ukiangalia kwenye uhalisia, baadhi ya maeneo kuna miradi inaendelea kutekelezeka. Kama kuna miradi inaendelea kutekelezeka na mingine imeshatekelezwa, hii ina maana bado tuna tatizo kubwa kwenye suala la madeni ya wakandarasi na wahandisi washauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kama Serikali tujipange, ni namna gani tunakabiliana na hii changamoto? Kwa sababu hakijawa kilio cha leo, kila tunaposimama; mimi nina kumbukumbu kwenye michango yangu, kila ninaposimama nazungumzia suala la wakandarasi. Madeni ya wakandarasi yamekuwa ni tishio kwa Taifa letu. Ni lazima Serikali tuone ni namna gani tunakabiliana na hii changamoto ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosheleza kwenye *TANROADS* ili tuweze kuziepuka hizi changamoto, kwa sababu mwisho wa siku tunaenda kuua uchumi wa Taifa letu kwa mikono yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumza kwenye changamoto ya bajeti kwenye suala la *TANROADS*. Tumeendelea kusema hapa, katika bajeti ya mwaka 2023/2024 tumepitisha shilingi trilioni 1.4 kwenye miradi ya maendeleo. Hali siyo shwari. Nimesema kila mtu akisimama hapa ataelezea uhalisia kwenye mkoa wake. Barabara zinakatika, madaraja yanabomoka, hali ni mbaya, mawasiliano yanakatika hasa ukizingatia hali ya mvua tuliyonayo sasa hivi. Hali inazidi kuwa mbaya kwenye maeneo ya barabara na fedha hatuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuvuka na kutoka salama hapa, ni lazima tutenge shilingi trilioni tano ili shilingi trilioni tatu iende kwenye miradi ya maendeleo ya barabara na shilingi trilioni mbili iende kwenye ukarabati. Hali ni mbaya! Barabara zimetengenezwa kwa gharama kubwa na fedha nyingi, lakini zinaendelea kuharibika kwa sababu hata fedha ya ukarabati haipo. Ni lazima tuliangalie hilo, hali ni mbaya sana kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumza jambo la pili kuhusu suala la fidia kwa wananchi ambao wamepitiwa na miradi hii ya barabara. Ukitoka Tunduma ukapita kwenda Rukwa pale, ni miaka ya 2000 huko wananchi walishachorewa '*X*' za kijani na wakaambiwa Serikali inakuja kuwalipa fedha. Wananchi hao wamekaa wakisubiri Serikali ije iwalipe fedha, hawawezi kuendeleza maeneo hayo, hawawezi kufanya chochote kwenye hayo maeneo, hawawezi kuendeleza shughui zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia miaka ya 2000 ni umri wa mtu sasa hivi, mtu mzima. Huyo ameolewa sasa hivi ana watoto. Hii hali ni mbaya, hebu Serikali mtuambie kama mna uwezo kweli wa kulipa gharama za fidia kwa wananchi hawa ili ikiwezekana kama Serikali mtashindwa, wananchi mwape ruhusa ya kuyaendeleza maeneo yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, kwa sababu mwisho wa siku tunaangalia tu gharama za ulipaji wa fidia ndani ya nchi

nzima ni shilingi trilioni 7.5. Hebu Serikali tuambieni, mna uhakika wa kukifanya hiki? Je, hao wananchi mliowachorea '*X*' za kijani mna uhakika wa kwenda kuwalipa? Kama uhakika haupo, waambieni wananchi wayaendeleze yale maeneo. Tusiwakwamishe wananchi wetu. Hali siyo nzuri, wananchi wanalia huko, hawana tumaini kabisa kwamba Serikali je, itakuja? Mwisho wa siku isije ikatokea Serikali mnawaambia hao wananchi endelezeni maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi miaka 20 umemchelewesha mwananchi hajafanya chochote, utamlipa fidia? Waambieni wananchi ukweli. Kama Serikali hamna uwezo wa kuwalipa fidia, wayaendeleze maeneo yao kwa kufanya shughuli zao kama kawaida, kuliko kuendelea kuweka '*X*' zenu za kijani pale na hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hali inawaumiza sana wananchi wetu, kwa sababu mwisho wa siku wanabaki wanayatazama tu maeneo, hawawezi kufanya chochote. Hii siyo sawa. Ili tukomeshe haya, tunaomba sana bajeti ya Wizara ya Ujenzi iongezeke sasa hivi ili tuweze kuona matokeo yaliyo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Sheria ya *PPP* iko kwako, waacheni *TANROADS* watengeneze barabara zilizoharibika. Barabara mpya jengeni kwa pesa za *PPP*. *Very simple*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kundo, jiandae na Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Mbarawa na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya sekta ya mawasiliano yanachangiwa kwa kiasi kikubwa sana na Kamati hii ya Miundombinu. Hivyo nawapongeza sana na tunaendelea kuwashukuru sana kama Serikali kwa kuendelea kutushauri na kutusimamia, na pale ambapo tutahitajika tutashirikiana vizuri ili kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea maeneo mawili. Eneo la kwanza ni safari ya Tanzania kuelekea kwenye uchumi wa kidijitali. Uchumi huu unahitaji miundombinu ya kidijitali, na miundombinu hii ni pamoja na ujenzi wa mikongo ukianzia mkongo wa baharini, mkongo wa Taifa, *last mile connectivity* ambayo inahusisha minara pamoja na *fiber* mlangoni kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya nini? Upande wa Mkongo wa Baharini Serikali inaendelea kuvutia wawekezaji ili tuweze kuwa na mikongo mingi ili kuhakikisha kwamba tunashusha gharama ya matumizi ya *internet*. La pili, ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa, Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani alitoa kiasi cha shilingi bilioni 170 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mkongo wa mawasiliano unajengwa na kufika katika Wilaya nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkongo wa Mawasiliano ni moja ya *ecosystem* katika miundombinu ya mawasiliano. Tunapoanza na mkongo wa baharini, tunakuja mkongo wa Taifa, tunapokuja kwenye *last mile connectivity,* sasa tunafika kwenye minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi cha kuanzia 2021 - 2023 imeweza kutoa fedha za ujenzi wa minara 1,070 yenye gharama ya takribani shilingi bilioni 170.978. Minara ambayo bado ipo katika hatua za utekelezaji ni minara 758 ambapo minara 320 inatokana na fedha za ndani na minara 438 inatokana na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba kuna maeneo ambayo bado yana changamoto na Mheshimiwa Rais anaendelea kutafuta fedha ambazo zitakuja kutatua changamoto katika baadhi ya maeneo. Tayari Mheshimiwa Rais ameshapata fedha kwa ajili ya kuongeza minara mingine 636, lakini katika minara hiyo kuna minara ambayo itaenda kujengwa katika maeneo yenye changamoto ya *TBC*, minara ambayo ni takribani 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo minara tayari imeshajengwa na Waheshimiwa Wabunge wameonesha changamoto ya minara kuwaka asubuhi na mingine inawaka kwa masaa machache baadaye jioni inakuwa haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshatoa maelekezo kuhakikisha kila mtoa huduma anapojenga minara ya mawasiliano cha kwanza ni lazima iwe na huduma ya *internet*. Jambo la pili, ni kuhakikisha kuwe na *source* ya *power* tatu; ya kwanza ikiwa *solar*, ya pili ikiwa betri na ya tatu ikiwa *generator*. Tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo, hata kama *solar* itakosa nguvu, basi betri itaweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongea kidogo kuhusu suala la ujenzi wa Chuo cha *ICT*. Mheshimiwa Rais tayari ameshaelekeza na Mshauri Elekezi ameshafika kutoka *South Korea* na kazi ameshaanza tayari toka tarehe 29 Januari. Hivyo tutegemee kwamba ukamilishaji wa chuo hiki kitawasaidia Watanzania kuwajenga katika maarifa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile suala la kuwa na *ICT hubs,* tayari Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa kiasi cha dola milioni sita kwa ajili ya kujenga *ICT hubs* katika maeneo ya Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Lindi, Mwanza, Arusha pamoja na Zanzibar. Lengo ni nini? Lengo ni kuandaa vijana wetu wawe tayari kuingia katika soko la kidijitali ili Tanzania yetu ifikie uchumi wa kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongea kitu kidogo kuhusu suala la teknolojia zinazoibukia. Mheshimiwa *Engineer* Ulenga ameongelea kuhusu *attacks* katika *critical infrastructure*. Ni kweli kabisa, nchi za jirani hivi karibuni wawepambana na changamoto hii, lakini Serikali yetu tayari imeshaanda miongozo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali yetu imeshandaa miongozo mitano na tunapitia sera zetu ili kuhakikisha kwamba tunapambana na majanga haya yanayotokea. Mpaka sasa pamoja na kwamba nchi jirani zimeshapambana na haya majanga ya *attack,* Serikali yetu bado iko salama, mifumo yetu bado iko salama, lakini Serikali haitabweteka, itaendelea kuweka mkakati wa kuhakikisha kwamba mifumo yetu inaendelea kuwa salama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa mchango mzuri, lakini nanyi mjiandae na *artificial intelligence*. Sasa hivi bila *governance* au *regulations* za kitu hiki kipya, watu wameshaanza *voice scam*, watu wameshaanza *facial scam,* watu wameshaanza kufanya kila aina ya kutengeneza vitu kwa *artificial intelligence* bila kuwa na *regulation*. Nchi nyingi sasa zinaweka sheria ya matumizi ya *programe* hii. Kwa hiyo, naomba hilo nalo mlitilie maanani.

Mheshimiwa Bashungwa, jiandae Mheshimiwa Mbarawa na mtoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Hoja ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utendaji wa Serikali. Naanza kwa kukushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya katika majukumu yako

ya Unaibu Spika. Pia nakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya ya uwakilishi wa wananchi wako wa Jimbo la Ilala. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kakoso kwa wasilisho zuri la hoja ya Kamati. Pia, nampongeza Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mama yetu, Mheshimiwa Anne Kilango pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushauri Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara na taasisi zake, tunaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano. Pia tunawashukuru sana kwa ushirikiano mnaotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja hii zikiwemo hoja zinazohusu Wizara ya Ujenzi. Naomba kutumia muda niliopewa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya masuala ambayo yamejitokeza mara nyingi kutoka kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango, pamoja na Waheshimiwa Wabunge mmetoa pongezi kubwa…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya Kiti, naongeza muda mpaka nusu saa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamepongeza Serikali na Mheshimiwa Rais wetu, mpendwa wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kazi kubwa inafanyika ya kujenga miundombinu nchini ikiwemo miundombinu ya barabara pamoja na madaraja, na wakasema mvua za El-Nino zimeleta dosari kubwa ya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *concern* ya Waheshimiwa Wabunge, wote tunakubaliana kwamba miundombinu imara inajenga uchumi imara na Serikali inatambua hilo. Ndiyo maana pamoja na changamoto zinazojitokeza kipindi hiki ambacho tunapata Mvua za *El-Nino* mkakati wa Serikali ni mara moja baada ya miundombinu kuharibika ni kufanya kila linalowezekana kurudisha mawasiliano kama *emergency response* huku tukiangalia namna ya kuboresha miundombinu hii kwa maana ya mkakati wa *medium to long term*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia, Serikali katika bajeti hii tunayoandaa na bajeti zijazo, yale masuala ambayo yameleta dosari kubwa ambayo yanahitaji bajeti kubwa, tutayazingatia katika bajeti hii tunayoandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *concern* ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Mvua za *El-Nino* na barabara nyingi kufikia muda wake kwa maana ya matumizi ya barabara, umeleta hitaji kubwa la bajeti, limetajwa hitaji la shilingi trilioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nawaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mahitaji haya kwa upande wa Serikali na *nature* ya ujenzi wa barabara na madaraja mahitaji huwa hayatekelezwi kwa wakati mmoja yaani hatuwezi kusema tutapata shilingi trilioni tano leo hii tutimize mahitaji yote; lakini *incrementally* kwa *phases* wote tukishakubalina kama hapa tulivyochangia basi hata kwenye uzingatiaji wa bajeti na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa,

Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji na Mipango Profesa Mkumbo yuko hapa. Wiki hii nakutana na timu yake ili kuangalia kwenye miaka 25 inayokuja ya *Development Plan* ya nchi, masuala haya pia tuyaangalie ikiwemo suala la kujenga barabara za kutumia *PPP* na Mheshimiwa Rais pamoja na Waheshimiwa Wabunge, jambo hili mmelijadili na kuona sasa katika kujenga miundombinu, lazima tuwe

wabunifu na tutumie kila aina ya njia ikiwemo njia ya *PPP* kuboresho miundombinu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Mkumbo na timu yangu ya Wizara pamoja na timu yake, wiki hii tunakaa kuangalia *Development Plan* inayoisha mwakani, ile ya 2025 kwenda 2050, maeneo mahususi ya kimkakati yanayohusu ujenzi wa barabara pamoja na madaraja zikiwemo Barabara za *Trunk Road* ambazo zimetajwa na Kamati, kupitia mchango wa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti. Barabara 71 ambazo zimeisha muda wake, pia tunaangalia kupitia huo Mpango wa miaka 25 tunayoiandaa, baadhi ya barabara tuangalie namna ya kujenga kwa njia ya *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kwa mfano Barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja hapa Morogoro, kuja Dodoma hapa kupitia Morogoro tayari tunazungumza na wabia ambao tunaweza tukaingia nao kujenga *Express Way* kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, Makao Makuu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ningependa kulisema, barabara ambazo tutajenga kwa njia ya *PPP*, hatutaathiri barabara zilizopo ili mwananchi yeyote ambaye anataka kuendelea kutumia barabara zilizopo, maisha yaendelee. Pia ku-*support* uchumi wa nchi kwa kujenga barabara ambazo iwe ni mizigo, malori na watu ambao wanahitaji kwenda kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji uchumi, basi awe na *option* kutumia barabara iliyopo au barabara kwa njia ya *express*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yote haya Waheshimiwa Wabunge tunayachukua lakini tayari tumeanza kuyafanyia kazi. Kuhusu Wakandarasi wazawa, limezungumziwa suala la madeni kuchelewa kulipwa. Katika hili, Mheshimiwa Rais tunamshukuru, maelekezo yake Wizara ya Ujenzi kukaa na Wizara ya Fedha, tayari tumeshajiwekea utaratibu wa kupunguza madeni ya wakandarasi

wazawa kila mwezi na deni la wakandarasi wazawa mpaka hivi sasa tumelipunguza mpaka Disemba, mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni ambalo limebaki mwezi huu wa Februari, kupitia Wizara ya Fedha, wametuahidi tutaendelea kutoa *commitment* ya kulipa shilingi bilioni 50 kila mwezi ili takribani shilingi bilioni 115 ambayo imebaki kwa wakandarasi wazawa, kufika mwezi Aprili, tuwe tumekamilisha ina maana tutakuwa tuna *certificate* mpya za kuanzia Januari na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa maelekezo yake na kupitia Wizara ya Fedha, tunaendelea kulifanyia kazi; lakini hatujaishia hapo kwenye wakandarasi wazawa, ni dhamira ya Mheshimiwa Rais kuona uchumi wa nchi kwa kadri inavyowezekana, tunakuwa tuna mikakati endelevu ya kuwezesha wakandarasi wazawa. Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati ananiapisha kuja kwenye Wizara ya Ujenzi, niliunda Kamati ya kuchambua mapungufu yaliyopo ya wakandarasi wazawa yakiwemo masuala ya mitaji, mitambo, uwezo wa kusimamia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imeshakamilisha tunachokiita *local content strategy* ya wakandarasi wazawa. Ninaamini kupitia Ofisi yako, wakati wa Bunge la Bajeti, tukipata nafasi ya kuwasilisha kwa Bunge *local content strategy* tuliyoiandaa kwa ajili ya wakandarasi wazawa, tutapata ushauri ili Mkakati huu sasa ukawe ndiyo *Master Plan* ya kuwasaidia Wakandarasi Wazawa. Yamo masuala ya kulegeza vigezo ambavyo vilikuwa …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, malizia.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumalizia, namalizia na suala la miradi ya *EPC + F*. Niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, Wakandarasi saba ambao wamepata miradi hii, wanafanya mapitio ya *design* ambazo zilifanywa na *TANROADS* mwaka 2017 ili waweze kuwa na taarifa sahihi kuhusu

majenzi ya barabara hizi na jambo hili liko hatua za mwisho, kwa hiyo, miradi yote saba tutaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, suala la fidia, zimesemwa takribani shilingi trilioni 7.5. tunaendelea kufanya uchambuzi ndani ya Serikali ili kuona namna bora ya kuendelea kufidia maana siku zote barabara tumezijenga kwa utaratibu wa kufidia wananchi ili tuweze kujenga Miundombinu ya Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu suala la fidia limekuwa *accumulative* na la muda mrefu, tunafanya uchambuzi wa kina ili maeneo mengine ambayo yatasaidia kuokoa usumbufu upande wa wananchi lakini pia kupunguza gharama hizi tuweze kuyatumia, barabara tuzijenge lakini pia na wananchi wetu waweze kupata fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mbarawa, jiandae mtoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kusimama mbele yako kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Naendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kutuwezesha na kutupa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Serikali inatambua kwamba, miundombinu ndiyo inakuza uchumi wa nchi yeyote duniani. Ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo matano ambayo nitayatolea ufafanuzi. Eneo la kwanza, ni kuhusu bandari; wachangiaji wote kwa ujumla wamezungumzia bandari. Tunafahamu kwamba, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango kubwa la uchumi na imekuwa ikitegemewa na Tanzania na nchi mbalimbali za Jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumekuwa na ongezeko kubwa la meli pale Bandari ya Dar es Salaam. Hii ni baraka kubwa kwa nchi yetu lakini pia imetupa changamoto kubwa ya kujipanga jinsi gani tutaweza kutatua changamoto hii ili isiweze kujitokeza tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango huo, Serikali imeamua kujenga gati kubwa, lenye urefu wa mita 590 pale Malindi *wharf* ambayo itakuwa na uwezo wa kuwekeza meli mbili kwa wakati mmoja. Hivi ninavyozungumza, tunatafuta Mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo na pesa ipo. Mkakati wa pili ambao tumejipangia, ni kujenga bandari ya kisasa kwa ajili ya ushushaji wa mafuta pamoja na matenki ya kuhifadhia mafuta. Mradi huu unaendelea. Hivi sasa ninavyozungumza, tayari Mkandarasi tumeshampata kwa ajili ya kazi hiyo na tutatumia takribani shilingi bilioni 560 kwa ajili ya kujenga matenki hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili itakayofuata ni kujenga bandari hiyo huko Bagamoyo kwa ajili ya kuteremshia mafuta ili kupunguza msongamano wa meli za mafuta ambao sasa hivi upo. Hatua ya tatu ambayo tumeendelea nayo kupunguza msongamano unaoendelea, ni kujenga bandari Gati namba 13 mpaka 15. Sasa hivi tuko katika hatua ya kupitia *design* ya mradi huo ili tuweze kuitangaza, tupate mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuishia hapo tu, lakini huko Mtwara, tunajua hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la meli na tumeamua sasa kujenga Bandari Maalum kwa ajili ya mizigo michafu yaani *dirty cargos*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza tayari tuko katika hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa gati hilo. Hatukusimama hapo tu lakini karibu kila sehemu ya nchi yetu tunajenga Bandari ili kuifungua Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza biashara kati ya nchi yetu na nchi za Jirani. Kwa mfano, huko Mwanza, pale Mwanza *south*, tunajenga Bandari ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbalimbali na gharama yake takribani shilingi milioni 24. Huko Kemondo, Kagera tunajenga Bandari ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbalimbali za mizigo na za abiria na inagharimu takribani shilingi bilioni 19.6

Mheshimiwa Naibu Spika, huko vilevile Bukoba pale Mjini tunajenga bandari nyingine ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbalimbali. Huko Ziwa Nyasa, *Mbamba Bay* pia tunajenga bandari ya kisasa ambayo inagharimu takribani shilingi bilioni 75 kwa ajili ya abiria na mizigo ambayo Bandari hiyo wataitumia watu wa Malawi pamoja na watu wa Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuipa *TPA* na Taasisi zote za Serikali pesa ya kutosha kuhakikisha kwamba tunaijengea Miundombinu ya kisasa kuhakikisha, inakabiliana na ongezeko kubwa la mizigo inayotokea kwenye bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo kwa upande wa Miundombinu lakini Serikali tunajua unaweza kujenga miundombinu ya kisasa lakini bila kuboresha utendaji, haitosaidia sana. Kwa vile Serikali tumejipanga kuhakikisha kuwa tunaboresha utendaji kazi wa bandari zetu na hivi tunavyozungumza, tumeona ufanisi mkubwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ninalotaka kulizungumzia ni sehemu ya *marine service*. Kwa kweli kama Kamati walivyosema, kuna miradi mingi ya zamani ambayo bado haijamalizika kwa sababu mbalimbali lakini tunahakikisha kwamba tunaendelea kuimaliza ili imalizike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hivi majuzi tu tumesaini mradi wa kwanza kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha ujenzi wa meli huko Kigoma ambacho kitakuwa kina uwezo wa kujenga meli mbalimbali. Pia tumesaini mradi wa meli ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua mizigo tani 3,500 ambayo itahudunmia eneo la Kigoma, Congo pamoja na Zambia kwa ajili ya kupeleka mizigo. Tunafanya mambo haya yote ili kuhakikisha Bandari ya Dar es Salaam, inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaendelea na ukarabati wa meli ya *MV.* Sangara ambayo inagharimu takribani shilingi bilioni 9.016, pia mefikia asilimia 92 na tunategemea itamalizika mwezi Mei, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaifanyia utafiti ili tuweze kuitengeneza meli ya *MV.* Mwongozo. Ilikuwa na tatizo la *stability* ambayo hivi sasa wataalam wanajaribu kuifanyia utafiti kuona jinsi gani ambavyo tutaweza kuitengeneza ili na yenyewe iweze kufanya kazi ya kupeleka mafuta kutoka Tanzania kwenda *DRC* pamoja na Nchi ya Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia huko Kigoma tunaendelea, tumefunga saini mkataba kwa ajili ya ukarabati wa meli ya *MV.* Liemba ambayo ni meli ya siku nyingi na ukarabati huo utagharimu takribani shilingi bilioni 33.38. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Mwanza vilevile kama mnavyojua tunajenga meli ya kisasa *MV.* Mwanza. Tunategemea itamalizika mwezi Mei, 2024 na itagharimu kakribani shilingi bilioni 127.27 na imefikia asilimia 93, kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la *LATRA*, tunakubaliana na Kamati kwamba tupitie kanuni mbalimbali zilizopo ili tuweze kuboresha ufanisi wa utendaji wa *LATRA* na hii tutaifanyia kazi. Pia kuna changamoto ya wafanyakazi, tutaendelea kuajiri wafanyakazi wengi na wenye ujuzi ambao utaongeza ufanisi wa *LATRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAA* tunajipanga kuboresha au kutengeneza Sheria Mpya ya Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege. Tunaamini Sheria hii italeta mabadiliko makubwa kwenye Sekta ya Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuhusu *Air Tanzania*, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, *Air Tanzania* itakwenda maeneo yote ya nchi yetu. Tunajenga viwanja vya ndege vya kisasa na tunahakikisha Viwanja vyote vya ndege vya kisasa vinavyojengwa, vitakuwa na taa ili ndege ziweze kwenda masaa 24 kwa siku. Hivi tunavyotegemea, mwisho wa mwezi huu tutapata ndege moja ambayo itaongeza ndege tulizonazo na tutaongeza ufanisi wa *Air Tanzania* katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa nne Mungu akitujaalia tutapata ndege nyingine ya *Dream Liner* ambayo pia itaongeza ufanisi na usafiri katika maeneo mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mtoa hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nawashukuru sana wachangiaji wote ambapo wamebahatika kuchangia hoja ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Tumepata wachangiaji 16 wakiwemo na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Waziri, ambao wametoa hoja na ufafanuzi wa jinsi gani utekelezaji watakavyoufanya na ulivyotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazingatia yale ambayo Serikali ilikuja ikayaleta mbele ya Kamati na wakati huohuo, ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Anne Kilango amezungumzia suala la Miradi ya Maendeleo iliyoletwa na

Serikali ya barabara na Miradi ya Maendeleo ya upanuzi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumzia juu ya tatizo la barabara. Kwenye eneo la barabara, *TANROADS* imezidiwa, uhalisia jisi ulivyo, ili barabara za kwetu ziweze kuimarika na ziweze kufanya kazi, *TANROADS* inahitaji ipatiwe na Serikali bajeti isiyopungua shilingi trilioni tatu kwa ajili ya kujenga Miundombinu na kuimarisha barabara ambazo zilishatangazwa kwa ajili ya kuendeleza miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi ambao walikuwa na hamu kubwa ya kuangalia barabara zao zilizoahidiwa mbele ya Bunge Tukufu, asilimia kubwa hawajapata barabara zinazojengwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kuhakikisha kile ambacho kilipitishwa na Bunge kinafanyiwa kazi; lakini tuna tatizo la Mfuko wa Barabara ambao hauna fedha za kukidhi mahitaji. Mfuko wa Barabara uwezo wake kwa sasa unakusanya shilingi bilioni 850, kati ya hizo fedha, zinazoenda moja kwa moja kwenye miradi ya matengenezo ya barabara ni shilingi bilioni 600 ndio zinazoenda kwenye upande wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji halisi ya barabara zilizoharibika hapa nchini, zinahitaji matengenezo ya shilingi trilioni mbili. Kwa hiyo, kwa ujumla, Wizara ya Ujenzi ili tuweze kwenda vizuri, tuna uhitaji wa shilingi trilioni tano kwa ajili ya matengenezo ya miradi ya barabara mipya na iliyoanzishwa na Serikali na shilingi trilioni mbili ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara ambazo zimeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingi nchini zilishapitwa na wakati na mfano wametolea Waheshimiwa Wabunge, barabara ya kutoka Dodoma – Iringa, ile barabara ilishakwisha, barabara ya

kutoka Morogoro – Dodoma, barabara hii nayo ilishapitwa na wakati, muda wake umeskwisha, hali kadhalika, Barabara ya kutoka Chalinze – Kilimanjaro, Kilimanjaro – Arusha, hizi zote zilishakwisha muda wake. Tunayo barabara ya kutoka eneo la Makambako – Songea, tuna barabara ya kutoka Dar es Salaam – Mtwara, hizi barabara zote zinahitaji matengenezo makubwa sana. Eneo hili, tunaishauri Serikali, kwenye Mpango wa Bajeti waje na Bajeti ambayo itahimili matengenezo ya barabara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kwa kina, ni suala la kushindwa kuwalipa wakandarasi kwa muda. Eneo hili, Serikali inapata hasara kubwa sana kwa sababu tunaweka Wakandarasi, wanashindwa kuwalipa kwa wakati na badala yake sasa kunaingia riba ambazo zinakuja kuwalipa Wakandarasi ambazo zinafanya gharama ya barabara kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali kupitia Wizara, izingatie na waangalie hili kwamba ni suala muhimu sana ili tunapokuja kwenye mwaka wa fedha, tuje na bajeti ambayo itahimili kuweza kukamilisha hii miradi iliyotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni fidia za barabara, kwenye Wizara ya Ujenzi nchi nzima Serikali imeweka alama za barabarani ambazo wananchi wanahitaji wapishe miradi. Bahati mbaya sana wapo watu ambao wamewekewa alama za kupisha miradi hiyo zaidi ya miaka kumi wana matumaini ya kuendelea kupata fidia. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge kwa ripoti za Wizara, zaidi ya shilingi trilioni saba zinahitaji kulipa fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati, tunaishairu Serikali maeneo ambayo wanayaona hawana uwezo wa kuweza kuwalipa fidia na miradi ile haitaweza kwenda kwa wakati, wawaruhusu wananchi waendeleze maeneo yao kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Wizara ya Ujenzi, tunaiomba izingatie mfumo wa Waheshimiwa Wabunge ambao wanaishauri Serikali. Ili tuweze kwenda vizuri wizara ijipange vizuri kwa ajili ya bajeti ijayo angalau ifikie hizo trilioni tano. Trilioni mbili kwa ajili ya matengenezo ya barabara na trilioni tatu kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaipongeza Serikali kwa jitihada ni kwenye Taasisi ya *TBA; TBA* wameanza sasa kukusanya madeni yao, madeni ambayo asilimia kubwa wapangaji wamekuwa wakiishi kama nyumba za kwao binafsi ambazo haziitaji kulipa kodi. Walipoanza jitihada za kuwadai wananchi, zimekuwa na tija kidogo. kwa bahati mbaya taasisi za Serikali, watumishi wa Serikali ambao wanakaa kwenye nyumba za *TBA* bado hawajalipa hizo kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ule mfano uliotolewa kwa sababu na Waheshimiwa Wabunge wametolewa kwenye hizo nyumba tunaomba na taasisi zile za Serikali wafanye kama walivyofanya kwa Waheshimiwa Wabunge. Hili litasaidia *TBA* iweze kukaa vizuri na ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada ambazo amezifanya. Tunaomba nguvu uliyoitumia kutoka kuwatoa Waheshimiwa Wabunge na wengineo kawaondoeni na watumishi wa Serikali ambao hawajalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya uchukuzi; tunaipongeza Serikali, tunajua jitihada zipo kubwa sana zimefanywa na Serikali kwenye miradi ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana suala la kuiwezesha *TPA* ili iweze kuwa na nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote *wharfage* wanalipwa mamlaka husika ya bandari. Sisi tunakusanya hela zote tunazipeleka Serikali Kuu, na wakati huo huo tunapoanza kujenga miradi ya maendeleo tunaenda kuomba. *TPA* ina uwezo wa kutengeneza fedha nyingi sana endapo kutakuwa na utashi. Tunaomba na

kuishauri Serikali Mheshimiwa Waziri anapokuja mwakani kwenye bajeti yake, awaachie *TPA* waweze kujenga gati kwa kujitegemea wao. Wana nafasi, tumewasikiliza tumewaelewa na tumefananisha na nchi zingine ambavyo wanafanya. *TPA* wana nafasi ya kuweza kujenga gati kuanzia ile gati sifuri wakawa na gati tano ambazo wanaweza wakajenga kwa nguvu za kutumia nafasi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeishauri Serikali angalau mapato ya *wharfage* watoe kila mwezi waachie shilingi bilioni 35 ambazo zitawafanya waweze kujenga na watumie taasisi za fedha wajenge wao wenyewe; na zile fedha zitakuja kuleta *return* kubwa sana kwa Serikali kwa sababu gati moja ina nafasi ya kuweza kuzaisha bilioni 600. Kwa hiyo mkiwa na gati takriban tano zimejengwa Serikali itapata fedha nyingi sana kama mapato ya kodi pamoja na mapato ya ushuru wa gati yenyewe; kwa sababu tutakuwa tayari tumetengeneza mifumo sahihi. Naomba Serikali waliangalie hili kwa sababu ukitaka kumkamua ngombe aweze kuzalisha vizuri ni lazima umpe malisho ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la sekta ya uchukuzi, kuhusu Mradi wa *SGR*. Tunaipongeza Serikali, imejenga miradi mikubwa wa SGR kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Tabora – Isaka – Mwanza. Leo hii tena tumeanza mradi mkubwa wa kutoka Tabora – Kigoma na lile tawi la kutoka Msongati kwenda eneo la nchi ya Burundi. Tunaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuanzisha miradi hii. Tunaiomba Wizara iweke usimamizi mkubwa wa miradi imechukua muda mrefu sana kukamilika. Mradi unapochelewa kuchukua muda wa kukamilika tuliokubaliana nao kati ya Serikali na wajenzi inaifanya Serikali kutumia gharama kubwa za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili mlifanyie kazi na Serikali kupitia Wizara husika iwasimamie wakandarasi na wapunguze tatizo lililopo, hasa kwenye kampuni inayojenga reli kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Tabora wahakikishe

haki za watanzania wanaofanya kazi walipwe na kusiwe na malalamiko ya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya uwanja wa ndege. Viwanja vya ndege vinasimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kupitia Serikali. Tunaomba miradi hii iweze kusimamiwa ipasavyo na wakandarasi wale ambao wanadai waweze kulipwa haki na stahiki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Kampuni ya Meli *(MSCL)*. Kampuni hii imejenga meli, meli zile ambazo zinajengwa na Serikali; na tunaipongeza Serikali kwa jitihada ambazo zinafanywa za mara kwa mara za kuinusuru kampuni ambayo ilikuwa ilishakufa kabisa lakini Serikali tumeona nguvu yake iliyofanya; sasa tunaomba muwasimamie ile miradi ambayo imepitishwa na Serikali tuhakikishe inafanyiwa kazi ili kampuni ile iweze kusimama. Muda wote inategemea kupata ruzuku kutoka Serikalini. Tunaomba Serikali itoe fedha ya kutosha, wakamilishe ili ile kampuni iweze kusimama na ijitegemee yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Ziwa Tanganyika tuna miradi ya maendeleo ya ujenzi wa meli mpya, ya ukarabati wa meli ya *MV* Liemba na *MV* Mwongozo. Tunaomba jitihada za Serikali zifanyike haraka kuhakikisha lile ziwa nalo linapata uhalali wa kutumika vizuri kama maziwa mengine yalivyopewa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tunao Mradi wa Mkongo wa Taifa. Mkongo wa Taifa kwa sasa ni eneo ambalo Serikali wanaweza wakapata fedha za kiuchumi. Bahati mbaya sana, bado kuna maeneo ambayo hayajawekewa uzito mkubwa sana. Kamati imeshauri mradi wa kuunganisha Mkongo wa Taifa na nchi ya *DRC Congo* uharakishwe kwa sababu eneo hilo tukilishika tutakuwa tumetengezeza fedha ambazo Serikali itanufaika kama ambavyo sasa hivi Serikali wanapata fedha kupitia nchi ya Rwanda; wanalipwa kwa ajili ya uwekezaji wa Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala la miradi ya minara ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi walifurahia sana kupata minara 758. Mpaka sasa minara iliyokamilika ni minara 15 tu. Kasi ya uendelezaji wa ujenzi wa minara ni ndogo. Tunaishauri Serikali ikasimamie kuhakikisha minara yote ambayo iliwekewa mpango mkakati kwa mwaka wa fedha unaoisha sasa iweze kukamilika, na tunapokuja kwenye bajeti ijayo Serikali iwe na majibu ya msingi ya kutueleza nini kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TCRA* tunaishauri *TCRA* kuhakikisha wawe wabunifu ili waweze kukabiliana na changamoto ambazo zipo kwenye teknolojia ya mitandao, kwani kila siku kuna mabadiliko na watu wanafanya ufundi wa kila siku kuhakikisha nchi wanaiweka katika mazingira ambayo ni tofauti. Tunawapongeza, wamefanya jitihada sana kupitia Serikali. Maeneo ambayo wengi wametetereka kwa ku-*attack* mitandao kwa Tanzania tumekuwa salama hasa kwenye mifumo ile ya kifedha. Tunaomba jitihada zile ziendelee kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna tatizo kati ya Serikali na *TCRA* na watu wanaomiliki mitandao wahakikishe yale ambayo ni maudhui ya Kitanzania yaweze kuwepo, na mfumo ule wa kupeleka vitu ambavyo vinaleta uchochezi na taharuki kwa nchi. Hivyo viweze kutolewa ili kuhakikisha nchi inakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mawaziri kwa majibu ambayo wameyatoa tunaomba wakaongeze kasi kuhakikisha miradi ile ambayo Watanzania wanaitegemea iweze kufanya kazi na Watanzania wote waweze kunufaika. Kuhusiana na miradi ya barabara, naleta msisitizo mkubwa sana kwamba huko ndiko kwenye siasa ya nchi yetu. Tunajua kwamba nchi inapita katika kipindi kigumu barabara zimekuwa mbovu kwa sababu ya hali ya hewa. Hata hivyo, kama Serikali mkisimama vizuri mkashirikiana na Waheshimiwa Wabunge na mkachukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge mnaweza kufika kabisa kwenye mazingira ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninawashukuru sana Wabunge wote ambao wametoa mchango wao. Ninaamini mchango wenu utakuwa ni kumbukumbu sahihi na utakaotoa dira kwa Serikali kuweza kuyafanyia kazi mawazo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati imemaliza kazi yake sasa nawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023 na mapendekezo yake.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Natumia nafasi hii kwanza kukupongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Kamati yako kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana na mnastahili kupongezwa kwa ujasiri lakini kwa uzalendo wa Taifa lenu. Nawapongeza Mawaziri na Serikali kazi nzuri na majibu sahihi ambayo mmetoa, tuna Imani na ninyi, tunajua tutafika na ninyi.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.31 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 6 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*